# Nipashe

Jumatatu Novemba 25, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580084

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Nipashe Spotika

WANASOKA 10 WANAOLIPWA PESA NDEFU ZAIDI DUNIANI UK.16&17

ISIKUPITE

MECHI ZA KWANZA ZA MOURINHO

KIMGONGOMGONGO...

UKURASA 13



RIPOTI MAALUMU

## Ongezeko la watu linavyoiweka sekta uhifadhi, utalii njia panda

UKURASA 4

# Mkanganyiko uchaguzi mitaa

UKURASA 2




## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MTANZANIA ATEULIWA NAFASI NYETI YA UN**

MTANZANIA Elizabeth Maruma Mrema, ameteuliwa kuwa Kaimu...

UKURASA WA 3

**MAMIA BAVICHA WAJITOSA UCHAGUZI**

NI mchuano mkali, hivyo ndivyo unavyoweza kusema baada ya...


## Aliyekuwa mgombea mitaa adaiwa kuchinjwa

UKURASA 3






Ofisi za serikali za mtaa wa Kilimahewa, Kata ya Wazo Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, zikiwa zimefungwa. Nje ni askari waliokuwa vituoni na wengine ni wananchi waliofika kupiga kura na kujulishwa kuwa wagombea wa CCM wamepita bila kupingwa. **PICHA: SALOME KITOMARI. Chini;** wananchi wa Mtaa wa Mabambase Kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga wakipiga kura kuchagua viongozi wa Serikali za mitaa. **PICHA: MARCO MADUHU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## JPM azipa taasisi siku 60 kuipa serikali gawio

UKURASA 2




MICHEZO **BIASHARA YATAKA TATU ZA LIPULI** UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mtanzania ateuliwa nafasi nyeti ya UN

**Na Mwandishi Wetu**



MTANZANIA, Elizabeth Maruma Mrema (pichani), ameteuliwa kuwa Kaimu Katibu Mtendaji wa Sekretarieti inayosimamia Mkataba wa kimataifa wa Umoja wa Mataifa wa tofauti za kibiolojia (CBD) yenye makao yake makuu Monteal, Canada kuanzia Disemba 1, mwaka huu.

Uteuzi huo umefanywa hivi karibuni na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres kufuatia kujiuzulu kwa Cristiana Pasca Palmer, raia wa Romania kutokana na sababu za kiafya.

Kulingana na taarifa iliyotumwa kwenye wavuti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la mpango wa mazingira (UNEP), uteuzi huo unatajwa kuwa unaongeza matumaini katika uhifadhi wa masuala ya bayonuai ya kibaiolojia, matumizi endelevu ya baiolojia hizo, na ugawaji wa faida zitokanazo na rasilimali za kijenitiki kwa kuzingatia usawa na haki.

Kabla ya kuteuliwa kwake, Mrema alikuwa Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria katika Makao makuu ya UNEP jijini Nairobi, Kenya ambapo amefanya kazi kwa zaidi ya miongo miwili.

Majukumu yake katika Idara ya Sheria ya UNEP ni pamoja na uratibu wa ujenzi wa uwezo, maendeleo, utekelezaji na pia kufuatilia utekelezaji wa sheria za mazingira na mikutano ya kimataifa ya mazingira. Pia aliongoza masuala yanayohusiana na utawala wa kimataifa wa mazingira.

Mrema ni Mwanasheria kitaaluma na Mwanadiplomasia akiwa na Shahada ya Sheria (LLB) (Hons) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shahada ya Uzamili (LLM) kutoka Chuo Kikuu cha Dalhousie, Canada na Stashahada ya Juu katika masuala ya Uhusiano wa Kimataifa na diplomasia (Summa Cum Laude) kutoka Kituo cha Mahusiano ya Kigeni na Diplomasia jijini Dar es Salaam.

Aidha, Mrema amechapisha nakala kadhaa zinazohusiana na sheria za kimataifa za mazingira, ufuatiliaji na utekelezaji wa mikataba na maendeleo ikiwamo makubaliano kadhaa ya mazungumzo kuhusu hali mazingira ya kimataifa pamoja na miongozo inayotumika sasa na UNEP katika mipango yake ya kujengeana uwezo.

Kabla ya kujiunga na Kitengo cha Sheria cha UNEP mnamo Juni 2014, Mrema alikuwa Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Mazingira, anayesimamia uratibu, shughuli na utoaji wa programu kuanzia mwaka 2012 na kwa mwaka mmoja, pia aliwahi kuwa Kaimu Mkurugenzi wa Idara hiyo.

Mwaka 2004 alipewa tuzo ya Meneja wa UNEP bora zaidi wa mwaka kuwahi kutokea, aliyotambulika kama Tuzo ya Wafanyakazi ya UNEP Baobab kwa utendaji bora na kujitolea kufikia malengo ya UNEP.

Mnamo mwaka wa 2009 aliteuliwa kuwa Katibu Mtendaji wa UNEP/ Sekretarieti ya Mkataba juu ya Uhifadhi wa wanyamapori wanaohama (CMS)

Kabla ya kujiunga na UNEP, Mrema alifanya kazi na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Tanzania na hadi anaondoka alikuwa Mshauri Mwandamizi wa Sheria.

Katika kipindi cha uhudumu wake kwenye Wizara hiyo Mrema, pia alikuwa Mhadhiri wa Sheria ya Umma ya Kimataifa na Diplomasia ya Mkutano katika Kituo cha Uhusiano wa nje na diplomasia cha Tanzania.

# Mkanganyiko uchaguzi S/mitaa

**Na Waandishi Wetu**

MKANGANYIKO wakati wa kupiga kura kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa katika vituo mbalimbali vya kupigia kura nchini uliibuka jana baada ya wananchi kujitokeza kwa ajili ya kuwapigia kura wagombea wao kwa mujibu wa Katiba na kukuta baadhi ya vituo vimefungwa.

Ofisi za Serikali za Mitaa ambako ndiko vituo vya uchaguzi vilipangwa na wagombea wa vyama vya upinzani kujitoa, zilikuwa zimefungwa na hakukuwa na tangazo au taarifa yoyote kuwafahamisha wananchi.

Hata hivyo, wananchi walipohoji sababu ya vituo hivyo kufungwa, walielezwa kuwa ni kutokana na wagombea wa maeneo hayo kupita bila kupingwa, hivyo kutofanyika uchaguzi huo.

Vyama vya upinzani kikiwamo Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), ACT-Wazalendo na Chama cha Wananchi (Cuf), vilitangaza kujitoa na kupiga marufuku nembo za vyama vyao kuwekwa kwenye karatasi za kupigia kura.

Vyama tisa vilitangaza kutoshiriki uchaguzi huo vikidai kutoridhishwa na mwenendo uliojitokeza wakati wa uchukuaji na urejeshaji fomu za kugombea nafasi mbalimbali ikiwamo ofisi za watendaji kufungwa na majina ya wagombea kuenguliwa.

Siku chache baadaye Waziri wa Tamisemi, Selemani Jaffo, alitangaza kurejeshwa kwa wagombea wote ambao majina yao yalienguliwa.

Akitangaza hatua hiyo alisema, wagombea ambao hawatashiriki kupigiwa kura ni wale ambao fomu zao hazikuwa na udhamini wa vyama, walio na pingamizi la uraia, ambao hawakujiandikisha kwenye maeneo yao, waliojiandikisha mara mbili, waliojidhamini wenyewe, waliorejesha fomu zaidi ya mtu mmoja kutoka chama kimoja, na waliojitoa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi.

Licha ya agizo hilo, vyama vya upinzani viliendelea na msimamo wa kususia uchaguzi huo.


**SHINYANGA**

Manispaa ya Shinyanga mitaa minne ilifanya uchaguzi huo na katika karatasi za kupigia kura nembo za vyama vya CCM, Chadema, CUF, ACT-Wazalendo, zilionekana kwenye karatasi hizo.

Msimamizi wa uchaguzi wa manispaa hiyo, Rajabu Masanche, alisema wagombea hao ni ambao hawakuwasilisha barua za kujitoa kwenye kinyang'anyiro hicho.

Katika kata 17 za Shinyanga ni nne pekee zilizopiga kura ambazo ni Kambarage, Ibadakuli, Mwamalili

INAENDELEA UK. 8




Rais John Magufuli, akipokea gawio la Sh. bilioni 10.48 kwa Serikali, ikiwa ni sehemu ya faida ya benki ya NMB kwa mwaka 2018 kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Ruth Zaipuna. Katikati anayeshuhudia ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurungezi wa benki hiyo, Margaret Ikongo. Kushoto ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango na Spika wa Bunge, Job Ndugai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JPM azipa taasisi siku 60 kuipa serikali gawio

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

RAIS John Magufuli ametoa miezi miwili viongozi wa mashirika, taasisi na kampuni za umma 187 kutoa gawio kwa serikali na endapo wakishindwa, waondoke wenyewe kwenye nafasi zao.

Alitoa agizo hilo jana Ikulu Chamwino alipokuwa akipokea gawio, michango na ziada kwa mashirika, kampuni na taasisi mbalimbali ambazo zinamilikiwa na serikali.

Alisema serikali hadi sasa imewekeza mtaji wa Sh.Trilioni 59.6 kwa mashirika na taasisi 266, lakini pamoja na uwekezaji mkubwa kuna changamoto ya usimamizi na utendaji mbovu kwenye mashirika ambayo serikali ina hisa mapato yanayopatikana ni kidogo.

Alitolea mfano mwaka 2014/15 serikali ilikusanya Sh. bilioni 130 kutoka mashirika 24 mwaka 2015/16 zilikusanywa Sh. bilioni 249.3 kutoka taasisi na mashirika 25.

"Kutokana na hali hiyo serikali ilianza kuchukua hatua mbalimbali ambazo zimeongeza ukusanyaji ambapo mwaka 2016/17 zilikusanywa Sh.bilioni 677 kutoka taasisi 38, 2017/18 zilikusanywa Sh. bilioni 842.13 kutoka mashirika na taasisi 40, mwaka 2018/19 Sh. trilioni 1.05 kutoka taasisi na mashirika 79," alisema.

Aliongeza: "Tujiulize katika mashirika hayo 266 yaliyochangia 79 na serikali imeweka mtaji wa Sh. trilioni 59.6, yanabaki mashirika 187 hayana habari ya kuchangia, yana Bodi, na

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Mamia Bavicha wajitosa uchaguzi

**Na Enock Charles**

NI mchuano mkali, hivyo ndivyo unavyoweza kusema baada ya vijana zaidi 100 kuchukua fomu za kuwania nafasi mbalimbali ikiwamo nafasi ya Mwenyekiti taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Taifa.

Vijana hao ni kutoka Baraza la Vijana Chadema (Bavicha) maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa Bavicha Taifa, Patrick Ole Sosopi, alisema idadi hiyo ni baada ya kuanza uchukuaji na urejeshaji fomu ambao utafika ukingoni majira ya saa 10 jioni Novemba 30, mwaka huu.

Alisema vijana wengi wamejitokeza kutokana na hamasa kubwa iliyofanyika ya kuwapa nafasi vijana kujiamini na kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

"Tuna expect (tunatarajia) vijana zaidi ya 100 kujitokeza kuchukua fomu ila kwa sasa bado zoezi linaendelea na watu wanachukua fomu maeneo mbalimbali wengine mtandaoni ,wengine kwenye ofisi zetu za kanda nakadhalika," alisema Sosopi.

Mkurugenzi wa Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje, John Mrema, alisema kwa sasa wananchi wanachukua fomu kwenye tovuti ya chama na ofisi za chama.

"Kwa sasa ni vigumu kujua idadi ya waliojitokeza kuwania nafasi mbalimbali, wanachukua fomu mtandaoni na ofisi, wanazilipia na kurudisha, wakianza kurudisha tutakuwa kwenye nafasi nzuri ya kueleza," alisema.

Kwa mujibu wa Mrema, kuanzia leo uchaguzi kwenye kanda mbalimbali utaanza kufanyika kwa kadri ya walivyojipanga na hadi mwisho wa wiki hii utakuwa umekamilika.

Alisema mwisho wa kurejesha fomu ni saa 10 jioni Novemba 30, mwaka huu.

Hivi karibuni, Katibu Mkuu wa chama hicho Taifa, Dk. Vincent Mashinji, alitangaza kuanza kwa mchakato wa uchaguzi ndani ya chama hicho ulioanza Novemba 18, mwaka huu na unaotarajiwa kukamilika Desemba 18, mwaka huu.

Nafasi zinazowaniwa ni Mwenyekiti wa baraza hilo Taifa, Makamu mwenyekiti nafasi mbili ikiwamo nafasi moja kutoka Zanzibar na nyingine kutoka Tanzania bara, Katibu Mkuu, Naibu Katibu

Mkuu ,Mratibu wa uhamasishaji, mweka hazina ,wajumbe watano wawakilishi wa mkutano mkuu pamoja na wajumbe 20 wawakilishi wa baraza kuu la chama hicho.


中国水电
SINOHYDRO

**JOB ANNOUNCEMENTS**

We are **SINOHYDRO CORPORATION LIMITED,** currently implementing the Zanzibar Irrigation Infrastructure Construction Project both at Unguja and Pemba.

We are recruiting heavy equipment **operators, truck drivers, electricians, fitters, concrete workers, steel bar workers, and experienced worker of** all related disciplines.

We are sourcing **fuels, steel bars, cement, aggregates, rip rap stones, geotextiles, PE/PVC pipes, steel pipes, scaffoldings, and various other materials.**

We are also in need of small machines, tools, and equipment.

115529602

Kindly send your application/quotation to Mr. Yan at yyg608@163.com or call 0778 460047.


# Aliyekuwa mgombea S/mitaa adaiwa kuchinjwa

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

ALIYEKUWA mgombea wa ujumbe wa serikali ya mtaa wa Mnara wa Voda Esso, Kata ya Ungalimited jijini hapa, Sirili Homary, amekutwa amekufa kwa madai ya kuchinjwa nyumbani kwake.

Tukio hilo linadaiwa kutokea eneo la Mnara wa Voda siku tatu zilizopita.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi Mkoani Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Jonathan Shana, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuwa kimetokea siku tatu zilizopita.

Alisema Homary alikutwa nyumbani kwake katika eneo la Mnara wa Voda, huku funguo ikiwa ndani akiwa amefariki dunia.

"Bado tunachunguza na tutatoa taarifa, maana mtu amekutwa ndani na funguo ikiwa ndani inawezekana pia amejidhuru mwenyewe kutokana na labda msongo wa mawazo," alisema Kamanda Shana.

Vile vile, alisema kuna baadhi ya wanasiasa wanaoleta uchochezi kuhusu kifo hicho na kuahidi wakiendelea atawachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

"Naomba watupe muda vyombo rasmi vya uchunguzi vifanye kazi yake, jambo kama hilo lina taratibu linapotokea tunachunguza kwa kuhusisha vyombo vinavyoaminiwa na wananchi na tutatoa taarifa kupitia vyombo vya babari," alisema Shana.

Naye Mbunge wa Arusha, Godbless Lema, akihojiwa na Nipashe alisema jambo hilo ni la kikatili na la kuhuzunisha na kwamba amezungumza na Kamanda wa Polisi ambaye amemwambia watu kadhaa wanashikiliwa kuhojiwa kutokana na mauaji hayo.

Alisema Chadema mkoani hapo kimeunda kamati maalum kufuatilia mauaji hayo kutokana na kifo hicho kuwa na utata na kwamba Homary alikuwa kada maarufu na mwaminifu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

"Sio kawaida kwa polisi kukaa kimya hapa kuna utata, RPC alipaswa aite kikao na wanahabari na waulize majibu na ajibu sasa ukimya huu unatushangaza maana jamii itapata picha gani?" Alihoji Lema.

Alisema wanaodai amejichinja haiingii akilini kutokana na ugumu wake kwa mtu timamu kuchukua uamuzi huo kwa kuwa hata mkanda wa suruali ungetosha kufanya hivyo.

"Katika binadamu 100,000 ni mmoja tu ambaye anaweza kukatisha maisha yake kwa kujichinja ni jambo ambalo si rahisi kulitekeleza maana linahitaji uwendawazimu na sio kwa mtu mwenye akili za kawaida," alisema Lema.

Alisema polisi asije kutoa majibu rahisi kuhusu mauaji hayo, itoe majibu ambayo jamii itaridhika na kutotafsiri vingine ili kuleta picha nzuri kwa nchi.

Alitoa mfano wa mume anapofumaniwa na mke haitasaidia kupunguza uzito wa fumanizi kwa kile kitakachoelezwa kuwa alikuwa anatumia kinga.

Hata hivyo Lema alisema, hawezi kuhusisha tukio hilo na siasa kwa kuwa marehemu pamoja na baadhi vyama vya upinzani wailishajitoa katika kinyan'ganyiro cha uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mwili wa marehemu Homary unatarajiwa kuagwa leo saa 10 nyumbani kwake na baadaye kutasafirishwa kwa ajili ya mazishi yatakayofanyia Katesh, wilayani Hanang.


**SHUKRANI**



*Marehemu Cornel Lundu Apson*
*1944 - 2019*

Familia ya Marehemu **Cornel Lundu Apson** wa Mbezi Beach Dar es salaam, wanapenda kutoa shukrani za dhati kwa ndugu, jamaa na marafiki wote walioshiriki nasi katika mazishi ya mpendwa wetu Mzee Cornel Lundu Apson aliyefariki tarehe **7.10.2019** na kuzikwa tarehe **12.10.2019** katika makaburi ya shambani kwake Shiwanda Vwawa Mbozi. ***Familia inakukaribisha kwenye misa ya shukrani Jumapili tarehe 1.12.2019 saa 4 asubuhi katika kanisa Katoliki Parokia ya Vwawa Mbozi.*** Baada ya misa tutashirikiana chakula cha mchana nyumbani kwa marehemu, Shiwanda Vwawa Mbozi.

**Pia tunapenda kuwashukuru kwa dhati**
**Hospitali ya Hindu mandal, Hospitali ya Emilio Mzena, Jakaya Kikwete Cardiac Institute, Wilgers Hospital South Africa, Ubalozi wa Tanzania South Africa, Ofisi ya Rais na Idara ya usalama wa Taifa.**
**Shukrani za kipekee ziende kwa**
**Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**Dkt. John Pombe Magufuli.**

**2 Timotheo 4:7 "NIMEVIPIGA VITA VILIVYO VIZURI, MWENDO NIMEUMALIZA, IMANI NIMEILINDA"**

# Ongezeko la watu linavyoiweka sekta uhifadhi, utalii njia panda

## ■Mamia ya vijiji yahalalishwa hifadhini
## ■Makazi yawekwa shoroba kongwe
## ■Mkapa atoa angalizo tuendako



**Na Sanula Athanas**

SAFARI ya nchi kuelekea uchumi wa kati imeiva. Hilo halina mjadala. Mada kuu katika safari hiyo ni ujenzi wa uchumi wa viwanda ambao kimsingi utendaji wake, unagusa moja kwa moja kufufuka au kusimama sawia kwa sekta nyingi za kitaifa.

Juni 1999, Tanzania ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo pamoja na mambo mengine, inalenga kupunguza nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya wawe katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Lakini, katika upande wa pili wa shilingi, haina maana safari hiyo iliyobakisha miaka sita, ni ya lami tambarare -- kuna mashimo na matuta.

Hadi sasa, kuna baadhi ya sekta ambazo zina hisa katika ukuaji wa uchumi wa nchi, zinaguswa kwa namna hasi na safari hiyo kiujumla. Kwa vipi?

Miongoni mwa sekta zinazoguswa kwa namna hasi, utalii na uhifadhi haikosekani. Tayari kuna vilio kutoka maeneo tofauti ya kitaifa kuhusu baadhi ya watu kuvamia na kubadili matumizi ya maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za uhifadhi na utalii.

Hiyo inajumuisha ujenzi wa makazi ya kudumu na uingiliaji wa maeneo ya mtawanyiko na mapito ya wanyamapori (shoroba), ambayo yana sheria na kanuni zinazoongoza matumizi yake.

Kinachoelezwa kitaalamu ni kwamba, picha kuu inayotawala mageuzi hayo ni kasi ya ongezeko la watu nchini inayotajwa kutishia uhai wa sekta hiyo na nyinginezo.

Kuna hatua kadhaa zimechukuliwa na serikali kuhusiana na mustakabali wa ustawi wa uhifadhi na utalii na kasi ya ongezeko la watu katika maeneo yanayogusa sekta hiyo muhimu.

Itakumbukwa hatua mojawapo ni ya Septemba 23, mwaka huu, serikali ilipotangaza kufuta mapori tengefu 12 yenye ukubwa wa ekari 707,659.94 na kuagiza yagawiwe kwa wananchi kwa ajili ya makazi na shughuli za kilimo na ufugaji.

Ni uamuzi uliotangazwa baada ya kikao cha Baraza la Mawaziri jijini Dar es Salaam, kupokea taarifa ya kamati iliyoundwa na Rais John Magufuli, kufuatilia migogoro ya ardhi iliyomea nchini.

Taarifa iliyotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, baada ya kumalizika kwa kikao hicho, ilieleza kuwa serikali imeamua kuhalalisha vijiji 920 kati ya 975 vilivyotajwa kuwapo ndani ya hifadhi.

Pia, uamuzi huo ukaelekeza mipaka ya vijiji hivyo irejewe, vipatiwe vyeti vipya vya milki ya ardhi na kupangiwa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

"Orodha ya vijiji hivyo itatangazwa baadaye. Vijiji 55 vilivyobaki vinaendelea kufanyiwa tathmini ya kina kwa maeneo yaliyobaki ndani ya hifadhi," alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali pia imeridhia misitu ya hifadhi saba yenye ukubwa wa ekari 46,715, itolewe kwa wananchi kwa ajili ya makazi na shughuli za kilimo na ufugaji ili kuwaondolea kero za uhaba wa ardhi.

Majaliwa aliongeza kuwa serikali pia imeridhia kumega hifadhi za misitu 14 ili wananchi wapate maeneo kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

**ONGEZEKO LA WATU**

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Tanzania mwaka huu inakadiriwa kuwa na watu 55,890,747 (milioni 55.89). Kati yao, wanaume ni 27,356,189 na wanawake 28,534,558.

Kwa makadirio hayo, idadi imeongezeka kwa watu milioni 43.59 katika kipindi cha miaka 42 kwa kuwa takwimu za NBS zinaonesha mwaka 1967, Tanzania ilikuwa na watu milioni 12.3, Tanzania Bara ikiwa na watu milioni 11.9 na Zanzibar watu 354,815.

Hoja ya kasi ya ongezeko la watu nchini pia imegusiwa na Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, kupitia kitabu chake cha 'My Life, My Purpose' (Maisha Yangu, Kusudio Langu) alichokizindua Novemba 12, mwaka huu.

Katika kitabu hicho, Mkapa anaeleza shaka yake kuhusiana na kasi hiyo anayoona inakosa sera na mwongozo sahihi wa kuikabili ishara hiyo mbaya kwa maendeleo ya umma.

"Ongezeko la watu katika nchi siyo kipimo cha maendeleo bali ni kikwazo kwa maendeleo. Shida kubwa ya nchi nyingi za kiafrika, hatuna mjadala madhubuti kuhusu sera ya idadi ya watu katika nchi zetu," Mkapa analalamika.

Kiongozi huyo mstaafu anaeleza ubashiri wa kisayansi wa mwelekeo wa sensa zijazo, kwamba ifikapo mwaka 2025, ambao ndiyo ukomo wa Dira ya Maendeleo ya Taifa, nchi inatarajiwa kuwa na wakazi milioni 67. Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 947,300.

Mkapa anasema wakati wa uhuru mwaka 1961, kulikadiriwa kuwapo Watanganyika milioni 10.4 na idadi iliongezeka hadi Watanzania milioni 27.4 alipoanza kukalia kiti cha urais mwaka 1995 na iliongezeka hadi milioni 36.1 alipoondoka madarakani mwaka 2005.

Vilevile, Ripoti ya Juni 21, 2017 ya Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA), ilibainisha kuwa Tanzania imo katika nchi tisa zinazochangia kasi ya ongezeko la watu duniani. Tanzania ilitangazwa kuwa ni ya nne barani Afrika.

Ripoti hiyo inaitaja India, taifa linalokadiriwa kuwa na watu bilioni 1.3, ndiyo ya kwanza kwa kasi kubwa ya ongezeko la watu na katika mataifa nane yanayofuata, matano ni ya barani Afrika. Kati yake, matatu ni ya kusini mwa Jangwa la Sahara na mawili ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Orodha ya mataifa hayo kwa nafasi zake nyuma ya India ni: Nigeria; Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC); Pakistan; Ethiopia; Tanzania; Marekani; Uganda na Indonesia.

Vilevile, ripoti inasema wakazi wa dunia wataongezeka kutoka bilioni 7.6 wa mwaka 2016 hadi bilioni 8.6 ifikapo mwaka 2030, ambao ni ukomo wa kipindi cha Malengo ya Maendeleo Endelevu.

**ITAENDELEA KESHO**

### JEDWALI LA SENSA TANZANIA

| Mwaka | Idadi ya watu | Tanzania Bara | Zanzibar |
|---|---|---|---|
| 1967 | 12,313,469 | 11,958,654 | 354,815 |
| 1978 | 17,512,610 | 17,512,610 | 476,111 |
| 1988 | 23,095,878 | 22,455,193 | 640,685 |
| 2002 | 34,569,232 | 33,584,607 | 984,625 |
| 2012 | 44,928,923 | 43,625,354 | 1,303,569 |

**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)**

Jedwali Inaoonesha ongezeko la watu nchini. Chanzo: Takwimu za NBS

HABARI KITAIFA



Rais Dkt. John Magufuli akipokea hundi ya gawio kwa Serikali kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB Ally Laay na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Abdulmajid Nsekela wakati wa hafla ya upokeaji gawio na michango kwa serikali iliyofanyika Ikulu Chamwino, Dodoma. Wengine pichani ni Waziri wa fedha Dkt. Philip Mpango na Spika wa Bunge Job Ndugai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yajivunia kupungua mauaji ya wenye ualbino

**Na Rose Jacob,** MWANZA

SERIKALI imesema imepata mafanikio makubwa kuhusu mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili kwa watu wenye ualbino ambao awali walikuwa wakikatwa viungo na kuuawa kipindi cha uchanguzi wa siasa.

Kauli hiyo ilitolewa na Ofisa Ustawi wa Jamii Jiji la Mwanza, Devis Justine, wakati wa uzinduzi wa mradi wa miezi minne wa kuwawezesha wanawake 30 walio na ualbino na wasio na ualbino, lakini wamejifungua watoto wa wenye ulbino huo ili kuwa mabalozi katika familia na jamii katika wilaya zote za Mkoa wa Mwanza.

Mradi huo ambao umefadhiliwa na Shirika la Under The Same Sun linalojihusisha na utetezi na haki za watu wenye ualbino kwa kushirikiana na wahisani kutoka Canada, umelenga kuwawezesha wanawake hao kutambua hali zao, namna ualbino unavyotokea, kupambana na changamoto zinazojitokeza na kutoa taarifa pale wanapobaini kuna viashiria vya vitendo vya ukatili.

Justine alisema Serikali ilitumia nguvu kubwa kukokomeza vitendo vya kinyama na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino ambavyo vilikuwa vikitokea hasa nyakati za uchaguzi wa viongozi wa siasa.

Alisema mafanikio hayo yametokana na Serikali kushirikiana na wananchi pamoja na wadau wengine kuwafichua waliokuwa wanasababisha hali hiyo, hali ambayo inaichafua taifa, na kueleza kuwa hivi sasa watu wenye ualbino wanaishi kwa uhuru na

**INAENDELEA UK. 8**

# NSSF yawanoa wafanyakazi kaskazini

**Na Mwandishi wetu**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limetoa mafunzo ya mabadiliko ya utendaji kazi kwa wafanyakazi wake, kwa lengo la kuhakikisha wanawahudumia kwa ustadi mkubwa wanachama wake.

Mafunzo hayo yametolewa kwa wafanyakazi wa mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha, na kufunguliwa na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa NSSF, Julius Mganga, ambaye alisema mipango iliyopo ni kuhakikisha kuwa kunakuwa na mabadiliko makubwa ya utendajikazi.

"NSSF imedhamiria kuboresha utoaji wa huduma kwa wanachama wake ili kuendana na matarajio ya wanachama na matakwa ya shirika, tunataka kutoa huduma kwa wanachama wetu katika ubora unaotakiwa, wafanyakazi wanatakiwa kutoa huduma kwa kufuata sheria na matakwa ya wanachama," alisema.

Alisema wanataka kuona kuwa huduma zote kwa kipindi wanapokuwa na mwanachama taarifa zake zinaakisi kilichokusudiwa kuhakikisha anahudumiwa kwa mujibu wa sheria, jambo ambalo litakuwa faraja kwa wanachama.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Imamu Mkuu wa Msikiti wa Maamur, Sheikh Issa Othuman Issa, alisema kwenye dini kazi ni ibada kama zilivyo ibada nyingine na kwamba wafanyakazi wanatakiwa kuzingatia maadili ya kazi kwa kutoa huduma sahihi. "Tumezungumza na wafanyakazi wa NSSF wa Tanga, Kilimanjaro na Arusha na tumewaeleza kuwa kazi ni ibada na umuhimu wa kushikamana na maadili katika utendaji kazi wao. Hivyo wanatakiwa wawe na misimamo ya kuwa na haki kwa kuzingatia kuwa wakifanya hivyo watakuwa wanamfurahisha mwenyezi Mungu na binadamu wanaowahudumia" alisema Sheikh Issa.

Kwa upande wake, Mchungaji Mwaipopo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Azania Front, aliwataka wafanyakazi wa NSSF kuhakikisha hawajipangi kwa mabadiliko bali wanajifunza kubadilika, kwani mabadiliko hayaepukiki bali ni utayari wao kuyapokea na kubadilika kuwa chanya yaani kuwa watumishi bora.

# Tanzania yakubali mkutano tabianchi

**Na Mwandishi Maalum**

TANZANIA imekubali kuhudhuria mkutano wa tabianchi wa siku 12 utakaofanyika Mjini Madrid, Hispaniola chini ya Umoja wa Mataifa kuanzia Desemba 2, mwaka huu.

Mkutano huo unaandaliwa na taasisi ijulikanayo kama 'United Nations Framework Convention on Climate Change' (UNFCCC) ambayo Tanzania ni mwanachama.

Akitangaza kukubali kwa Tanzania mwaliko uliwasilishwa na Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini, Manfredo Fanti alipokutana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais

(Muungano na Mazingira), George Simbachawene, alisema Tanzania inaupa uzito mkutano ujao wa Madrid na inazipa uzito mkubwa sana juhudi za pamoja za kupambana na athari za tabia duniani kote.

Alisema athari za na mabalaa yatokanayo na janga la tabianchi havitabiliki, vinaongezeka na vinadhihirika nchini.

Viongozi hao walikutana jijini Dar es Salaam katika mwendelezo wa mashauriano juu ya ushirikiano kati ya pande hizo mbili. Waziri Simbachawene alisema mazungumzo juu ya ushirikiano huo, ambao safari hii utakuwa wa kipindi cha miaka saba (2021-2027), yamo katika hatua ya mwisho.

Alisema EU ni mdau muhimu wa maendeleo wa Tanzania, huku ikiushukuru umoja huo kwa kuisaidia Tanzania kutunza mazingira.

"Tunakushukuru hasa kwa msaada umbao tumepokea kupitia Global Climate Change Alliance Programme (GCCA) na ambao kwetu umepitia wizara ya fedha."

Waziri Simbachawene alisema katika ushirikiano wa miaka saba ijayo, Tanzania ingependa ushirikiano ulenge hasa kwenye maeneo ya athari za tabianchi, uthibiti wa taka, utuzaji wa ardhi (kwa kupanda miti), uchumi wa bahari na maziwa na utunzaji wa viumbe, hasa kwa kujitikita kwenye viumbe vigeni. Balozi Fanti aliipongeza Tanzania kwa hatua mbali mbali inazozichukua katika kupambana na kupunguza athari za tabianchi.


CSDR Settlement & Custody

TANGAZO

WITO KWA WANAHISA KUFUATILIA MALIPO YA GAWIO

CSD & Registry Company Limited (CSDR) kampuni tanzu ya Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) inahusika na ulipaji wa gawio kwa wanahisa wa makampuni yafuatayo ambayo yalitangaza kulipa gawio kwa wanahisa wake:

1. Vodacom (T) PLC
2. TOL Gases Limited (TOL)
3. TCCIA Investment PLC (TICL)
4. Tanga Cement PLC (TCPLC)
5. National Investments PLC (NICOL)
6. Mkombozi Commercial Bank PLC (MKCB)
7. Dar es Salaam Stock Exchange PLC (DSE)

Tunapenda kuwataarifu wanahisa wote wa makampuni tajwa hapo juu kuwa, mpaka kufikia tarehe ya tangazo hili kuna idadi kubwa ya wanahisa ambao hawajachukua pesa zao za gawio. Hii inatokana na CSDR kutokuwa na taarifa zao za kibenki au namba za simu ambazo zitawezesha kulipa gawio.

Ili kuweza kulipwa gawio, mwanahisa anapaswa kututumia Taarifa za Kibenki (Namba ya Akaunti na Jina la Benki), Namba ya Simu ya Mkononi pamoja na nakala ya nyaraka zifuatazo:

- Stakabadhi ya Umiliki wa Hisa (CDS Receipt)
- Kitambulisho (kati ya kitambulisho cha taifa, pasi ya kusafiria, leseni ya udereva au kadi mpya ya mpiga kura)

Mwanahisa anaweza kutuma taarifa zake kwa barua au kwa kujaza fomu ya kuboresha kumbukumbu za mwanahisa inayopatikana kwenye tovuti yetu **www.csdr.co.tz** na kutuma kwa Sanduku la Posta, barua pepe au WhatsApp kupitia anuani ifuatayo:

Msajili wa Hisa
CSD & Registry Company Limited
Kambarage House, Gorofa ya 2, Mtaa wa Ufukoni
S.L.P 70081
Dar es Salaam
Simu: 0746 160516 / 0677 070414
Barua Pepe: registrar@csdr.co.tz

Ofisi zipo wazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 2 asubuhi mpaka saa 11 Jioni kwa siku za kazi tu.

MKURUGENZI MKUU
CSD & REGISTRY COMPANY LIMITED (CSDR)

215530401

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuungane kuishangilia Kili Queens itupe ubingwa leo

**LEO** michuano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge Cup) kwa Wanawake inafikia ukingoni kwa kupigwa mechi ya fainali itakayozikutanisha timu ya Taifa ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Queens na majirani zao, Kenya.

Katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam majira saa 10 jioni, itatanguliwa na ya kutafuta mshindi wa tatu kati ya Burundi na Uganda saa saba na nusu mchana.

Kilimanjaro Queens imetinga hatua hiyo baada ya kuongoza Kundi A, ambapo ilianza kwa kuichapa Sudan Kusini mabao 9-0 kisha ikatoa kipigo cha 4-0 dhidi ya Burundi kabla ya kuhitimisha kwa kuwatandika ndugu zao wa Tanzania Visiwani, Zanzibar Queens kwa mabao 7-0.

Na katika hatua ya nusu fainali ikatoa kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Uganda iliyomaliza nafasi ya pili katika Kundi B lililoongozwa na Kenya ambayo ilitoa Burundi katika hatua hiyo kwa kuifunga mabao 5-0. Kwa ujumla mechi hiyo ya fainali ni ngumu hasa kutokana na ubora wa timu zote hasa ikizingatiwa Kenya nayo imefanya vizuri kuanzia hatua ya makundi ambapo katika Kundi lake la B ilitoa kichapo cha mabao 12-0 dhidi ya Djibouti, ikaichapa Ethiopia 2-0 na kisha ikaitandika Uganda 3-0.

Hivyo ni timu mbili ambazo zinakutana katika fainali zikiwa hazikupoteza mchezo hata mmoja huku pia zikiwa hazijaruhusu nyavu zao kutobolewa ambapo kwa Kilimanjaro Queens imefunga jumla ya mabao 21-0 wakati Kenya ikitingisha nyavu mara 17-0 hadi zinafika fainali.

Kimahesabu Kenya si ya kubeza hata kidogo na inaonekana kuimarika na kuwa bora hasa ukizingatia, mpinzani wa Kilimanjaro Queens katika hatua ya makundi, Burundi na yule wa hatua ya nusu fainali, Uganda, Kenya iliwafunga kwa idadi kubwa zaidi ya mabao ukilinganisha na waliyofungwa na timu hiyo ya Tanzania Bara. Wakati hatua ya makundi Kilimanjaro Queens ikiifunga Burundi 4-0 na kisha nusu fainali ikaifunga Uganda bao 1-0, Kenya yenyewe katika hatua ya makundi iliwachapa Waganda hao mabao 3-0 kisha nusu fainali ikawafumua Warundi hao 5-0, hivyo inaonyesha ni kwa namna gani Wakenya walivyo bora.

Hata hivyo, Nipashe hatuna wasiwasi kabisa kuhusu ubora wa Kilimanjaro Queens chini ya kocha mtaalam Bakari Shime, kuelekea mchezo huo wa leo ambao kama ikishinda itatwaa taji hilo kwa mara ya tatu mfululizo, wakati Kenya hii itakuwa mara yao ya kwanza kulibeba endapo itaibuka na ushindi.

Tunaamini Shime atakuwa ameielekeza vema safu yake ya ulinzi namna ya kuwa makini katika kumkaba mshambuliaji Jentrix Shikangwa ambaye anaongoza katika orodha ya wafungaji akiwa na mabao tisa hadi sasa kwenye michuano hiyo.

Na si mshambuliaji huyo pekee, bali winga Mwanalima Jereko anapaswa kutazamwa vema na mabeki wa Kilimanjaro Queens kwani amekuwa bora zaidi katika ufungaji pamoja na kumtengenezea mabao Shikangwa.

Kinachotakiwa zaidi kwa Kilimanjaro Queens, mbali ya ilivyofanya kwenye mechi zilizopita, inatakiwa kuongeza umakini zaidi lakini pia ikicheza kitimu mwanzo mwisho ili kuweza kuibuka na ushindi.

Tunachotamani kukiona kikitokea ni kama ilivyo matamanio ya Watanzania wote kwa ujumla, ni Kilimanjaro Queens kutwaa ubingwa huo kwa mara ya tatu mfululizo na kutokubali katu kupoteza ikiwa katika ardhi yake ya nyumbani.

Tunatambua ili hilo liwezekane, mchezaji wa 12 uwanjani [mashabiki] wa kuwapa wachezaji hamasa ili kuweza kuongeza morali ya ushindi, ni muhimu kuwapo uwanjani, kwa kulitambua hilo hatuna budi kuwahimiza Watanzania kujitokeza katika Chamazi leo ili kuishangilia Kilimanjaro Queens mwanzo mwisho. Nipashe tunaitakia kila la kheri Kilimanjaro Queens kushinda leo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Samatta kuwamo tu Stars ni ushindi tosha

Na Adam Fungamwango

**MBWANA** Samatta kama angekuwa ni Mganda, Mkenya, Mzambia au hata raia ya Madagascar tu, basi angepewa heshima kubwa tofauti na baadhi ya mashabiki wa soka la Tanzania wanavyomchukulia.

Baadhi ya mashabiki wa soka nchini wamekuwa wakitokwa na povu, wakimshutumu straika huyo kuwa anapochezea timu yake ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, hajitumi tofauti na anavyocheza kwenye klabu yake ya KRC Genk ya Ubelgiji.

Baada ya mechi ya kutafuta tiketi ya kufuzu AFCON 2021 nchini Cameroon dhidi ya Equtorial Guinea, Taifa Stars ikashinda mabao 2-1, ilianza minong'ono na kipigo cha mabao 2-1 ugenini dhidi ya Libya kilisababisha mashabiki hao kupaza sauti zao kwenye mitandao ya kijamii na baadhi ya vyombo vya habari kuwa Samatta ndiye anayeangusha Stars kwa sababu anakosa sana mabao.

Hali ikawa mbaya kwenye mitandao ya kijamii ya kumfanya Samatta mwenyewe kujibu meseji ya baadhi ya mashabiki wa soka wanaomshutumu.

Alijibu kiukomavu wa hali juu. Akiwaambia amesikia na atajirekebisha. Kwangu mimi nadhani wanaomshutumu Samatta wanauangalia mpira kijuujuu au kishabiki zaidi.

Wanachoangalia pale kutaka Stars ishinde, tena bao lenyewe afunge Samatta. Hawauangalii mpira kiufundi na umuhimu wake uwanjani.

Kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Ubelgiji tangu atoke kucheza mechi za kufuzu AFCON, Samatta hajafunga bao, timu yake ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Royal Excel Mouscron.

Ina maana walifunga wachezaji wengine. Hili ndilo soka. Asipofunga yeye mwingine afunge. Asipofunga David Molinga, Juma Balinya afunge kwa Yanga na kwa Simba asipofunga Meddie Kagere, Miraji Athumani na afunge.

Haiwezekani Simba ikikosa ushindi alaumiwe Kagere kwa nini hafungi, au Yanga isiposhinda basi lawama zote kwa Molinga, hii si sawa kwa sababu soka ni mchezo wa ushirikiano zaidi na si kama ngumi ambapo anakuwa mtu mmoja tu ulingoni akipigana na mwenzake.

Samatta anapokuwa uwanjani hasa kwenye timu ya taifa, anakuwa anachungwa zaidi na mabeki zaidi ya mmoja au wawili.

Makocha wa timu pinzani ni rahisi zaidi kumuwekea mikakati ya kumlinda Samatta kuliko Ditram Nchimbi au Simon Msuva kwa sababu anacheza ligi Ulaya ambayo ni rahisi zaidi kuiona.

Nchimbi na wenzake ndiyo wanakuwa kwenye wakati mzuri zaidi wa kusumbua na kufunga kuliko Samatta mwenyewe ambaye anamulikwa na 'kijiji' uwanjani.

Wakati Samatta anatembea na mabeki wawili au watatu uwanjani, ina maana kuna wenzake anaocheza nao Stars hawana watu wa kuwakaba wanabaki huru.

Hawa wanafanyaje kuisaidia timu wakati wakiwa huru tofauti na mwenzao ambaye mgongoni kuna watu wanaomlinda?

Hata ukitazama akiwa anacheza Genk, Samatta huwa haangahiki sana, badala yake analishwa kwa pasi murua za mpenyezo na krosi au kona zenye macho na yeye kazi yake ni kufunga tu.

Je, Stars tumeziona pasi, krosi au kona za aina hiyo? Haiwezekani kwa sababu Samatta ni staa, basi awe anahangaika uwanjani kwa kila kitu, achukue mpira yeye apige chenga yeye na kufunga.

Straika huyo naona anatatizwa zaidi na kutokuwapo kwa wachezaji wengi wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi tena lile la ushindani.

Ndiyo maana nikasema kama ingekuwa kwenye mataifa ambayo yenye wachezaji wengi wanacheza soka nje tena kwenye ligi za ushindani, au kuwa na wachezaji ambao wenye viwango vya juu na kujua jinsi ya kuchezesha, basi angekuwa anafanya vitu vikubwa zaidi ya hivi. Baadhi ya Wabongo wasijidanganye kutaka eti asipangwe kwenye mechi zinazofuata.

Kuwapo kwake uwanjani tu kunasababisha hata wapinzani wacheze kwa woga na wasipande wote na kuwa salama kwa Stars.

Na itakuwa ni vichekesho kwa mataifa mengine duniani kwa timu kama ya Tanzania ambayo haina wachezaji wa viwango vya juu kama yeye, kumuweka nje au kumuacha na kuchezesha wachezaji wengine.

Waswahili wana msemo 'kondoo hajui thamani ya mkia wake hadi ukatwe'. Chondechonde, tusiombee hali hiyo isije ikajitokeza Stars.

## MJADALA

# Soka la wanawake lina mvuto, lisitelekezwe

Na Adam Fungamwango

ILIKUWA ni raha kuwaona akinadada, akinamama na watoto wao bila kujali jua wala mvua wakimiminika kwa wingi kuujaza Uwanja wa Azam Complex kwenye michuano ya Kombe la Challenge kwa Wanawake kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Kina kaka na kina baba nao pia walikuwa si tu wakiujaza uwanja, lakini pia walionekana kufurahia, kucheza, kuimba na kushangilia kile kilichokuwa kikifanywa na akinadada kutoka nchi mbalimbali za ukanda huu.

Kwa muda mrefu michuano kama hii ilikuwa inafanyika nje ya nchi na hata timu ya Tanzania, Twiga Stars au Tanzania Bara (Kilimanjaro Queens) ilipokuwa ikirejea na kombe, Watanzania walikuwa wakishangilia kwa uzalendo tu, lakini wengi walikuwa hawajapata kuona kile ambacho wachezaji hao wakikifanya uwanjani.

Mwaka huu, Challenge imefanyika nchini, mashabiki wa soka nchini wameshuhudia burudani ya aina yake, ufundi wa hali ya juu ukifanywa na kinadada, wakati mwingine ni zaidi ya kile kinachofanywa kwenye soka la wanaume.

Mashabiki wameshuhudia baadhi ya akinadada si wa Tanzania Bara tu, hata Ehiopia, Uganda, Kenya na Burundi wakifanya vitu vyao, wakiwa na vipaji vya hali ya juu vilivyowashangaza wengi.

Kuonyeshwa laivu kwa michuano hiyo nayo pia imekuwa chachu kubwa ya kuhamasisha mashabiki kwa wingi kutazama soka la wanawake ambalo limewavutia wengi.

Watanzania wengi wameonekana kuvutiwa mno na michuano hiyo na nadhani wanaombea hata mwakani ifanyike tena nchini, kutokana na burudani kubwa iliyokuwa ikionyeshwa uwanjani na kinadada hao.

Nadhani mashabiki wengi wa Kibongo hawakudhani kama kuna akinadada wenye uwezo kama ule ulioonekana wakati huu leo ikipigwa mechi ya kutafuta mshindi wa tatu na ile ya fainali.




Kifupi tu ni kwamba michuano ya Challenge kwa wanawake msimu huu, imefana zaidi kuliko ilivyotarajiwa.

Nadhani hapa kuna kitu cha kujifunza kwa Watanzania wote, hasa kwa serikali, Shirikisho la Soka nchini (TFF) ambalo nadhani liliamua kuipeleka michuano hiyo Uwanja wa Chamazi, Mbagala likidhani ni soka ambalo halina mashabiki wengi, jambo ambalo nilitarajia baada ya kuona muitiko mkubwa basi mechi za kutafuta mshindi wa tatu na ile ya fainali, ingehamishiwa Uwanja wa Uhuru ama Taifa lakini hilo halikutokea.

Ni kwamba kama watu wakiwekeza kwenye soka la wanawake litalipa. Imeonekana kuwa Watanzania wanapenda soka, liwe la wanaume au wanawake, ili mradi tu kuwe na mikakati ya kuyatangaza na kuyawekea mazingira mazuri ya watu kwenda uwanjani.

Ilionekana kana kwamba soka la wanawake halipendwi kwa sababu mashabiki hawajishughulishi kwenye kuangalia Ligi Kuu ya Wanawake nchini.

Kwa nini kwenye michuano hii watu wamehamasika sana? Ni kwa sababu Cecafa na TFF waliamua kuhamasisha mashabiki na kuweka mazingira mazuri ya watu kwenda uwanjani, pamoja na kuyatangaza.

Hili pekee ndilo lililoonekana kukosekana kwenye soka la wanawake. Kwa maana hiyo, kabla watu hawajapoa na kusahau, TFF iendelee pale ilipoachia kuwahamasisha mashabiki kujitokeza kwa wingi kwenye mechi za Ligi Kuu ya Wanawake.

Staili ile ile iliyotumika kwenye Challenge ndiyo hiyo iendelee, na hata uwanja uwe ni ule ule wa Azam Complex ili kutowachanganya mashabiki.

Kama upande mmoja watu waliingia bure na upande wa jukwaa Kuu kwa kiingilio, basi iwe hata kwenye ligi ili kuendelea kuvuta watu na kuupenda mchezo huo kwa akinamama.

Lakini pia baadhi ya mechi zingekuwa zinaonyeshwa ili kuifanya ligi hiyo kukubalika na kuwa machoni na midomoni mwa mashabiki nchini.

Mbinu hii ilitumika wakati wa baadhi ya Ligi Kuu pendwa za Ulaya ambazo miaka kadhaa iliyopita ilikuwa ikionyeshwa bure kwenye luninga, lakini nia ilikuwa ni kuwafanya Wabongo wapende na kufuatilia ligi hizo na baada ya kujiridhisha kuwa tayari mchezo huo umeshawaingia watu damuni, ndiyo mambo ya kulipia ving'amuzi yakaanza hadi leo hii.

Ni wakati sasa wa kampuni mbalimbali hasa ya bidhaa za akinamama na akinadada kujitokeza kudhamini Ligi Kuu ya Wanawake, kwa sababu imeshaonekana kuwa ni kivutio.

TFF sasa inapaswa kuandaa mazingira bora ya kampuni kuingia kwenye soka la wanawake na sidhani kwa muitikio kama ule wa michuano ya Challenge kuna makampuni yatakataa kudhamini.

Hii itafanya klabu na hata wachezaji kuwa na hali bora, kwani mara kwa mara tunasikia malalamiko ya ukata kwenye soka la akinamama, wakiishi kwa matatizo makubwa kambini hata kusafiri kwa shida, bado sijasema posho na mishahara.

Kwa hapa ilipofikia, itakuwa ni uzembe mkubwa kwa TFF kama tutaona soka la wanawake likianza kudorora kwani tayari imeshaonyeshwa njia kuwa mashabiki wa soka la akinamama wapo, cha kufanya ni mikakati tu ya kuwahamasisha.

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz






# Mkanganyiko uchaguzi S/mitaa

INATOKA UK. 2

na Ndembezi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa kupiga kura, baadhi ya wananchi walisema wamejitokeza ili watumie haki yao ya kikatiba kuchagua viongozi ambao watawatumikia na kuwaletea maendeleo.

Agnes Temba, mkazi wa Manispaa hiyo, alisema ameamua kujitokeza kupiga kura ili achague kiongozi makini na muadilifu, ambaye atapigania maslahi ya wananchi na kuwaletea maendeleo badala ya kususia uchaguzi na kusababisha kupata kiongozi asiye na sifa.

"Nimejisikia furaha sana kupiga kura na kuchagua kiongozi ambaye namtaka ili atutumikie wananchi kutatua shida zetu pamoja na kutuletea maendeleo," alisema Temba.

Baadhi ya wasimamizi kwenye vituo vya kupigia kura akiwamo Aminael Brown, ambaye anasimamia kituo cha eneo la wazi Mama Katabi, kwenye mtaa wa Jomu, Kata ya Kambarage, alisema zoezi la upigaji kura limeendelea vizuri na wananchi wamejitokeza kupiga kura.

Alisema hakuna changamoto yoyote iliyojitokeza kwenye kituo hicho, huku hali ya usalama ikiwa imeimarishwa zaidi na kulikuwa na askari wawili wakilinda ili kusitokee tatizo la uvunjifu wa amani.

**SINGIDA**

Msimamizi wa uchaguzi wa Wilaya ya Ikungi, Haika Massawe, alisema upigaji kura kwenye vijiji na vitongoji umeenda vizuri kwa utulivu na amani.

Alisema uchaguzi umefanyika kwenye kata tano, vijiji 10 na vitongoji 50, kukiwa na wapiga kura 9,734.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, mkoani Singida, Justice Kijazi, alisema vijiji 91 na vitongoji 488, wagombea walipita bila kupingwa.

"Kura zinaendelea kupigwa kwenye vituo na watu wamejitokeza zaidi ya nusu, unaendelea kwa amani kabisa," alisema Kijazi. Alitaja wagombea wanaochuana ni kutoka vyama vya ACT- Wazalendo, Chadema, CUF na CCM, ambavyo wagombea wake waliingia kwenye kiyang'anyiro hicho.

**CHADEMA KUSHTAKI**

Chadema, kimesema yeyote atakayetumia nembo au jina la chama kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, atachukuliwa hatua kwa kushtakiwa kama taasisi au mtu binafsi.

Hatua hiyo inakuja baada ya chama hicho kutangaza kujitoa kwenye uchaguzi huo, na kupiga marufuku ya nembo au alama ya chama hicho kutumika kwenye karatasi za kupigia kura.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje, John Mrema, alisema msimamo wa chama hicho uko pale pale kutokana na kusiginwa kwa demokrasia katika mchakato wa kuchukua na kurejesha fomu.

Amesema wanachofahamu hakuna uchaguzi unaofanyika maeneo mbalimbali nchini.

"Bado haijaripotiwa popote nembo yetu kutumika kwa kuwa wanajua uchaguzi hakuna, ikitokea ikatumika tutachukua hatua za kisheria, tutawashtaki walitumia nembo kwa majina, tutazidai halmashauri fidia," alisema Mrema na kuongeza:

"Kimsingi leo (jana) hakuna uchaguzi, walipaswa kutangaza kuwa CCM imepita bila kupingwa."

Akizungumzia uchaguzi huo, alisema kinachofanyika kwa sasa nchini ni hatari kwa demokrasia kwa kuwa hata viongozi wa kitaifa wa vyama vya upinzani ambao walijiandikisha maeneo mbalimbali nchini hawakupiga kura na kuona sawa kwa hali iliyojitokeza licha ya wanaochaguliwa ni wa ngazi ya chini.

"Tunaweza kusema wananchi wamenyimwa haki, hata viongozi walioenda kujiandikisha kwenye makazi yao bado hawajaweza kupiga kura, hii ni kutokana na mchezo mchafu uliofanyika wakati wa kuandikisha, kuchukua fomu na kurejesha," alidai.

"Uchaguzi huu ni ushahidi wa kutokuwa na demokrasia, na ikiendelea hivi kutasababisha madhara kwenye mustakabali wa demokrasia nchini," alisisitiza Mrema.

**DAR WAKOSA TAARIFA**

Nipashe ilitembelea kata mbalimbali jijini Dar es Salaam ikiwamo ya Wazo na Kijitonyama na kukuta wananchi waliojitokeza

INAENDELEA UK. 26

## Serikali yajivunia kupungua mauaji ya wenye ualbino

INATOKA UK. 5

wanafanya shughuli zao nyakati zote bila kubughudhiwa.

"Kama Serikali tunasema tumepata mafanikio makubwa sana kuthibiti vitendo vya kinyama dhidi ya wenzetu wenye ualbino, tumeaunda kamati za watu wenye ualbino mitaani , lengo ni kupaza sauti," alisema na kuongeza kuwa pia Chama ca Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS), ngazi ya taifa na mkoa kinashirikiana na Serikali kuhakikisha matukio hayo yanadhibitiwa.

Naye Mratibu wa mradi huo kutoka Shirika la Under The Same Sun, Grace Wabanu, alisema wameamua kuandaa wanawake hao kuwa mabalozi kutokana na vitendo hivyo kutokea katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo akiwamo, Angelina Chuma, alipongeza shirika hilo kuwapa elimu hiyo na kuwaandaa kuwa mabalozi na wakufunzi wa vitendo dhidi ya watu wenye ualbino, huku akisisitiza kutimiza majukumu atakayopangiwa.

# JPM azipa taasisi siku 60 kuipa serikali gawio

INATOKA UK. 2

Bodi zina wenyeviti, wanalipana posho kila wanapokaa, wakurugenzi wanapanga semina, mikutano, wanasafiri, wanastarehe, wana magari na serikali imeweka pale fedha zake."

Rais Magufuli alisema yapo mashirika ambayo mishahara yake inalipwa na serikali na wengine wamepewa nyumba.

"Unaweza kujiuliza katika situation ya namna hiyo ungekuwa wewe ndo Rais ungefanyaje? Tena unaweza kukuta wengine wapo hotelini wanaangalia TV, serikali fedha za Watanzania, maskini wameweka fedha zao kama mtaji, ninyi mtakuzalishie...Mishahara wengine tutalipa, nyumba tunawapa kafanyeni biashara."

"Kila siku wanasema wanafanya biashara, lakini wakizungumza wanasema wanapata hasara, lakini magari wanayo, mikutano wanafanya, hotelini utawaona kwenye semina mbalimbali wamewaacha nyie 79 mtoe gawio,"alisema.

Rais Magufuli alisema: "Sasa Waziri (Dk.Mpango) tumebembelezana sana haiwezekani kukaa na viongozi na bodi za aina hii ambapo tunazungumza hawataki kuelewa na fedha zetu za serikali zinateketea kule never."

Alitoa siku 60 kuanzia jana wakabidhi gawio kwa Waziri wa Fedha na wasipokabidhi kwa kipindi hicho, bodi zake zijivunje zenyewe.

"Waandike barua Mwenyekiti kama ni wa kuteuliwa na mimi maana yake siku hiyo sio mwenyekiti tena, kama ameteuliwa na mwingine wajivunje wenyewe bodi isiwapo, Mkurugenzi naye ajihesabu hayupo, wapo wanaolipwa mishahara Sh. milioni 15 kwa mwezi, halafu hakuna gawio hata senti tano why?hufai kuwapo," alisema.

Alimuagiza Waziri Mpango awaandikie barua wale wote wasiokuwapo kwenye orodha ya mashirika 79 yaliyotoa gawio na orodha yao anayo.

"Sasa hawa wengine wenye viburi hivi ni nani? Katibu Mkuu na Msajili baada ya siku 60 ambaye hataleta gawio lolote ajihesabu hayupo, kila siku wewe unapata hasara, lakini za kula na kununua gari unazo si uache basi kununua gari utoe gawio,"alisisitiza.

Naye, Waziri Mpango alisema asilimia 70 ya bajeti ya serikali inategemea makusanyo ya ndani na nusu ya makusanyo yasiyo ya kodi yanatokana na gawio na michango kutoka kwa kampuni, taasisi, wakala na mashirika ya umma.

Alisema wanaendelea kufanyia kazi mashirika yanayojiendesha kwa hasara na kwamba mwaka ujao hakutakuwa na hadithi ya mashirika hayo.

Alifafanua kuwa mapato ya gawio la taasisi, mashirika na kampuni yameongezeka na kufikia Sh.Trilioni 1.05.

Awali, Msajili wa Hazina, Dk. Athuman Mbuttuka, alisema mashirika na kampuni 81 za kibiashara kati yao 40 yameshindwa kutoa gawio kutokana na kujiendesha kwa hasara.

Alisema katika kutekeleza agizo la Rais la uhakiki wa mali nchi nzima, hadi Juni 30, mwaka huu, wamepita mikoa 10 na kubaini kuwa mali za mashirika yaliyokuwa yamebinafsishwa hazipo kwenye ubinafsishaji zimeshikiliwa na watu wengine.

KDF Kilimanjaro Development Forum

P.O Box 32055,
Dar es Salaam, Tanzania
+255 658 591 182
john@stageneraltz.com
www. kilimanjarodevforum.co.tz

**MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WANACHAMA**

Wanachama wa KDF wanatangaziwa kwamba kutakuwa na mkutano mkuu wa mwaka wa wanachama wote utakaofanyika tarehe 21, Desemba, 2019 katika ukumbi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Manispaa ya Moshi.

**Agenda:**

1. Kupokea taarifa ya maendeleo ya KDF;
2. Kupokea na kupitia taarifa ya fedha ya KDF;
3. Kuchagua maafisa wa KDF na wajumbe wa bodi ya uongozi;
4. Kuteua wakaguzi na wadhamini au kuwathibitisha wanaoendelea;
5. Kupanga michango/ada za mwaka unaofuata, na
6. Kupitia na kupitisha marekebisho ya katiba.

**Uchaguzi wa viongozi katika nafasi zifuatazo;**

1. Mwenyekiti
2. Makamu Mwenyekiti
3. Katibu
4. Naibu Katibu
5. Mweka Hazina
6. Mweka Hazina Msaidizi

**Maombi ya kugombea nafasi hizi yatumwe kwa anwani zifuatazo:**

**Dr. Jonas Kipokola,**
**Katibu (KDF),**
**S.L.P 8448, Moshi au barua pepe**
**info@kilimanjarodevelopmentforum.org au piga simu 0754386003**
**Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya kugombea ni tarehe 7 Desemba, 2019.**

Mkutano Mkuu utafuatiwa na sherehe ya Kilimanjaro Day itakayofanyika siku hiyo hiyo. Umoja wetu ndiyo nguvu ya mafanikio yetu, karibuni sana

**Imetolewa na:**
**Dr. Jonas Kipokola**
**Katibu, Kilimanjaro Development Forum**

615528802

HABARI KITAIFA




Ofisa Masoko wa Zantel, Haji Said Khatibu, (kulia) akimkabidhi simu janja ya gharama nafuu aina ya Smarta, Elizabeth John, mmoja wa washindi wanne katika wiki ya pili ya Smarta, katika hafla iliyofanyika mjini Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bosi NECTA awapa somo walimu, wazazi

**Na Enock Charles**

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Dk. Charles Msonde, ametaka kuwapo ushirikiano baina ya wazazi, walimu na wanafunzi ili kuinua zaidi maendeleo ya taaluma na maadili mashuleni nchini.

Akizungumza katika mahafali ya kwanza ya Shule ya Sekondari ya Kiislam ya Ihsan iliyopo Kigamboni jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki,

Dk. Msonde alisema ushirikiano wa karibu baina ya pande zote utaongeza zaidi ufaulu mashuleni na kuinua taaluma.

"Nimezunguka katika shule nyingi, lakini sikuwahi kuona kitu kinachoitwa umoja wa wazazi, walimu na wanafunzi, nawapongeza sana Ihsan Sekondari kwa kuanzisha mfumo huu ambao utakuwa na mchango mkubwa katika kukuza elimu, maadili na uzalendo kwa taifa," alisema Dk. Msonde.

Alishauri shule zingine kuanzisha mfumo kama huo kwani unaleta muunganiko mzuri na kuwajenga vijana katika mshikamano, upendo na uzalendo.

"Umoja kama huu unafaa sana kuwapo katika shule zetu kwani licha ya kuongeza mshikamano baina ya walimu, wazazi na wanafunzi pia huongeza uthubutu kwa wanafunzi na kujikuta wanafanya mambo makubwa zaidi na yenye faida kwa taifa," alieleza. Mkuu wa Shule hiyo Dk. Hashimu Saiboko, alieleza juu ya maendeleo ya shule hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016 wanafanikiwa kufanya mahafali ya kwanza ya kidato cha nne.

"Shule yetu imepitia changamoto nyingi tangu kuanzishwa kwake mpaka Leo, lakini tunawashukuru wazazi kwa namna walivyoshirikiana nasi katika kuzitatua changamoto hizo na hatimaye tunafanya mahafali haya ya kwanza tangu kuanzishwa kwa shule," alisema Dk. Saiboko. "Haikuwa kazi rahisi kufikia hatua hii, ilikuwa safari ngumu yenye changamoto nyingi, lakini ushirikiano wetu na wazazi na wadau mbalimbali wa elimu imetufanya tuonekane miongoni mwa shule bora inayoamini katika nidhamu, utii na taaluma," alieleza Dk. Saiboko.

Dk. Saiboko alisema kuwa malengo ya shule hiyo kwa mwaka 2020/2021 ni kuhakikisha wanakuwa na wanafunzi wa kidato cha tano.

# Tanzania yashauriwa kuongeza uvunaji gesi

**Na Beatrice Moses**

TANZANIA imetakiwa kuongeza kasi ya uvunaji wa gesi asilia na kuongeza matumizi ya nishati hiyo ili kunufaisha wananchi na kuiwezesha nchi kukua kiuchumi.

Serikali ilitangaza kuwa imekusudia kujenga vituo vya gesi vitatu, kikubwa kitakuwa eneo la Ubungo, ili mabasi ya mwendokasi ambayo yanatarajiwa kuwekewa mfumo wa kutumia gesi badala ya petroli kupata nishati hiyo kwa urahisi.

Hayo yamejiri jana kwenye uzinduzi wa kitabu cha 'Governing Petroleum Resources 'kinachoelezea kuhusu sekta ya madini na gesi asilia kilichoandikwa kwa utafiti uliofanywa na Repoa, kikasimamiwa na Prof. Beno Ndulu.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, Sebastian Shana ambaye ni Kamishna Msaidizi wa Gesi Wizara ya Nishati, alisema serikali imejipanga vyema katika kuhakikisha gesi inanufaisha wananchi.

"Watanzania waelewe kabisa kuwa rasilimali hii ni muhimu kwa maendeleo ya nchi, sasa zaidi ya asilimia 54 ya umeme unaotumika nchini kwa sasa unatokana na gesi, magari 300 yameunganishwa kwenye mfumo wa kutumia gesi," alisema.

Aliishukuru Repoa kutokana na kufanikisha kitabu hicho, akiahidi kwamba serikali itaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali katika kuendeleza sekta ya gesi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Repoa, Dk. Donald Mmari, alisema katika kitabu hicho waliangalia mambo mengi ikiwamo sera na sheria zinazohusu madini na gesi na wametoa mapendekezo.

Alisema wameangazia namna ambavyo uwazi unaweza kusaidia kuondoa uwezekano wa rushwa na matumizi mabaya. " Tumeangalia kwenye nchi nyingine za wenzetu wenye madini na gesi wapi lipatia na walipokosea," alisema.

Alisema lengo la kitabu hicho ni kuona rasilimali hiyo inasaidia kuinua sekta nyingine ikiwamo sekta ya elimu, uchukuzi na uchumi, na kuhakikisha wananchi wanapata ajira vipato vyao vinaimarika na kufikia uchumi wa kati kama vile dira yetu ya maendeleo inavyoelekeza.

Alisema yapo maeneo ambayo hatua zimepigwa ikiwamo matumizi ya umeme kwa viwanda vinavyotengeneza saruji hatua ambayo itasaidia kushusha gharama ya bidhaa hiyo.

Gesi ambayo ipo kwenye kina cha bahari, serikali ione jinsi ya kuizalisha gesi kutoka kwenye kina cha bahari, kwenye masoko makubwa yanayohitaji gesi nyingi ikiwamo Asia.

Dk. Mmari alibainisha kuwa pia ushirikishwaji wa wananchi na kampuni ndogo zinazojihusisha na gesi nalo ni jambo ambalo linapaswa kupewa umakini, kwa kuwa licha ya kuwafungulia fursa ya kuongeza kipato, itasaidia pia kuwekeza katika kujenga ujuzi kwa vijana katika sekta hiyo.

Mbunge wa Sengerema (CCM), William Ngeleja, alisema kuwa Tanzania kama zilivyo nchi nyingi za bara la Afrika imejaaliwa kuwa na rasilimali mbalimbali za asili na inajulikana kimataifa.

Ngeleja ambaye amewahi kuwa Waziri wa Nishati na Madini, alisema kitabu hicho kina mapendekezo mazuri umuhimu wa usimamizi wa uvunaji wa rasilimali hiyo, ili kunufaisha wananchi zaidi na kujipatia maendeleo.

# Wizi wa saruji wakwamisha ujenzi zahanati

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Kijiji cha Nyika Kata ya Imesela, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wameutuhumu uongozi wa kijiji uliopita kwamisha ujenzi wa zahanati kijijni humo, kutokana na kuibwa saruji mifuko 70 ambayo ilitolewa na Mbunge wao wa Jimbo la Solwa, Ahmed Salum.

Walibainisha hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge huyo ambao ulikuwa na lengo la kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi kuwa changamoto kubwa ambayo inawasumbua ni ukosefu wa huduma ya afya kutokuwa karibu, hivyo kulazimika kuifuata vijiji vya jirani kilomita saba.

Mmoja wa wananchi hao, Daniel Shija, alisema tatizo ambalo limekwamisha ukosefu wa huduma ya afya kwenye kijiji hicho linatokana na uongozi uliopita wa kijiji kutoonyesha ilipokwenda mifuko 70 ya saruji, ambayo ilitolewa na mbunge huyo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa zahanati.

"Mheshimiwa Mbunge, wewe tunakupongeza sana kwa kutujali wananchi wako, tunafahamu kabisa ulitoa mifuko 70 ya saruji kwa ajili ya kuanza ujenzi wa zahanati na ilifika hapa kijijini na tuliiona, lakini uongozi wa kijiji uliokuwapo waliuza saruji hiyo na kugawana fedha ukiwahoji wanakuwa wakali," alisema Shija.

"Baada ya wananchi kuwabana juu ya mifuko hiyo ya saruji imekwenda wapi, na kuwataka watusomee mapato na matumizi ya kijiji, wamekuwa wakipiga chenga, na hata hapa kwenye mkutano wako hawapo, wakijua kabisa suala hili lazima litazungumzwa ili watoe majibu sahihi kwako," aliongeza.

Naye Mbunge Salum alisema suala hilo la kufuatilia mifuko hiyo ya saruji 70 iliyotafunwa atauachia uongozi mpya wa kijiji walishughulikie, huku akitoa ahadi ya kuleta mifuko mingine 100 ya saruji ili waanze ujenzi wa zahanati kijiji humo.

Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji hicho aliyemaliza muda wake, Mihambo Nkwabi, alipohojiwa na Nipashe kwa njia ya simu kujibu tuhuma hizo, alisema mifuko hiyo ya saruji haikutafunwa, bali ilitumiwa kwenye matumizi mengine ya kujenga nyumba za walimu.

## NMB yajikita huduma uhifadhi wa dhamana za wawekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeanzisha mchakato wa kuwavutia wateja katika huduma yake ya uhifadhi wa dhamana na usimamizi wa uwekezaji katika masoko ya mitaji. Lengo la huduma hii, iliyoanza rasmi kupatikana ndani ya Benki ya NMB Machi mwaka huu, ni kuongeza idadi ya Watanzania wanaojihusisha na uwekezaji katika dhamana za serikali na pia soko la hisa.

Huduma ya uhifadhi wa dhamana inahusisha benki kutunza dhamana za wateja wake. Huduma hii pia huhusisha benki kuzisimamia akaunti za dhamana za wateja wake; kukamilisha miamala inayofanyika katika dhamana hizo kwa niaba ya wateja na kukusanya gawio na kulipa riba kwa niaba ya mteja.

"Kimsingi, lengo ni kuhakikisha benki inafanya kila kitu kinachotakiwa kufanywa na mwekezaji aliyewekeza katika dhamana za serikali kwa niaba ya wateja ili kutoa nafasi kwa wao (wateja) kujikita zaidi katika biashara zao za msingi," alisema Ofisa Mkuu wa wateja Binafsi, Biashara ndogo na za kati, Filbert Mponzi.

Mweka hazina wa benki hiyo, Aziz Chacha, akisema mara nyingi wawekezaji hujitokeza kwa wingi kununua dhamana za serikali za muda mrefu kila inapotokea nafasi ya serikali kuuza dhamana zake kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Matokeo yake ni kuwa Benki Kuu hulazimika kurudisha sehemu ya pesa zilizokusanywa kwa wawekezaji ili kubaki na kiasi kinachotakiwa pekee.

Agosti mwaka huu Benki ya NMB ilitangaza matokeo ya mauzo ya toleo la tatu la hati fungani yake yaliyofunguliwa Juni 10, mwaka huu ambapo matokeo yalionyesha kuwa wawekezaji waliwekeza kiasi cha pesa ambacho kilivuka malengo kwa asilimia 33.

"Kazi yetu ni kurahisisha jinsi ya kuwekeza katika amana hizi za serikali. Unachotakiwa kufanya ni kuongea na sisi na tutakuunganisha na Benki Kuu na biashara inafanyika," alisema Agnes Mayoro kutoka idara ya Hazina ya benki hiyo. Kwa mujibu wa meneja mwandamizi wa huduma za dhamana kutoka, Avith Massawe, miongoni mwa kazi ambazo benki itazifanya kwa niaba ya mwekezaji ni pamoja na kukamilisha miamala ya dhamana za serikali zilizouzwa katika soko la awali na soko la upili). Litakuwa pia ni jukumu la benki kuandaa taarifa kamili ya biashara ya dhamana hizo ilivyokwenda na kutuma kwa mwekezaji mara moja kwa mwezi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa la Dar es Salaam, Moremi Marwa, alisema mpaka sasa ni wawekezaji wapatao 550,000 kati ya Watanzania zaidi ya milioni 45 ambao hujihusisha na mauzo ya hisa na amana za serikali na hatifungani za kampuni zinazouzwa katika soko hilo la hisa.

Meneja wa masoko ya fedha kutoka BoT, Lameck Kakulu, alisema hati fungani ya Serikali ya miaka 20 hutoa faida ya asilimia 17, hivyo kufanya uwekezaji katika dhamana za serikali kuwa moja kati ya maeneo yenye faida zaidi kwa wawekezaji.

# Viashiria hatarishi vya uchumi vyadhibitiwa

**Na Elizabeth Zaya,**
BAGAMOYO

WIZARA ya Viwanda na Biashara, imesema katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, imefanikiwa kudhibiti mianya ya viashiria hatarishi vya uchumi na maendeleo nchini.

Kamishna wa Vipimo wa Wizara hiyo, Dk. Ludovick Christian, aliyasema hayo mjini Bagamoyo wakati akifungua kongamano la pili la Taasisi ya Kudhibiti Viashiria Hatarishi vya Uchumi na Maendeleo Tanzania (IRMT) lililowakutanisha wadau kutoka sekta ya umma na binafsi.

Dk. Christian alisema moja ya viashiria ambavyo serikali imefanikiwa kudhibiti kwa miaka minne ni matumizi mabovu ya fedha za umma na usimamizi mbaya wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na shughuli nyingine zinazo husiana na jamii.

Alisema katika kufikia malengo ya uchumi wa viwanda kuna umuhimu wa kuendelea kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma na usimamizi bora wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali.

"Sasa tunaenda kwenye uchumi wa viwanda, ambao una mambo mengi ambayo yanatakiwa yaangaliwe kwa ufanisi zaidi, na moja ya vitu vinavyotakiwa visimamiwe kwa ufanisi zaidi ni viashiria vya kuleta matokeo hasi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku," alisema Dk. Christian.

Alisema kutokana na mabadiliko ya teknolojia kuna uwezekano mkubwa wa kuwapo kwa viashiria hivyo kutokana na watu kubuni mbinu mbalimbali kwa nia ovu ya kudororesha uchumi.

"Kwa sababu ya mabadiliko ya teknolojia, hata viashiria vya kuleta athari katika maendeleo ya uchumi navyo vinakuwa vingi, kwa hiyo bila kuwa na uangalifu wa kudhibiti matumizi ya fedha za umma tunaweza kukwama kufikia malengo yetu tuliyojiwekea katika upande wa serikali hata sekta binafsi," alisema Dk. Christian.

Rais wa IRMT, Pius Maneno, alisema wamejipanga kutumia teknolojia kuvitambua vihatarishi hivyo na kuvidhibiti kabla ya kuleta athari.

Katibu Mtendaji wa IRMT, Fredrick Mgaya, alisema tangu taasisi hiyo ianze imesaidia kutoa mafunzo kwa mashirika ya umma na binafsi na imezalisha wataalamu 76 na kutengeneza mifumo ya ndani ya kudhibiti viashiria hivyo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene (kulia), akiteta jambo na Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini, Manfredo Fanti, baada ya kufanya mazungumzo ya awali juu ya kuhuisha miradi mbalimbali ya utunzaji wa mazingira kwa mwaka 2021/2027 inayofadhiliwa na Jumuiya hiyo nchini. **MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 5/- kupeleka maji Bukene

**Na Tiganya Vincent,**
TABORA

SERIKALI itatumia Sh. bilioni 5 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa bomba za maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Bukene wilayani Nzega mkoani Tabora.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alipopita wilayani Nzega kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda mkoani Tabora.

Alisema fedha za ujenzi wa mradi huo zipo na usanifu wa mradi huo umeshafanyika ambapo utakuwa umbali wa kilometa 36 kutoka maji yatakapochukuliwa kwenye tenki la maji la Ushirika lilipo Nzega mjini hadi Bukene. Prof. Mbarawa alisema katika mpango wa awali Bukene haikuwapo kwenye mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, ,lakini Serikali imetafuta fedha kwa ajili ya kujenga mradi huo. Alisema kwa kuwa fedha zipo kazi hiyo itaanza mara moja ambapo kukamilika kwake utasaidia kutatua tatizo la maji katika vijiji 19 vya Bukene kwa kuwahakikishia wakazi wa eneo hilo wanapata majisafi na salama mapema.

Alisema utekelezaji wa mradi wa kuleta kutoka Ziwa Victoria kwa ujumla umefikia asilimia 85 na anatarajia kuanzia Desemba utakuwa umekamilika kwa kiwango kikubwa na wananchi wataanza kupata maji safi na salama.

Aliongeza kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha inapeleka majisafi na salama kwa wananchi wengi ili kuwaondolea tatizo la maji.

Awali Mhandisi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mkoani Tabora (TUWASA), Athuman Kilundumya, alisema zaidi ya watu 240,000 wanatarajia kunufaika na ongezeko la eneo la utekelezaji wa mradi wa maji kutoka ziwa Victoria katika Wilaya za Igunga, Nzega na Uyui.

# Mradi wa bil. 520/- waikuna wizara

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WIZARA ya Maji na imesema imeridhishwa na utekelezaji wa ujenzi wa mradi mkubwa wa maji wa Sh. bilioni 520 unaotekelezwa katika Jiji la Arusha.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara ya kutembelea mradi huo, Mkurugenzi wa Idara ya Usambazaji wa Maji na usafi wa Mazingira kutoka wizarani, Nadhifa Kemikimba, alisema ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo. Alisema lengo la serikali ifikapo Juni mwaka 2020 upatikanaji wa huduma ya maji kwa mijini uwe kwa asilimia 95 na kwa maeneo ya vijijini kwa asilimia 85.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alisema awali mradi wa ujenzi wa makao makuu ya Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira (AUWSA) ulikuwa ukisuasua, lakini baada ya ofisi yake kwa kushirikiana na wataalamu kumsimamia mkandarasi kwa makini sasa ujenzi huo unaendelea vizuri. "Awali tulipotembelea mradi huu ujenzi ulikuwa ukisuasua na ulikuwa umefikia asilimia 7.5, lakini baada ya kumsimamia makandarasi sasa umefikia asilimia 10 hii ni hatua kubwa," alisema Gambo.

Alisema kwa muda mfupi wa usimamizi wa mradi huo, kuna mabadiliko makubwa yaliyotokea kutokana na jitihada za ofisi yake na wataalamu kwa ujumla.

Kaimu Mkurugenzi wa AUWSA, Mhandisi Justine Mwangijomba, alisema mradi huo umefikia hatua ya kusafisha mtandao wa mabomba yanayopeleka maji kwenye tanki sambamba na kuweka dawa.

"Tumepita katika tanki letu la maji la lita milioni 10, pia ujenzi wa tanki hilo umekamilika hivyo muda siyo mrefu wananchi watapata ongezeko la huduma ya maji," alisema Mwangijomba.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, alisema kukamilika kwa mradi huu kutapunguza tatizo la maji kwa wakazi wa Arusha.

Alisema kwa sasa maji yanapatikana kati ya lita milioni 40, kwa kipindi cha kiangazi na milioni 60, kwa kipindi cha masika wakati mahitaji halisi ni lita milioni 90 kwa wakazi wa Jiji la Arusha.



Mhifadhi mambo kale katika Hifadhi ya Ngorongoro, Godfery Ollemoita, (kulia) akiwaelezea Wabunge na Wajumbe kutoka Shirikisho la Watu wenye Mahitaji Maalum Udongo unaohama walipotembelea hifadhi hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: BUNGE**

# Wakulima mpunga Lekitatu wafunguka

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAKULIMA wa mpunga katika eneo la Lekitatu, mkoani Arusha, wameisifia Kampuni ya Yara Tanzania kwa kusema kwamba imewapa mbolea sahihi na huduma za ugani ambavyo vimeongeza vikubwa mavuno ya zao hilo.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana ambao walitembelea eneo hilo, wakulima wamedai kuwa juhudi za Yara Tanzania katika kukuza mazao ni kichocheo cha kufikia uchumi wa kati.

"Serikali inazungumza habari ya Tanzania kufikia uchumi wa kati. Mambo yanayofanywa na kampuni hii (Yara Tanzania) ni kichochezi cha kufikia uchumi wa kati," alieleza Anneth Moshi.

Moshi alisema huduma za Yara zinachochea kuinuka kwa kipato cha wakulima na hivyo kufikia azma ya serikali ya ujenzi wa viwanda na uchumi wa kati.

"Nimelima mpunga tangu mwaka 2004 na kwa miaka mingi sikuwahi kupata zaidi ya magunia 15 kwa ekari moja. Lakini tangu nimeanza kutumia mbolea za Yara uzalishaji umeongezeka na kufikia magunia kati ya 30-35 kwa ekari," alisema Moshi.

Joel Msangi alisema huko nyuma wakulima wamekuwa wanaendesha kilimo cha mazoea tena wakitumia mbolea bila elimu ya matumizi sahihi ya mbolea na aina ya udongo unaofaa kwa zao mpunga.

"Ukosefu wa elimu ya kutosha juu ya matumizi ya mbolea, kutokuwapo kwa elimu ya upimaji wa udongo na muda sahihi wa kuweka mbolea ni miongoni mwa changamoto chache zilizokuwa zinafanya tupate mazao kidogo. Lakini ujio wa mbolea za Yara kwetu imekuwa ni ukombozi mkubwa," alifafanua Msangi.

Mkulima huyo alisema mbolea za YARA zina virutubisho vyote muhimu vya ukuaji wa mmea mpaka kuvunwa kwa mazao.

## Polepole amkabidhi kadi aliyekuwa Meya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Humphrey Polepole, amemkabidhi kadi ya uwanachama kwa aliyekuwa Meya wa Jiji la Arusha, Kalisti Lazzaro na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha DC.

Akizungumza juzi wakati akifunga kampeni za chama hicho katika viwanja vya soko la Sombetini, jijini Arusha Polepole alisema amewakabidhi kadi za uwanachama viongozi hao ili waendelee kufanya kazi ya kuwahudumia wananchi.

"Kalisti tangu mwanzo hakuwahi kuibeza serikali wala kubeza maendeleo yaliyofanywa na serikali," alisema Polepole. Alisema kwa Jiji la Arusha tangu alipokuwa meya alifanya kazi kubwa za kimaendeleo ambazo hadi sasa serikali wanazitambua kutokana na juhudi zake za kuchapa kazi.

Katika hatua nyingine Polepole aliwaapishwa viongozi hao waliohama kutoka Chadema mbele ya wananchi, wanachama na makada wa CCM.

Naye Lazaro alisema amefurahia kujiunga na chama hicho, na amewaomba wanachama kumpokea na kumpa ushirikiano.

ya taarifa zinakosekana kutokana na wazee wa zamani waliokuwa wakitabiri wengi wao kufariki.

## Wapewa elimu tabia za nchi

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WANANCHI wa Vijiji sita vya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wamepatiwa elimu ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa yanayosababisha mifugo na kilimo kuathirika.

Aidha vijiji vilivyonufaika na mafunzo hayo ni Korongo, Magadini, Kitwai A na B, Olchoronyori, pamoja na Loonderkes.

Ofisa ufuatiliaji na tathmini wa mradi wa ardhi yetu kutoka shirika lisilo la kiserikali la Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF), Rogath Massay, alisema wilaya hiyo asilimia 80 ni wafugaji na ufugaji ndiyo unaowapatia kipato na chakula.

Alisema kutokana na hali hiyo, ameona vema wawape elimu hiyo ili kuwanusuru na mabadiliko hayo kwenye sekta za mifugo, kilimo, uvuvi, na uchimbaji wa madini.

Rogath alisema kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), wanaijengea jamii uwezo kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili iondokane na changamoto mbalimbali ikiwemo ya taarifa kutofika kwa wakati kwao.

Ofisa Kilimo Wilaya ya Simanjiro, Jenifa Mbuya, alisema taarifa za utabiri wa hali ya hewa za kijadi na kisayansi ni msaada mkubwa kwa wakulima na wafugaji, ingawa baadhi ya taarifa zinakosekana kutokana na wazee wa zamani waliokuwa wakitabiri wengi wao kufariki.

## Mbinu za zamani uhifadhi mazingira sasa kurejeshwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI imekubali kurejea mbinu zilizokuwa zikitumiwa na wazee kuhifadhi mazingira miaka nyuma ambazo hazikuleta athari ya mabadiliko ya tabianchi yaliyochomoza miaka ya hivi karibuni.

Akizungumza jana na wadau wa mazingira kwa niaba ya mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, alisema ni vyema wadau wa mazingira wakajifunza kutoka kwa wazee na kujua ni aina gani ya miti inayotakiwa kuoteshwa ili kuhifadhi uoto wa asili.

"Wazee wanajua aina gani ya miti ambayo inahifadhi maji na inatakiwa kuoteshwa sehemu gani, na wakati gani hivyo wataalamu wakitumia wazee mkoa huu utarudisha hali yake ya zamani," alisema.

Alisema nishati mbadala zimekuwa ni garama kubwa kwa maisha ya wanachi wenye kipato cha chini, hali ambayo inasababisha wananchi kuendelea kuharibu mazingira.

Mkurugenzi wa Shirika la Foresta Tanzania, Richard Mhina, alisema shirika hilo limekuwa likihifadhi mazingira mkoani kilimanjaro kwa kuwaelimisha wananchi kulima kilimo rafiki.

Alisema shirika hilo lina vikundi 411 katika mkoa huo vinavyojihusisha na utunzaji wa mazingira, na kwamba kwa mwaka huu wanaotesha miti 1,600,000.

# Ndugai aifunda wizara maliasili na utalii

**Na Mary Mosha,**
KILIMANJARO

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameitaka wizara ya Maliasili na Utali kujitathmini kupitia maofisa misitu kwa kuwa wamekuwa chanzo cha ujangili katika eneo la kazi.

Aliyasema hayo wakati wa mahafali ya 55 ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka.

Alisema upo umuhimu wa wizara kujitathmini katika vyuo wanavyopata mafunzo na maadili ili kuleta mabadiliko katika sekta ya maliasili na utalii licha ya serikali kudhibiti ujangili kwa asilimi 90.

"Mimi nimepata mafunzo katika chuo hikii, nilifundishwa kujiamini na kutobabaishwa na mazingira ...ndio maana hata leo unaponiona naweza kusimama bungeni licha ya moto mkali wakati mwengine unapowaka," alisema na kuendelea:

"Katika kambi yoyote tuliyokuwa tukienda kwa ajili ya mazoezi tulionekana kuwa bora na wenye maadili, hatukubabaishwa na mazingira licha ya kuwa na mazingira magumu ya kufanyia kazi."

Aidha aliitaka wizara hiyo kuacha tabia ya ubabe wa kutumia silaha kila mara kwa wananchi na badala yake kutoa elimu kwa wananchi waishio pembezoni mwa hifadhi kuwapenda na kuwalinda wanyama.

"Hatumaanishi kuwa mtupe silaha chini ili kuruhusu ujangili bada yake hakikisheni mnaweka nguvu kubwa katika kutoa elimu kwa wananchi wa pembezoni mwa hifadhi zetu, msisahau kuishauri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknologia ili kuweka mitaala maalumu kuanzia shule za awali hadi vyuoo vikuu ili kuwasaidia kuwafahamu wanyama wetu, rasilimali zetu na kuwa wazalendo," alisema.

Wakati huo huo, Ndugai aliitaka wizara hiyo kuangalia sheria ambazo hazieleweki ili zipelekwe bungeni ili kufanyiwa kazi na kuleta mabadiliko katika sekta ya utalii.

"Bunge lenu lipo, ikiwa kuna sheria mbovu leteni tuzifanyie kazi ili sekta ya utalii ikue na kuleta tija kwa taifa wakati tunapoelekea uchumi wa kati," alisema Spika.

Akimkaribisha mgeni rasmi wa mahafali hayo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, alisema wizara hiyo inatambua wanakabiliwa na changamoto nyingi hasa katika vyuo, lakini wameshaanza kutatua kidogo kidogo.

"Tumetambua kuna utofauti mkubwa kati ya wanafunzi wanaomaliza Mweka na wa vyuo vingine wawapo eneo la kazi, tumeshaandaa utaratibu maalum wa kuhakikisha wote wanapita mafunzo Jeshi Usu ili kukabiliana vyema na matukio ya ujangili," alisema.

Nao baadhi ya wanafunzi, Samson Edward alisema mafunzo wanayoyapata katika chuo hicho yanawafanya kuwa na nguvu ya kukabiliana na changamoto mbalimbali zikiwamo za mishahara midogo wawapo kazini na ujangili.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA), Dk. Charles Msonde akitoa neno kwa wahitimu wa kwanza ya kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Kiislam Ihsan iliyopo Kigamboni jijini Dar es salaam kwenye mahafali yaliyofanyika mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkuu wa Shule hiyo, Dk.Hashim Saiboko, kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na wapili kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya shule hiyo Mhandisi Musa Nyamsingwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wataka kila mwanafunzi kupanda mti

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wadau wa mazingira Manispaa ya Moshi, wametoa mapendekezo kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha wanafunzi watakaoandikishwa kuanza darasa la kwanza mwaka 2020, na wale waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 2020 kila mmoja aoteshe mti wake mmoja.

Lengo la kufanya hivyo wamesema ni kuboresha hali ya mazingira nchini. Wadau hao walitoa mapendekezo yao kwa wizara hiyo ili ipeleke bungeni muswada wa marekebisho ili kumtaka kila mwanafunzi atakayejiunga na elimu yake ya msingi na ya sekondari kupanda mti wake mmoja inayotolewa na wadau wa mazingira na kuutunza hadi hapo atakapomaliza elimu yake.

Hayo yamo kwenye risala iliyosomwa na Sophia John, wakati wa zoezi la uoteshaji miti ya asili katika maeneo ya taasisi za umma, binafsi na kwenye makazi ya watu.

zoezi ambalo lilifanyika katika Kata ya Majengo mjini Moshi juzi na kuratibiwa na asasi isiyo ya kiserikali inayojishughulisha na utunzaji wa mazingi ya Kibo Environment Conservation Group ya Manispaa ya Moshi.

Pia wamewaomba walimu wa shule za msingi na sekondari kuanzisha mashindano ya upandaji wa miti ili kila mtoto anayeingia shuleni hapo anaotesha mti wake mmoja, jambo ambalo litasaidia katika kabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Akizindua zoezi hilo la miti ikiwa ni siku ya kumuenzi aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Leonidas Gama, Ofisa Mazingira Manispaa ya Moshi, Emanuel John, alisema kuwa Manispaa hiyo imeanzisha kampeni ya kukamata mifugo yote inayozurura mitaani na kuharibu miti inayopandwa ili kulinda na kutunza mazingira.

Alifafanua kuwa serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa za kupanda miti katika maeneo mbalimbali na kwa manispaa ya Moshi, na kuwa kampeni hiyo ilianzishwa na Marehemu Gama tangu mwaka 2012.

Mkurugenzi wa Kibo Environment Conservation Group, Daniel Mvungi, alisema kutokana na uharibifu kubwa wa mazingira ikiwamo ukataji miti kwa ajili ya kujipatia nishati ya kuni na mkaa, asasi hiyo imeanzisha siku maalumu ambayo itakuwa ikifanyika Novemba 22 ya kila mwaka kupanda miti, ili kumuenzi Gama, ambaye alisimama katika kuhakikisha Mkoa wa Kilimanjaro unaendelea kuwa mkoa wa kijani.

Naye Kamishna wa Skauti Tanzania Manispaa ya Moshi, Mbena Emerensiana, alisema upandaji wa miti ni njia moja wapo ya utunzaji wa mazingira na kulinda uoto wa asili, hivyo Skauti Tanzania itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kushiriki kupanda miti ambayo itasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

NIPASHE JUMATATU NOVEMBA 25, 2019

Nipashe Spotika



WANASOKA 10 WANAOLIPWA PESA NDEFU ZAIDI DUNIANI UK. 16&17

## ISIKUPITE

TANGU alipoanza kazi ya ukocha kwa kuinoa Benfica Septemba 2000, Jose Mourinho hajawahi kupoteza mechi yake ya kwanza katika klabu nane alizozifundisha hadi sasa, ikiwa ni pamoja na vipindi viwili tofauti alivyoinoa Chelsea (Kashinda 5, Sare 3).



### MECHI ZA KWANZA ZA MOURINHO

| | |
|---|---|
| BENFICA (2000) | L 1-0 |
| U LEIRIA (2001) | D 0-0 |
| PORTO (2002) | W 2-1 |
| CHELSEA (2004) | W 1-0 |
| INTER (2008) | D 2-2 |
| R MADRID (2010) | D 0-0 |
| CHELSEA (2013) | W 2-0 |
| MAN UTD (2016) | W 2-1 |



# KIMGONGOMGONGO...

Kiungo wa Manchester City, Kevin De Bruyne (kulia) akimdhibiti kiungo wa Chelsea, N'Golo Kante katika mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Etihad na City kushinda 2-1 juzi. **PICHA: MTANDAO**



# CHANGAMOTO 10 ZA MOURINHO TOTTENHAM

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amechukua mikoba ya kuinoa Klabu ya Tottenham Hotspurs timu inayoshika nafasi ya 14 kwenye msimamo na ikiwa haijashinda mchezo wowote wa ligi kwa miezi miwili. Atawezaje kuirudisha klabu kwenye ubora wake?

**Mourinho alitua Tottenham akikabiliwa na changamoto kubwa, akirithi kikosi chenye matokeo mabaya katika mwanzo wake wa Ligi Kuu kwa kipindi cha muongo mmoja na imepitwa pointi 11 kutoka kwenye nne bora.**

Lakini ni changamoto gani inayomkabili Mourinho pale Spurs? Hapa tunazichambua changamoto 10, twende sasa...

**1. KURUDISHA KIWANGO**

Kiwango cha sasa cha Tottenham kwenye Ligi Kuu ni kibaya zaidi. Hawajashinda mechi ya ligi tangu Septemba 28. Tangu walipofungwa na Newcastle Agosti, kiwango chao kimekuwa cha ovyo.

Mtihani wa kwanza wa Mourinho utakuwa ni kurudisha kiwango bora cha Tottteham.

**2. KUTAMBULISHA STAILI YAKE**

Spurs imekuwa na falsafa yake kwa kipindi cha miaka michache iliyopita kwa soka la kushambulia na kutawala mchezo. Na hiyo siyo stali ya Mourinho, hivyo jukumu lake jingine ni kutambulisha staili yake klabuni hapo.

**3. USHINDI BILA MASHAKA**

Ujio wa Mourinho umepokelewa kwa mtazamo tofauti na mashabiki 'damu' wa Tottenham ambao walitilia shaka staili yake ya kucheza na hasa alivyoshindwa kufanikiwa pale Old Trafford. Atarudi kuwa yule Mourinho wa zamani aliyeshinda taji la Ligi Kuu England mwaka 2005, 2006 na 2014?

Tabia yake ni tofauti na Pochettino ambaye ni mara chache mno alikuwa akiwalaumu wachezaji kwa matokeo mabaya dimbani na Mourinho yeye mdomo wake hauna breki kwenye kulaumu wachezaji.

**4. KURUDISHA UBORA WA ERIKSEN NA ALLI**

Wakati Spurs ilipokuwa kwenye ubora wake chini ya Pochettino, wachezaji Dele Alli na Christian Eriksen ndio walikuwa kama moyo wa timu. Lakini sasa wote hawapo kwenye kiwango chao.

Mkataba wa Eriksen limekuwa jambo ambalo halijatatuliwa, huku Alli alishutumiwa na Roy Keane mwezi uliopita kwa kupoteza ubora wake, je, Mourinho ataweza kulimaliza hilo?

**5. KUIMARISHA SAFU YA ULINZI**

Haihitaji utafiti wa kisayansi kujua nini kinachoisumbua Tottenham kwa sasa. Kwa kipindi hiki cha msimu wa 2019/20, wamekuwa wakishambuliwa zaidi tofauti na miaka mitatu iliyopita. Kwa kipindi cha miaka mitatu walikuwa nafasi ya kwanza kwa kuwa na safu bora zaidi ya ulinzi kwenye Ligi Kuu. Lakini hadi sasa wameruhusu kufungwa mabao 18 kwenye mechi 12 na wamecheza mchezo mmoja tu bila kuruhusu bao.

**6. MIKATABA YA WACHEZAJI**

Moja ya kitu kikubwa ambacho Pochettino kilikuwa kinamsibu ni wachezaji watatu Eriksen, Toby Alderweireld na Vertonghen - ambao waliruhusiwa kuingia kwenye mwaka wao wa mwisho wa mikataba yao bila kusaini mipya. Hilo limeleta athari kubwa kwa kikosi.

Mourinho lazima aamue kama wachezaji hao watakuwa sehemu ya mipango ya kikosi chao ili kuwawezesha kusaini mikata mipya, kwani kwa sasa ni wazi kwamba wataondoka mwishoni mwa msimu wakiwa wachezaji huru.

**7. KUSHINDA TAJI**

Tottenham licha ya kuwa na maendeleo na mafanikio makubwa kiuchezaji dimbani na kuonyesha kiwango cha kuvutia chini ya Pochettino, lakini hawakuwahi hushinda taji lolote. Walikaribia kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kutinga fainali Juni, hata hivyo, wakafungwa na Liverpool. Lakini Kombe la Ligi la msimu wa 2007/08 ndio linabaki kuwa taji pekee walilolibea Spurs kwa kipindi cha miaka 20.

Hivyo, kipaumbele cha kwanza kwa Mourinho ni lazima ashinde taji na klabu hiyo.

**8. KUJENGA KIKOSI NA BAJETI**

Mourinho aliahidiwa kupewa fedha na kuimarisha kikosi wakati wa kipindi cha majira ya joto Januari na kipindi cha majira ya joto wakati akiwa kule Manchestet United. Lakini deni la Tottenham la uwanja wao mpya ni ngumu hilo kuwezekana. Uwezekano wa Tottenham kumpatia fungu la bajeti inaweza kuwa changamoto kubwa kwao.


**9. KUSAJILI WAPYA**

Kikosi bado kinahitaji kufanyiwa kazi, lakini Mourinho amerithi wachezaji wapya waliosajiliwa, Tanguy Ndombele, Giovani Lo Celso na Ryan Sessegnon. Wachezaji hao waliwasili hapo kwa jumla ya pauni milioni 140 na kwa vyovyote Mourinho atahitaji kusajili wachezaji wapya zaidi.

**10. KUNUNUA WA MUDA MREFU**

Mounrinho anatakiwa kuwa na mpango au mradi wa muda mrefu katika kusajili wachezaji wa kikosi hicho. Hii inamaana kwamba, kama Mourinho anataka kuimarisha kikosi chake kuendelea kuwa na ushindani kwenye Ligi Kuu ya England ni lazima anunue wachezaji ambao atakaa nao kwa muda mrefu.

**JE, WAJUA?**



Arsenal imekabiliwa na penalti tano kwenye Ligi Kuu msimu huu, ambazo ni nyingi zaidi kuliko zilizotolewa kwa timu nyingine kwenye ligi hiyo. Aidha, Bernd Leno amekuwa kipa wa kwanza Arsenal kuokoa mkwaju wa penalti kwenye Ligi Kuu tangu Peter Cech alipofanya hivyo dhidi ya Watford Machi 2018.



Winga wa Kilimanjaro Queens Mwanahamisi Omari 'Gaucho', akitafuta mbinu za kumtoka beki wa Burundi kwenye mechi ya Kombe la Challenge Wanawake katika Uwanja wa Chamazi wiki iliyopita.

# HAT-TRICK ZILIVYOFUNIKA CECAFA YA WANAWAKE

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI leo timu ya soka ya Wanawake ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Queens ikitarajia kucheza fainali ya Kombe la Cecafa Challenge kwa Wanawake dhidi ya Kenya, michuano ambayo ni maalum kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, jumla ya mabao 78 yamefungwa kwenye michezo 14 ya michuano hiyo mpaka sasa.

**Mechi hizo ni kuanzia kwenye hatua ya makundi ambako zilichezwa mechi 12 na mbili za nusu fainali.**

Kilimanjaro Queens kama itashinda leo, basi itakuwa imelichukua kombe hilo kwa mara tatu mfululizo, kwani imeshalichukua kwenye michuano hiyo ilipofanyika nchini Rwanda na Uganda.

Kwenye mechi ya nusu fainali, Kili Queens, iliichapa Uganda bao 1-0, huku Kenya ikiitandika Burundi mabao 5-0.

Michuano ya msimu huu imekuwa na msisimko mkubwa kutokana na umati wa mashabiki kujitokeza kwa wiki kwenye Uwanja wa Azam Complex kushuhudia kandanda hilo la wanawake, huku wakionyesha soka la hali ya juu, ingawa baadhi ya timu zikionekana kuwa dhaifu sana. Timu za Kenya, Uganda, Ethiopia na Djibouti zilikuwa kwenye Kundi A na timu za Kili Queens, Zanzibar Queens, Sudan Kusini na Burundi zilikuwa Kundi B

Mwandishi wa makala haya amekusanya takwimu mbalimbali za michuano hiyo ilipoanza hadi nusu fainali, hizi hapa...

**1. HAT-TRICK SABA**

Jumla ya hat-trick saba zimepatikana kwenye michuano hiyo hadi kufikia hatua ya nusu fainali.

Mwanahamisi Omari alifunga hat-trick ya kwanza kwenye michuano hiyo katika mechi kati ya timu yake ya Kilimanjaro Queens dhidi ya Sudan Kusini, ikishinda mabao 9-0, Juliet Nalukenge, Fazila Ikwaput na Asifa Nasuuna wa Uganda wakipiga hat-trick zao kwenye mechi kati ya timu yao dhidi ya Djibouti, wakishinda mabao 13-0.

Jentrix Shikangwa wa Kenya na mwenzake Mwanalima Jereko wao walifunga hat-trick kwenye mechi dhidi ya Djibouti, wakiipa ushindi timu yao kwa mabao 12-0, huku Erehiman Zelega wa Ethiopia naye akijipatia hat-trick yake kwenye mechi dhidi ya Djibouti, timu yake ikishinda mabao 8-0.

**2. PENALTI SITA**

Penalti sita zimepatikana kwenye michuano hiyo hadi hatua ya nusu fainali huku zote zikiwekwa wavuni.

Jentrix Shikangwa wa Kenya amefunga penalti mbili kwenye mechi dhidi ya Ethiopia na Djibouti, Asifa Nasuuna wa Uganda akifunga mbili kwenye mechi moja ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Djibouti, Mercy Airo wa Kenya naye akifunga penalti mbili kwenye mechi moja dhidi ya Djibouti.

**3. KILI QUEENS YAFUNGA MABAO 21**

Timu ya Kilimanjaro Queens imeweka rekodi ya aina yake, baada ya kufunga mabao 21 kwenye mechi nne, huku ikiwa haijaruhusu wavu wake kuguswa.

Hadi kufikia hatua ya fainali, timu hiyo iliichapa Sudan Kusini mabao 9-0, ikaichapa Burundi mabao 4-0, ikaishindilia Zanzibar Queens mabao 7-0, kabla ya kuifunga Uganda bao 1-0 katika mechi ya nusu fainali juzi.

**4. STRAIKA WA KENYA KUCHEKA NA NYAVU**

Jentrix Shikangwa wa Kenya ndiye straika hatari kwenye michuano hiyo mpaka sasa akiongoza kwa kupachika mabao tisa.

Kwenye mechi ya fainali leo, mabeki wa Kili Queens wanapasa wamchunge zaidi, pamoja na winga Mwanalima Jereko.Mabao ya Shikangwa ambayo mawili ni ya penalti, moja alilifunga kwenye mechi dhidi ya Ethiopia, matano kwenye mechi dhidi ya Djibouti, moja dhidi ya Uganda na mawili kwenye mechi ya nusu fainali dhidi ya Burundi.

**5. ZANZIBAR YAONGOZA KWA KUJIFUNGA**

Mabao matatu ya kujifunga yamepatikana hadi hatua ya nusu fainali, huku Zanzibar Queens ikiongoza kwa kujifunga mawili.

Mwajuma Abdallah na Aziza Mwadini wa Zanzibar walijifunga wenyewe pamoja na Sumeiya Abdi ambaye ni kipa wa Djibouti.

Aziza alijifunga kwenye mechi dhidi ya Burundi na Mwajuma dhidi ya Sudan Kusini, huku kipa wa Djibouti akijifunga kwenye mechi dhidi ya Ethiopia.

**6. ZANZIBAR, DJIBOUTI ZAONDOKA BILA BAO**

Timu ya Djibouti iliyokuwa Kundi A na Zanzibar iliyokuwa Kundi B, zimeondoa kwenye michuano hiyo bila kufunga bao hata moja.

Timu hizo ambazo zimeshika mkia kwenye makundi hayo, hazikufanya chochote cha maana zaidi ya kugawa pointi na mabao.

Djibouti ilichapwa mabao 13-0 dhidi ya Uganda, 12-0 dhidi ya Kenya na 8-0 dhidi ya Ethiopia, wakati wenzao wa Zanzibar walipata vipigo vya mabao 5-0 dhidi ya Burundi, 5-0 dhidi ya Sudan Kusini, kabla ya kushindiliwa mabao 7-0 dhidi ya Kili Queens.

**7. ZANZIBAR, DJIBOUTI ZAFUNGWA MABAO 50**

Timu hizo zimefungwa jumla ya mabao 50 kwenye michuano hiyo ya Challenge mwaka huu.

Kwenye mechi zote tatu, Djibouti imefungwa jumla ya mabao 33, huku Zanzibar ilifungwa jumla ya mabao 17, hivyo jumla kuu inakuwa 50 ambayo timu hizo mbili zimefungwa.

**NJE YA UWANJA**

KIUNGO wa Manchester City, Kevin de Bruyne, amehusika katika mabao mengi ya mechi za nyumbani kuliko mchezaji mwingine yeyote katika Ligi Kuu England msimu huu (mabao tisa - akifunga matatu, pasi za mwisho sita).



# WANASOKA 10 WANAOLIPWA PESA NDEFU ZAIDI




**LONDON,** England

MPIRA wa miguu ndio mchezo unaojulikana zaidi na ukweli kwamba fedha nyingi zinahusishwa, angalau kwa kusema hivyo.

**Wachezaji kama Lionel Messi na Cristiano Ronaldo bila shaka yoyote ndio wachezaji wanaolipwa kiasi kikubwa zaidi cha fedha kwa sasa.**

Makala haya yanakuchambulia wanasoka 10 wanaolipwa kiasi kikubwa zaidi cha fedha duniani kwa sasa, shuka nayo...

### 10. OSCAR (SHANGHAI SIPG)

Mkataba wa sasa wa miaka minne unamfanya aiingize kiasi cha dola milioni 26 kwa msimu (2017-2021). Matangazo binafsi yanamfanya aingize dola milioni 3 na hivyo jumla yake kuwa na kiasi cha dola milioni 29 na anadhanimiwa na kampuni ya vifaa vya michezo ya Adidas.

Oscar mwenye umri wa miaka 28, alihamia China katika Klabu ya Shanghai SIPG mwaka 2017 baada ya kuahidiwa kiasi kikubwa cha fedha. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil aliamua kuachana na Klabu ya Chelsea ya Ligi Kuu ya England na kuondoka Ulaya na kwenda barani Asia.

### 9. MESUT OZIL (ARSENAL)

Mkataba wake wa sasa wa miaka mitatu una thamani ya dola milioni 24 kwa msimu (2018-2022), huku matangazo binafsi akiingiza dola milioni sita na hivyo jumla yake kumfanya aiingize kiasi cha milioni 30 na anadhaminiwa na kampuni za Mercedes Benz, Adidas na Beats by Dre.

Ozil alitajwa kuwa mchezaji anayelipwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya England baada ya kusaini mkataba kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2018, akiwa chini ya kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger. Mchezaji huyo raia wa Ujerumani hayupo kwenye mipango ya kocha Unai Emery na bado uvumi unazagaa anahusishwa na mpango wa kuondoka pale London Kaskazini.

### 8. KYLIAN MBAPPE (PARIS SAINT-GERMAIN)

Mkataba wake wa sasa wa miaka mitatu una thamani ya dola milioni 20 kwa msimu (2018-2021), huku matangazo binafsi akijiingizia kiasi cha dola milioni 10 na hiyo inamfanya apate jumla ya dola milioni 30 na anadhaminiwa na Kampuni za Nike na Hublot.

Katika umri wake wa miaka 20, Mbappe amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa wachezaji bora duniani. Tangu alipojiunga na Paris Saint-Germain kwa ada iliyoweka rekodi mwaka 2017, Mfaransa huyo amekuwa mmoja wachezaji muhimu zaidi kwa klabu yake na timu ya taifa.

### 7. ALEXIS SANCHEZ (MANCHESTER UNITED, INTER MILAN)

Kwa sasa anacheza kwa mkopo katika Klabu ya Inter Milan akitokea kule Manchester United na mkataba wake wa sasa wa miaka minne unamfanya aiingize kiasi cha dola milioni 21 kwa msimu (2018-2022), huku matangazo binafsi yakimuingizia dola milioni tisa na hivyo inamfanya apate jumla ya dola milioni 30 na anadhaminiwa na Kampuni za Nike, Pepsi na Huawei.

Alexis Sanchez alishindwa kung'ara pale Man United tangu alipojiunga akitokea Arsenal na hivyo mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile akalazimika kutolewa kwa mkopo kwenda Inter ya Italia.

### 6. ANDRES INIESTA (VISSEL KOBE)

Mkataba wake wa sasa wa miaka mitatu una thamani ya dola milioni 30 kwa msimu (2018-2021), huku matangazo binafsi akiingiza dola milioni mbili na jumla yake kumfanya atie mfukoni dola milioni 32 na anadhaminiwa na Kampuni za Nike, Sony, Arcos, Nissan na UFX.

Baada ya kucheza kwa miaka 22, akiwa pale Barcelona, Andres Iniesta aliondoka hapo kwenye viunga vya Catalunya kipindi cha majira ya joto mwaka 2018 na kwenda Vissel Kobe ya Japan.

### 5. PAUL POGBA (MANCHESTER UNITED)

Mkataba wake wa sasa wa miaka mitano una thamani ya dola milioni 20 kwa msimu (2016-2021), huku matangazo binafsi yakimuingizia kiasi cha dola milioni 13 na hivyo kumfanya achukue nyumbani jumla ya dola milioni 33 na anadhaminiwa na Kampuni ya Adidas.

Pogba alirudi pale Man United kutoka Juventus kipindi cha majira ya joto mwaka 2016 kwa ada ya pauni milioni 89 akiweka rekodi kwa mwaka huo.

### 4. GARETH BALE (REAL MADRID)

Mkataba wake wa sasa wa miaka mitano thamani yake ni dola milioni 28 kwa msimu (2016-2022), huku matangazo binafsi yakimuingizia kiasi cha dola milioni sita na hivyo kumfanya aingize jumla ya dola milioni 35. Na anadhaminiwa na Kampuni za Adidas, Nissan Motors, Konami na Foot Locker.

Licha ya Bale mahusiano yake ya sasa na Kocha wa Real Madrid, Zinadine Zidane kutokuwa mazuri, lakini alikuwa na mchango mkubwa mno wakati klabu hiyo ikitamba kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### 3. NEYMAR JR (PARIS SAINT-GERMAIN)

Mkataba wake wa sasa wa miaka mitano una thamani ya dola milioni 70 kwa msimu (2017-2022), huku matangazo binafsi yakimuingizia dola milioni 35 na jumla yake inamfanya atie mfukoni jumla ya dola milioni 109. Anadhaminiwa na Kampuni za Gillette, McDonald's, Beats by Dre, Apple Inc. (AAPL) na Nike.

Uhamisho wa Neymar kwenda Paris Saint-Germain kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2017 ulimfanya kuweka rekodi ya pauni milioni 222 akitokea kule Barcelona.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 27, amekuwa mchezaji muhimu zaidi wa klabu yake na nchini yake na ni wa pili kwa kuwa na wafuasi wengi zaidi kwenye mtandao wa kijamii wa Instagram akizidiwa na Cristiano Ronaldo.

### 2. CRISTIANO RONALDO (JUVENTUS)

Mkataba wake wa sasa wa miaka minne una thamani ya dola milioni 70 kwa msimu (2018-2022), huku matangazo binafsi yakimuingizia kiasi cha dola milioni 45 na hivyo inamfanya aingine kiasi cha dola milioni 109. Anadhaminiwa na kampuni za Nike, Altice, DAZN, MTG na Herbalife.

Ronaldo alihamia kwenda Juventus kipindi cha majira ya joto mwaka 2019, baada ya kubeba mara tatu mfululizo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Yeye ndiye mwanamichezo mwenye wafuasi wengi zaidi duniani kwenye mtandao wa kijamii wa Instagram, akiwa na wafuatiliaji wake zaidi ya milioni 190. Ronaldo pia alikuwa mchezaji wa pili kwenye historia ya soka duniani kufunga mabao 100 kwa timu yake ya taifa.

### 1. LIONEL MESSI (BARCELONA)

Mkataba wake wa sasa wa miaka minne unathamani ya dola milioni 80 kwa msimu (2017-2021), huku matangazo binafsi yakimuingizia kiasi cha dola milioni 47 na hivyo jumla yake kubeba dola milioni 127 anazoziingiza kwa mwaka. Anadhaminiwa na Kampuni za Adidas, Pepsi, Lays, Gatorade, Jacobs & Co, Mastercard na Ooredoo.

Anatajwa kama ndiye mchezaji bora zaidi wa wakati wote kwa mchezo wa mpira wa miguu na Messi tangu utoto wake amecheza hapo Barcelona kwenye viunga vya Catalunya.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 kwa sasa ndiye mwanasoka anayeingiza mkwanja mrefu zaidi kuliko yeyote duniani.

## Nukuu

"Linapokuja suala la maendeleo, kwa uhakika kabisa kuna mataifa yako mbele yetu kwa ubora. England, Hispania, Ufaransa, Italia na Ubelgiji – hizi ni timu ambazo naziona kabisa kwamba zipo mbele yetu kwa ubora, michuano iliyopita kwa mfano, England walifanya maajabu makubwa kwenye Kombe la Dunia na bado wana nafasi kubwa kwenye michuano hii ya Euro," **Kocha wa Ujerumani Joachim Low akikitoa kikosi chake katika nafasi ya kubeba taji Euro 2020.**



"Hakuna haja kwa Arsenal kupaniki, ingawa hatupo kwenye msimu mzuri kwa sababu mbalimbali, lakini ili kuwa juu ni lazima kuhakikisha kwamba unachukua makocha makini kama [Mauricio] Pochettino. Ninamuelewa mno Pochettino na naamini akitua pale Arsenal anaweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi chetu," **beki wa zamani wa Arsenal, Martin Keown.**



"Nimeshitushwa mno kwa uamuzi wa Tottenham, ni upuuzi kufikiri [Mauricio] Pochettino amepoteza uwezo wake haraka. Aliiongoza Tottenham kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Juni Mosi. Klabu nyingine zingefikia hatua hii, zingemjengea sanamu ya heshima kocha kwa mafanikio makubwa aliyofika kwenye soka," **mshambuliaji wa zamani wa Tottenham, Peter Crouch**



## Michezo




Winga wa Simba, Miraji Athumani, aliyefunga mabao mawili Jumamosi iliyopita dhidi ya Ruvu Shooting. **PICHA: MAKTABA.**

# MSHIKEMSHIKE WA LIGI KUU KATIKA NAMBA

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara imerejea tena na kufikia patamu. Iko kwenye raundi ya 12, na ilisimama kwa wiki moja kupisha mechi za kimataifa ambazo ziko kwenye Kalenda ya Fifa.

**Matokeo ya mechi za raundi ya 12 yanaonyesha kuwa ligi ya msimu huu imeendelea kuwa ngumu na isiyotabirika kila mechi zinavyozidi kuendelea kuchezwa. Hakuna timu yenye uhakika na ushindi. Hata zile timu zinazoitwa au kujiita kubwa nazo zinapata ugumu wa kushinda.**

Ligi ya msimu huu hakuna timu yenye uhakika hata wa kushinda kwenye uwanja wake wa nyumbani. Timu zinafungwa nyumbani na zinakwenda kushinda ugenini.

Mpaka kufikia raundi hiyo, timu na wachezaji wao wameweka rekodi mbalimbali tamu na chungu.

Mwandishi wa makala haya amekusanya rekodi hizo pamoja na takwimu za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mtindo wa namba, zisome hapa...

**208 -** Ni idadi ya mabao yaliyofungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi sasa wakati ikiwa imefikia raundi ya 11.

**106 -** Hizi ni idadi za mechi zilizochezwa kwenye Ligi Kuu mpaka sasa kufikia raundi ya 11, zingine zikifikisha raundi hiyo, huku kuna baadhi ya timu zikiwa hazijafikia idadi ya mechi 11.

**74-** Namba hii inasimama kama idadi ya mechi za kushinda kwenye Ligi Kuu. Timu zote zilizoshinda kwenye ligi mpaka sasa ukijumlisha idadi ya mechi zao za kushinda unapata idadi hii, zikiongozwa na Simba iliyoshinda mechi saba ikiwa ni nyingi zaidi kuliko timu zingine.

**32-** Ni idadi ya mechi zote za sare kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ukizijumlisha, huku Prisons ikiwa ndiyo kinara wao, ikiwa imetoa sare saba na kuzishinda timu zote kwa wingi huo.

**31-** Uwanja unaotumiwa kama uwanja wa nyumbani na timu za jijini Dar es Salaam umeruhusu mabao mengi zaidi ya viwanja vyote vya Ligi Kuu, ukiwa umeruhusu idadi hiyo ya mabao.

**24-** Uwanja wa Samora mjini Iringa unaotumiwa na Lipuli FC kama wake wa nyumbani umeruhusu idadi hiyo ya mabao, ikiwa inashika nafasi ya pili nyuma ya Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**17-** Hizi ni pointi za Kagera Sugar ilizozivuna ikicheza ugenini, ikiwa ndiyo timu inayoongoza kwa kuvuna pointi nyingi ikiwa nje ya kwao. Imecheza mechi saba ugenini, ikishinda tano, sare mbili na haijapoteza mechi yoyote ugenini.

**16-** Namba hii ni pointi za Namungo FC ilizozipata ikicheza nyumbani kwenye Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi, ikiwa inakamata nafasi ya pili kwa timu zilizopata pointi nyingi zikicheza nyumbani, zikiongozwa na Lipuli FC ambayo imejikusanyia pointi 17 ikicheza nyumbani, Uwanja wa Samora Iringa.

**12-** Ni idadi ya mabao ya kufunga ya Simba na Kagera Sugar kila moja zikiwa ugenini na kuwa timu zinazoongoza kwa kucheka na nyavu mara nyingi zaidi ikicheza nje ya uwanja wake wa nyumbani.

**10-** Ni idadi ya pointi za Simba ilizokusanya ikicheza kwenye uwanja wake wa nyumbani ambao ni Taifa na Uhuru.

**8-** Penalti za idadi hii ndizo zilizopatikana kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, huku Mbao FC ikiongoza kwa kupata penalti nyingi zaidi kuliko timu yoyote. Mbao imezawadiwa penalti tatu mpaka sasa, Simba ikifuatiwa ikiwa na penalti mbili. Zingine ni KMC, Mbeya City, na Kagera Sugar.

**7-** Ni idadi ya mabao na pointi za Yanga ilizozipata ikicheza kwenye uwanja wake wa nyumbani.

Yanga imefunga mabao saba ikicheza nyumbani, pia kukusanya pointi saba ikicheza nyumbani.

**6-** Hii ni idadi ya penalti zilizotinga wavuni mpaka sasa, Simba ikiongoza kwa kupachika penalti mbili zote zikiwekwa na Meddie Kagere kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar, ikishinda mabao 3-0 na dhidi ya Mbeya City, ikishinda mabao 4-0. Zingine zilizopata penalti zao ni KMC, Mbeya City, Kagera Sugar na Mbao FC ambayo ilipata moja na kukosa mbili.

**5-** Wachezaji waliojifunga wenyewe kwenye Ligi Kuu ni watano ambao ni Ibrahim Said wa Mbao FC kwenye mechi dhidi ya Alliance FC na kutoka sare ya bao 1-1, George Chota wa Mbeya City aliutumbukiza mpira katika nyavu zake kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1.

Mwingine ni Yassin Mustapha wa Polisi Tanzania aliyejifunga kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting na kusababisha timu yake kufungwa bao 1-0, huku Dickson Daudi akijifunga kwenye mechi kati ya timu yake ya Mtibwa Sugar dhidi ya Coastal Union, timu yake ikishinda mabao 2-1. Wa tano ni Mtenje Juma wa Coastal Union aliyejifunga kwenye mechi hiyo hiyo dhidi ya Mtibwa Sugar na kufanya timu yake kupoteza kwa mabao 2-1.

**2-** Hat-trick kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ziko mbili mpaka sasa, moja ikipigwa na Ditram Nchimbi kwenye mechi kati ya timu yake ya Polisi Tanzania dhidi ya Yanga, zikitoka sare ya mabao 3-3, na nyingine ni ya straika wa Lipuli, Daruwesh Saliboko aliyeipatia timu yake ikiisulubu Singida United mabao 5-1.

**1-** Ni idadi ya mabao yaliyofungwa kwenye viwanja vitatu vya Taifa jijini Dar es Salaam, Namfua Singida na CCM Shabib Gairo. Ndivyo viwanja vilivyoruhusu idadi ndogo zaidi ya mabao. Bao pekee la Uwanja wa Taifa lilifungwa na Meddie Kagere wa Simba kwenye mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Azam, ikishinda bao 1-0. Ndiyo mechi pekee ya Ligi Kuu iliyochezwa kwenye uwanja huo mpaka sasa. Gairo, mechi pekee iliyochezwa ni kati ya Mtibwa Sugar ikitumia kwa sasa kama uwanja wa nyumbani dhidi ya Mwadui na kushinda bao 1-0. Bao pekee kwenye Uwanja wa Namfua lilifungwa kwenye mechi kati ya timu mwenyeji Singida United dhidi ya Alliance, tena wageni wakishinda bao 1-0.

**0-** Namungo FC ndiyo timu pekee kwenye Ligi Kuu haijaambulia hata pointi moja ikicheza ugenini.

Timu hiyo yenye pointi 16 zote imezipatia nyumbani, Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi, lakini haijapata pointi yoyote nje ya hapo.

Kati ya mechi 11 ilizocheza, nne imecheza ugenini na kupoteza zote. Namba hii pia inasimama kwa Prisons kuwa ndiyo timu pekee ambayo haijapoteza mechi yoyote ya Ligi Kuu mpaka sasa.

**NAJUA WAJUA**



ARSENAL haijawahi kupoteza katika mechi 25 zilizopita ikiwa nyumbani dhidi ya Southampton (imeshinda 18, sare 7) tangu ilipopoteza kwa bao 1-0 dhidi yao Novemba 1987. Aidha, Southampton imecheza mechi nyingi za ugenini kwenye Ligi Kuu dhidi ya Arsenal bila kushinda kuliko timu nyingine katika historia ya ligi hiyo.

## SOKA



Van Djik (kushoto) na Matip (kulia) wakiwa kazini.

# PACHA 3 BORA ZA MABEKI WA KATI MSIMU HUU

**LONDON,** England

INGAWA wachezaji wanaocheza nafasi ya ushambuliaji wanachukua nafasi kubwa zaidi ya kutamkwa kwenye soka, lakini timu bingwa inajengwa na uti wa mgongo kwa kuwa na ukuta wa mabeki 'pacha' wawili wa kati. Hawa ni namba tano na namba 4.

**Kila timu inahitaji walinzi wa kati ambao wanafanya kazi ya kusaidiana kwa pamoja.**

Pea ya walinzi wa kati kwenye soka la kisasa wanaonekana kama ndio nguzo muhimu zaidi kwa timu.

Msimu huu pia, soka la dunia limeshuhudia pea ya walinzi wa kati wenye kiwango cha juu zaidi, lakini makala haya yanakuchambulia pea tatu za walinzi bora wa kati kwa sasa duniani.

### 3. KALIDOU KOULIBALY NA KOSTAS MANOLAS (NAPOLI)

Kalidou Koulibaly amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi akiwa na Napoli kwa kipindi cha misimu kadhaa sasa. Raia huyo wa Senegal amekuwa kwenye ubora wa hali ya juu na mafanikio makubwa kwenye nafasi yake ya ulinzi wa kati. Klabu kadhaa za Ulaya zimekuwa zikiwania saini yake kwa muda mrefu.

Kipindi cha majira ya joto, Carlo Ancelotti alimnunua Kostas Manolas kuwa patina na Msenegal huyo kwenye moyo wa ulinzi wa klabu hiyo na kwa uhakika wamekuwa na upatina mzuri zaidi pale Napoli.

Beki huyo raia wa Ugiriki amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia tangu atue hapo kwenye Uwanja wa San Paolo. Kama ilivyo kwa Koulibaly, Manolas ni mtu makini zaidi kwenye safu ya ulinzi ya timu hiyo.

### 2. STEFAN SAVIC NA JOSE GIMENEZ (ATLETICO MADRID)

Pea hii ya walinzi wa kati wa Atletico Madrid imekuwa pamoja baada ya kuondoka kwa gwiji Diego Godin kipindi cha majira ya joto kilichopita. Wawili hao wamekuwa na upatina mzuri zaidi kwa staili yao ya uchezaji, na wamekuwa uti wa mgono wa klabu hiyo hadi sasa.

Stefan Savic anaonekana kuwa mlinzi mtundu zaidi ya Diego Godin. Raia huyo wa Montenegro ni imara kwa mipira ya juu na anakuwa makini zaidi anapocheza mipira ya nyuma. Ana uwezo wa kucheza na mpira kutoka nyuma na kusambaza kwenye winga zote mbili na ni kiongozi mzuri zaidi.

Upatina wao mzuri umeisaidia Atletico Madrid kuwa moja ya timu yenye beki bora zaidi msimu huu.

### 1. VIRGIL VAN DIJK AND JOEL MATIP (LIVERPOOL)

Uwezo wa Virgil van Dijk unajulikana na wapenzi wengi wa soka kwa namna alivyokuwa na mafanikio makubwa pale Liverpool.

Raia huyu wa Uholanzi alitokea kwenye akademi ya vijana pale Willem II na baadaye akaibukia Southampton na kutambulisha uwezo wake mwenyewe.

Mwanzo wa msimu wa 2018, Jurgen Klopp alimnunua na kutua pale Liverpool kwa ada iliyoweka rekodi ya kuwa beki bora.

Pale kwenye dimba la Anfield, Mholanzi huyo amekuwa na upatina mzuri kwenye ulinzi wa kati na Joel Matip.

Matip raia wa Cameroon ameonekana kucheza kwa kiwango cha kuvutia zaidi akiwa na upatina na Virgil.

Matip alijiunga na Liverpool kutoka Schalke 04 kipindi cha majira ya joto mwaka 2016 na amekuwa kwenye kiwango bora chini ya Jurgen Klopp. Uwapo wake umemsaidia Van Dijk kuimarisha safu yote ya ulinzi ya timu hiyo.


Raia huyo wa Cameroon, pia amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi ndani ya timu hiyo na kwa namna yoyote wana nafasi ya kuendelea kuwa na upatina mzuri zaidi kwa siku za usoni.

TANGU kuanza kwa msimu uliopita, Liverpool imefunga mabao 38 yaliyotokana na 'mpira wa kutenga' (faulo, kona na penalti) kwenye Ligi Kuu, ambayo ni nane zaidi ya yaliyofungwa na klabu nyingine yoyote kwenye ligi hiyo.



NDANI YA 18

Nipashe
Spotika




MPIRA wa miguu ndio mchezo unaojulikana zaidi na ukweli kwamba fedha nyingi zinahusishwa, angalau kwa kusema hivyo. Wachezaji kama Lionel Messi na Cristiano Ronaldo bila shaka yoyote ndio wachezaji wanaolipwa kiasi kikubwa...

Uk. 16&17

# KLABU 3 ANAZOWEZA KUTUA POCHETTINO



**LONDON,** England

BAADA ya kuiongoza timu hadi nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, Tottenham Hotspur ikaamua kuachana na Mauricio Pochettino, na kumaliza kipindi chake cha miaka mitano na raia huyo wa Argentina.

**Tangu achukue mikoba, Pochettino alikuwa na falsafa ya aina yake kwa kuwafanya miamba hao wa London Kaskazini kuwapo tena kwenye ramani ya soka kwa kuwawezesha kubanana kwenye nne bora na kutoa ushindani katika mashindano makubwa.**

Baada ya mfululizo wa matokeo mabaya, kwa ligi ya nyumbani na michuano ya Ulaya, Spurs wakaamua kuachana na kocha huyo wa zamani wa Southampton na kuamua kumchagua Jose Mourinho, ambaye amerudi hapo baada ya kufukuzwa kule Manchester United.

Pochettino alitengeneza jina lake na kuwa mmoja wa makocha wanaotajwa zaidi duniani.

Licha ya kufukuzwa, klabu kadhaa zimekuwa zikitajwa kuwania saini yake, makala haya yanachambua timu tatu ambazo zinaweza kumchukua Pochettino, tiririka nayo...

### 3. MANCHESTER UNITED

Pochettino alikuwa mmoja wa makocha waliopewa nafasi kubwa zaidi ya kutua pale Manchester United baada ya kufukuzwa kwa Mourinho mwaka jana, lakini kimaajabu 'Special One' huyo amechukua mikoba ya raia huyo wa Argentina pale Tottenham Hotspur.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 48 amekuwa akitajwa pia kwamba, anafikiria kuchukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer, kwani matokeo mabaya ya kikosi hicho yanamfanya kuwa kwenye uwezekano kwa raia huyo wa Norway kufukuzwa na nafasi yake kupewa Pochettino. Mashabiki wa 'Mashetani Wekundu' hao wanaonekana kutokuwa na imani kubwa na kocha wao wa sasa.

Tangu kuteuliwa kwake, United imeshindwa kuwa kwenye kiwango chake na wamepitwa pointi 21 na vinara Liverpool kabla ya mechi yao ya jana na pia umekuwa mwanzo wao mbaya zaidi kwenye Ligi Kuu na hivyo kumweka kwenye wakati mgumu Solskjaer.

Kama 'Mashetani Wekundu' hao wakiamua kuachana na raia huyo wa Norway, Pochettino anatarajwa kuwa chaguo la kwanza na anaonekana kuwa na uwezo wa angalau kurudisha mafanikio ya Man United tangu kuondoka kwa Sir Alex Ferguson.

### 2. REAL MADRID

Msimu wa 2018/19 kiukweli kabisa ulikuwa ndio mbaya zaidi kwa Real Madrid. 'Los Blancos' hao walianza msimu na Julen Lopetegui, lakini raia huyo wa Hispania alitemwa na nafasi yake ikachukuliwa na Santiago Solari, ambaye alifukuzwa baada ya kuwa na matokeo mabaya.

Kabla ya Zinadine Zidane kurudi kwa mara ya pili pale kwenye dimba la Santiago Bernebeu, Pochettino aliripotiwa kwamba ndiye aliyekuwa akiwaniwa zaidi na Rais Florentino Perez kwamba ndiye angekuwa kocha wa muda mrefu wa kukijenga kikosi hicho.

Real Madrid wamekuwa na upepo mzuri sasa chini ya Zidane na ingawa bado mambo hayajakuwa sawa kwa asilimia 100, Pochettino bado anaweza kuwa chaguo sahihi la kuweza kuchukua mikoba ya Mfaransa huyo.

### 1. BAYERN MUNICH

Bayern Munich kwa sasa ndio inayoongoza kwenye mbio za kuwania saini ya Pochettino, baada ya kuachana na Niko Kovac kwa matokeo mabaya na kuwafanya Bavaria wakivutwa hadi nje ya nne bora kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Kocha Msaidizi, Hansi Flick amepewa mikoba ya kuchukua nafasi ya Mjerumani huyo na ameonekana kuanza vizuri kwa kupata ushindi dhidi ya Olympiakos kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Borussia Dortmund kwenye Ligi Kuu.

Mabingwa hao wenye rekodi ya aina yake kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, awali waliripotiwa kwamba wanamuangalia kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger. Lakini Mfaransa huyo alichaguliwa kuwa mkuu wa maendeleo ya mpira wa miguu duniani na Shirikisho la Soka la Kimataifa, Fifa.

Tangu kufukuzwa kwa Pochettino pale Spurs, kumekuwa na uvumi kwamba raia huyo wa Argentina ndiye anakwenda kuwa mrithi wa Kovac na tayari pande zote mbili zimeshakutana.

Majina kama Erik ten Hag na Ralf Rangnick pia yalikuwa yakihusishwa na kazi hiyo katika wiki za hivi karibuni, lakini Bayern ni wazi kwamba itakuwa na nia ya kumchukua Pochettino mwenye umri wa miaka 48 kwa ajili ya kuimarisha kikosi hicho.

**USILOLIJUA**

CHELSEA imefunga mabao mengi zaidi kwenye mechi za ugenini za Ligi Kuu msimu huu (mabao 19) na hakuna timu iliyoruhusu mabao mengi ugenini kama 'Blues' msimu huu wa 2019-20 (mabao 14).





# Vyuo vya ufundi vya dini vyalia VAT

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

UENDESHAJI wa vyuo vya ufundi vinavyomilikiwa na Taasisi za dini nchini umetajwa kuwa mgumu kwa sasa kutokana na ongezeko la gharama za uendeshaji baada ya Serikali kuziondolea msamaha wa kodi taasisi hizo ikiwamo ya ongezeko la thamani (VAT).

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Chuo cha Ufundi Satadi cha Moraviani kilichopo eneo la Kadege jijini Mbeya, Gadi Lwinga, wakati wa hafla ya kuwatunuku vyeti wahitimu wa fani mbalimbali za ufundi chuoni hapo zikiwamo fani za ufundi umeme na magari.

Alisema kutokana na ongezeko la kodi hizo, wanashindwa kupata vifaa vya kisasa vya kuwafundishia wanafunzi mambo ya ufundi, hivyo kupungua kwa ufanisi wa ufundishaji.

"Hata vitu tunavyotengeneza tukiviuza lazima viwe na Vat ambayo huwa inasababisha bei kuonekana kuwa kubwa, hivyo kuwalazimu wateja wetu kukimbilia mitaani ambako hakuna kupeana risiti," alisema Lwinga. Alisema baadhi ya vifaa ambavyo vina gharama kubwa kutokana na ongezeko la kodi hizo ni vya kushonea nguo kama cherehani na vifaa vya kufundishia uchapaji ambavyo awali walikuwa wanavipata bila kodi.

Alisema kutokana na ongezeko hilo la gharama za uendeshaji wa chuo, hata idadi ya wanafunzi imepungua, hivyo kukifanya chuo hicho kuwa na wakati mgumu zaidi.

Vilevile, alisema chuo hicho kinakabiliwa na tatizo la upungufu wa fedha kwa ajili ya kuboreshea miundombinu yake kutokana na ongezeko la ada kwenye shughuli za mafunzo na uzalishaji.

Aidha, alisema kwa mwaka huu, wanafunzi waliohitimu walikuwa 191 ambao ni wa fani tofauti zikiwamo za muda mrefu na muda mfupi.

Akizungumza kwa niaba ya Askofu Mkuu wa Kanisa la Moraviani Jimbo la Kusini Magharibi, Mchungaji Zacharia Sichone aliwataka vijana waliohitimu mafunzo hayo kwenda kuzitumia fani zao kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa.

Alisema endapo watazitumia vema fani hizo, kuna uwezekano zikawasaidia kuboresha maisha yao binafsi na hata kusaidia katika kuchangia pato la taifa kwa kuanzisha kampuni za ufundi ambazo zitakuwa zinalipa kodi.

"Mimi siamini sana katika kazi za kuajiriwa na badala yake naamini katika kujiajiri kutokana na maarifa na ujuzi wako mwenyewe, sasa nawataka kila mmoja awe na wazo la kwenda kuzalisha ajira badala ya kusubiri kuajiriwa," alisema Mchungaji Schone.

Alisema kitendo cha vijana hao kukutana kwa pamoja chuoni hapo kinawasaidia kupanua mawazo yao kutokana na kila mmoja kuwa na uelewa wake. Nao baadhi ya vijana hao waliuomba uongozi wa chuo hicho kupanua maktaba ya chuo ikiwamo kuongeza vitabu ili kila fani iwe na vitabu vya kutosha.




Baadhi ya wajasiriamali wa Jiji la Mbeya wakiendelea kuuza matunda huku wakiwa wameyapanga chini katika eneo la Kabwe barabara ya kuelekea Uwanja wa Ndege wa zamani juzi, eneo ambalo walizuiliwa na uongozi wa Jiji kwa madai halikutengwa kwa shughuli hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mkandarasi wa barabara awakera Mbalizi

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

BAADHI ya wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, wameiomba Serikali kumshinikiza mkandarasi aliyekuwa anapanua barabara kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam), kurekebisha mitaro ili kuepusha madhara ya maji ya mvua ambayo yameanza kujitokeza.

Wanadai kuwa mkandarasi huyo alifukia mitaro ya maji wakati anajenga barabara hiyo na mpaka sasa hajaitengeneza hali ambayo inasababisha maji kujaa barabarani hasa kipindi hiki ambacho mvua imeanza kunyesha.

Mwenyekiti wa Stendi ya mabasi ya Mbalizi, Ezekia Mwanyanya, alisema maji yanaingia mpaka kwenye makazi ya watu na endapo mitaro hiyo haitatengenezwa haraka maji yanaweza yakasababisha madhara zaidi.

Alisema baadhi ya maeneo watu wameanza kufunga biashara zao kukwepa athari za maji hayo ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakiwatesa.

"Sisi tunalalamika miaka yote tukiiomba Serikali imalizie stendi yetu, sasa limeibuka tatizo hili la maji linalotokana na mitaro hii kutojengwa, maji yaliyokuwa yaelekee mtoni sasa yanarudi yanaingia mpaka stendi na tunashindwa kufanya kazi zetu vizuri," alisema Mwanyanya.

Naye Izrael Songa, fundi seremala, alisema mvua ikinyesha maji yanasambaa barabara nzima, hivyo kuanza kuleta madhara hata kwenye barabara yenyewe kwa kuchimbua baadhi ya maeneo.

Alisema mvua ikiisha barabara inajaa takataka ambazo zinazolewa kutoka maeneo mbalimbali na zingine ni hatari kwa maisha ya watu ambao wanaitumia barabara hiyo pamoja na vyombo vya moto.

Aliiomba Serikali iharakishe kuboresha mitaro hiyo kabla mvua haijawa nyingi ili kupunguza madhara hayo ambayo yanaweza kuwakuta wananchi hao.

# Tari yapata Baraza la wafanyakazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (Tari) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imezindua Baraza la Wafanyakazi ambalo litatumika kama chombo cha kuwashirikisha wafanyakazi wote kufanya uamuzi pamoja na kuwasilisha mawazo yao kwenye ngazi za juu kwa mujibu wa sheria.

Baraza hilo limeanzishwa kwa mara ya kwanza tangu taasisi hiyo ilipoanzishwa bila kuwapo chombo rasmi cha kuwashirikisha wafanyakazi kufanya uamuzi na taasisi hiyo na kuwasilisha mawazo yao ngazi za juu za Serikali.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa baraza hilo Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema kabla ya kuundwa kwa chombo hicho vilikuwa vinafanyika vikao vya utawala ambavyo ndivyo vilikuwa vinafanya uamuzi.

Alisema vikao hivyo ndivyo vilikuwa vinafanya kazi, lakini mawazo ya wafanyakazi hayakuwa yakiwasilishwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria za nchi, na kwamba anaamini kuundwa kwa baraza hilo kutasaidia kuboresha utendaji kazi wa taasisi.

"Uwakilishi wa wafanyakazi ulikuwa ni kwa kiasi kidogo sana, lakini sasa hili baraza litakuwa linakaa vikao mara mbili kwa mwaka na kuwasilisha mawazo ya wafanyakazi na hii itatusaidia kuifanya taasisi kuwa shirikishi zaidi," alisema Dk. Bucheyeki.

Katibu wa Chama cha Wafanyakazi Wanataaluma na Watafiti (Raawu), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Thomas Kasombwe, alisema kazi kubwa ya baraza la wafanyakazi ni kuwashirikisha wafanyakazi kuhusu mambo yanayofanywa na taasisi yao.

Vile vile, alisema baraza linatakiwa kufanya kazi ya kupitisha mambo yao kwenda makao makuu ya ili yapatiwe ufumbuzi na utendaji wa taasisi uwe bora zaidi.

Alisema uundwaji wa mabaraza ya wafanyakazi ni agizo la Rais wa kwanza, Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1970 ambapo aliagiza mahali popote penye mkusanyiko wa wafanyakazi kiundwe chombo cha kuwasemea.

"Agizo namba moja la Rais wa kwanza ilikuwa ndio hili la uundwaji wa mabaraza ya wafanyakazi na alifanya hivyo ili kuwarahisishia wafanyakazi uwasilishaji wa masuala yao katika ngazi za juu, hivyo hili baraza ni zuri na litatusaidia," alisema Kasombwe.

Nao baadhi ya wafanyakazi wa Tari Uyole walisema wanaamini baraza hilo litawaletea tija katika utendaji wa taasisi hiyo ikiwamo kuboresha utendaji wa wafanyakazi.

Mmoja wa wafanyakazi hao, Pricila Mbwaga, alisema kwa mujibu wa maelezo waliyoyapata, baraza hilo litakuwa ndio chombo chao cha kujadili masuala yanayohusu utendaji kazi wao ndani ya taasisi.

Alisema chombo hicho kitasaidia pia kupatikana kwa teknolojia bora za kilimo kutokana na wafanyakazi kuwa na uwanja mpana wa kujadiliana kabla ya kupitisha jambo lolote.



# Kamishna wa Maadili Kenya atoa somo klabu za Tanzania

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

KAMISHNA wa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi nchini Kenya, Rose Macharia, amezitaka klabu za wanachama wa tume ya maadili nchini kukuza maadili kwa jamii inayowazunguka ili kuwa na uzalendo.

Macharia alitoa kauli hiyo alipokuwa akizungumza na wanachama wa klabu hizo kwenye ziara yake katika shule ya sekondari Dodoma.

Aliwataka kukuza na kuheshimu misingi ya maadili, ili kujenga heshima kwa jamii.

Alisema kuwa ujio wao ni sehemu ya kujifunza na kuona jinsi vilabu vinavyoweza kukuza maadili kutoka kwa sekretarieti ya maadili viongozi wa umma jinsi wanavyoweza kusimamia utendaji wao hapa nchini.

Alihimiza klabu hizo kutoa elimu kwa vijana wenzao ili wawe na uzalendo wa kuilinda na kuipenda nchi yao.

Alibainisha kuwa hatua hiyo itasaidia kukemea vitendo vya rushwa na ufisadi vinavyofanywa na baadhi ya viongozi wasiokuwa waaminifu..

Awali, akisoma risala ya wanachama wa klabu ya maadili katika shule hiyo, Mwalilei Manase, alisema kuwa kwa kupitia klabu yao wamekuwa wakitoa elimu ya uhamasishaji na kufanya kampeni kwa vijana wenzao ili kuhakikisha maadili yanakuwapo na kuheshimiwa. "Pia tumetoa elimu kwa taasisi mbalimbali lengo likiwa ni kupanua wigo mpana ili elimu hii iwafikie vijana wenzetu ambao ni wasomi kwa ajili ya kuwaanda kwenye nafasi za uongozi," alisema.

Naye, Makamu mwalimu mkuu wa shule hiyo Ester Simchimba, alisema ujio wa tume hiyo kutoka nchini Kenya itasaidia wananchama hao kuwa viongozi wenye maadili mema kwa Taifa na jamii watakayowatumikia .

Kaimu Katibu Msaidizi Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa umma, Ofisi ya Kanda ya Kati, Dodoma Jasmin Awadhi, alisema ujio huo watume hiyo ya Kenya utapunguza utoro na kuwapo kwa nidhamu kwa wanafunzi.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Anthony Mavunde (kulia) akimtunuku Meneja wa NMB Tawi la Dodoma, Harold Lambileki Shahada ya Uzamili katika menejimenti ya biashara ya Kimataifa katika mahafali ya 45 ya Chuo cha Biashara (CBE) Dodoma yaliyofanyika mwisho wa wiki Jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Maeneo hatarishi maambukizo mapya VVU haya

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, ametaja maeneo ya uchimbaji madini na mialo ya wavuvi kuwa ni hatarishi kwa maambukizo mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya siku ya Ukimwi Duniani, itakayofanyika kitaifa jijini Mwanza, alisema kutokana na hali hiyo kwasasa kuna programu maalum ya kudhibiti maambukizo hayo imeanzishwa kwenye baadhi ya mikoa nchini yenye shughuli hizo. "Kuna mikoa ambayo tunataka kupeleka nguvu zetu za ziada, ni ile yote inayozunguka maeneo ya maziwa kwa mfano Mwanza ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa lengo ni kudhibiti maambukizi mapya kwenye mialo, tunaamini maeneo yanayozunguka maziwa kwasasa ni hatarishi kwa maambukizi mapya na pia maeneo ya migodi," alisema.

Alisema kupitia mfuko wa kudhibiti Ukimwi waliamua kujenga kituo kikubwa cha Afya eneo la Mererani ikiwa ni jitihada za kudhibiti maambukizi hayo.

"Pale Mererani ukichukua maambukizi ya mkoa mzima wa Manyara yapo kidogo ni kama asilimia tatu, wakati Mererani peke yake ni asilimia saba, kwasasa serikali na Tacaids tumejipanga kuhakikisha tunayafikia maeneo hayo na kuweka mipango madhubuti ili Watanzania hasa vijana wasiingie kwenye maambukizi mapya,"alisema.

Kadhalika, alisema serikali imeweka mkazo mkubwa kuelimisha vijana ili kupunguza maambukizi hayo kwa kundi hilo kutokana na kuwa na asilimia 40 ya maambukizi mapya.

Kuhusu maadhimisho hayo, Mhagama alisema katika maadhimisho hayo ambayo yanatarajiwa kuzinduliwa Novemba 25 hadi 30, mwaka huu kutakuwa na maonesho na utoaji wa huduma rafiki kwa vijana yatakayokuwa maalumu kwa ajili yao. Mkurugenzi wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (Tacaids), Dk.Leonard Maboko, alisema kila mwaka maambukizi mapya ya watu 72,000 na vijana wa kati ya miaka 15 hadi 24 wamekuwa wakichangia kwa asilimia 40.

"Hii inamaana maambukizi mapya kwa siku ni watu 200 na vijana 80 kwa siku wanapata maambukizi na mabinti ndio wengi, kwa maana hiyo kati ya vijana 80 wanaopata maambukizi mapya, 64 ni wa kike,"alisema.

## Energy wapata gawio bil. 22/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMPUNI ya Puma Energy Tanzania Limited imetangaza kutoa gawio la Sh. Bilioni 22 kwa mwaka 2018 kwa wanahisa wake.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Dominic Dhanah, hadi kufikia Desemba 31, mwaka 2018, kampuni ilitengeneza faida kabla ya kodi ya kiasi cha Sh. bilioni 25.

"Kampuni iliwekeza takribani Sh. bilioni 16 kwa mwaka 2018 kununua na kuendeleza miundombinu ikiwamo ukamilishwaji wa mfumo wa kujazia mafuta katika jengo namba Tatu (Terminal III) katika Uwanja wa Ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam," alisema.

Pia alisema wamekamilisha ununuzi wa vituo viwili vya mafuta kwenye jiji la Dodoma ikiwa ni kuiunga serikali mkono katika kuhamia Dodoma.

"Wakurugenzi wa kampuni wamependekeza gawio la Sh. Bilioni 22 kwa mwaka ulioishia Desemba 2018, kila mwanahisa atapata Sh. bilioni11," alisema.

Alifafanua kuwa kwa gawio hilo limeongezeka ambapo kwa mwaka 2017 gawio lilikuwa Sh. bilioni 18, mwaka 2016 gawio lilikua Sh.Bilioni 14 na mwaka 2015 gawio lilikuwa Sh.Bilioni 9.

"Kutokana na utendaji mzuri wa kampuni ya Puma Energy, gawio limekua kwa asilimia 57 ikilinganishwa na gawio la mwaka 2016 na kwa asilimia 22 ikilinganishwa na gawio na mwaka 2017," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema ukuaji huu unaendana sambamba na mikakati ya kampuni ya kuhakikisha kampuni inaendelea kukua, kutengeneza faida, kukuza ajira nchini, kuchangia pato la taifa kupitia kodi na kuendelea kuiunga serikali mkono katika kuwaletea Watanzania maendeleo.

"Ufanisi wa kibiashara wa Puma Energy Tanzania kwa mwaka 2018 ulikua mzuri kwa pande zote za mauzo pamoja na mapato na unatokana zaidi na biashara ya mafuta ya ndege ambako kwa sasa sisi ndio tunaongoza katika soko," alisema.

Alieleza kuwa taarifa za masoko zilizochapishwa na Mamlaka ya udhibiti wa Mafuta na Maji (Ewura) inaonesha kuwa uwepo wa Puma Energy kwenye soko la mafuta umeongezeka kutoka asilimia 12 mwaka 2015 hadi asilimia 14 kwa mwaka 2017.

Alipongeza juhudi za serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli na serikali yake katika mikakati yake ya kukusanya kodi, kutoa fursa kwa wawekezaji wa nje na ndani na kuanzisha miradi mikubwa ya kimkakati kama ilivyooneshwa kwenye bajeti ya 2019/20.

"Mikakati hii imewezesha Puma Energy Tanzania kupata kazi ya kuuza mafuta katika mradi wa reli ya kati, mradi wa bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere kule Rufiji, Daraja jipya la Salender na mingine," alisema.

Dhanah alisem miradi hiyo mikubwa inatoa fursa kwa wawekezaji mbalimbali kufanya biashara na kufanya kampuni nyingi ikiwamo Puma kutengeneza faida zaidi.

Alifafanua kuwa kampuni hiyo inamilikiwa kwa pamoja na serikali na Puma Investments Limited ambapo kila moja anamiliki hisa kwa asilimia 50.

Akizungumzia uwezo wa kampuni, alisema kampuni ina uwezo wa kuhifadhi jumla ya lita za mafuta milioni 94 , vituo 52 vya mafuta maeneo mbalimbali nchini na inahudumia viwanja vinane vya ndege.



# Wajasiriamali waililia serikali vifungashio

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAJASIRIAMALI wameiomba Serikali ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutafuta mashine ya vifungashio vya bidhaa ili kupunguza gharama za kuagiza vifungashio nje ya nchi.

Waliyasema hayo katika maonesho ya Juakali ya kusherehekea kutimiza miaka 20 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yanayofanyika katika viwanja vya Fumba.

Walisema ikiwa serikali zitatafuta wataalamu hao na kupata kiwanda cha kuzalishia vifungashio, wataweza kuwasaidia kupunguza gharama za kununua nchi za nje.

Mmoja wa wajasiriamali kutoka Dar es Salam, Brijita Joseph Kailembo, alisema vifungashio wanavyotumia katika kufungia bidhaa zao wamekuwa wakinunua China.

Kailembo alisema imefika wakati kuiga mifano ya nchi nyingine kwa kuwa na viwanda ambavyo vitawawezesha kuinua kipato chao na kuwawezesha kuingia katika soko la dunia.

"Kwanini nchi nyingine zinaweza ikiwamo Kenya ambayo ipo Afrika Mashariki, lakini sisi Tanzania tunashindwa kuwa na viwanda vya aina hiyo," alisema.

Alisema maonyesho hayo yanawasaidia kujuana na kujua mbinu mbalimbali za uzalishaji wa bidhaa zao ambazo zitawawezesha kuingia katika ushindani wa soko la kibiashara.

"Najivunia sana kushiriki katika maonesho haya kwani tunaimarisha muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar ambao unaendelea kutufanya kuwa kitu kimoja na kuendeleza udugu wetu ulioasisiwa na Mwalimu Julius Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume," alisema.

Aidha, aliwaomba wafanyabiashara kushirikiana ili kuwa na viwanda vikubwa ambavyo vitawawezesha wajasiriamali kujikwamua kiuchumi.

Naye mjasiriamali Elia Filbat kutoka Kinyasini Unguja, alisema maonesho hayo yana manufaa makubwa katika kujifunza na kuibua mbinu mbalimbali za kuimarisha bidhaa zao.

Aliwashauri wajasiriamali kujifunza kwa kuzalisha bidhaa zao wenyewe kwa kutumia kilimo hai ikiwamo mboga na kupata faida.

Naibu Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRAD), Latifa Mohammed Khamis, aliwapongeza wajasiriamali kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania kushiriki katika maonyesho hayo ambayo ni fursa ya kumfanya mfanyabiashara kutangaza biashara yake.

Aliwaomba wajasiriamali ambao bado hawajatumia fursa hiyo kushiriki ili kuuza bidhaa zao na kuongeza thamani.



Mratibu Miradi wa shirika lisilo la kiserikali la wanawake Amkeni 'Women Wake Up' (WOWAP),Nasra Suleiman, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mangda kwenye mkutano wa hadhara kuhusu mila potofu na madhara ya ukeketaji kwa mtoto wa kike mwishoni mwa wiki, katika Kata ya Msange, Halmashauri ya Wilaya ya Singida. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**

# Hospitali kisasa magonjwa akili kujengwa

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

HOSPITALI ya Chuo Kikuu cha Haukeland nchini Norway inatarajia kusaidia ujenzi wa hospitali ya wagonjwa wa akili ya Kidongo Chekundu Zanzibar ambayo itakuwa ya kisasa kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Akizungumza na uongozi wa hospitali hiyo, Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alisema hospitali ya wagonjwa wa akili Kidongo Chekundu ni kongwe ambayo ina historia kubwa inayotokana na utoaji huduma zake kwa wakati huo ilipojengwa na wakoloni.

Alisema hatua za kuijenga upya hospitali hiyo na kuwa ya kisasa itakuwa ni faraja kubwa kwa Wazanzibar kwa kuimarisha na kutoa huduma za kisasa za wagonjwa wa akili na kuwa msaada mkubwa kwa wagonjwa wa ndani na nje ya nchi.

Dk. Shein alisema Serikali ya Zanzibar inathamini sana ushirikiano inaoutoa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Hakeland katika kusaidia kuimarisha sekta ya afya Zanzibar ikiwamo kusaidia ujenzi wa majengo kwa ajili ya huduma za afya na tiba, vifaa, wataalamu na mafunzo kwa madaktari wa Zanzibar.

Aidha, aliupongeza uongozi huo kwa kufanya kazi na Wizara ya Afya kupitia Hospitali Kuu ya Rufani ya Mnazi Mmoja kwa miaka kumi sasa, hatua ambayo imeweza kukuza na kuimarisha sekta ya afya nchini na kuendeleza huduma za kijamii na kukuza uchumi wa Zanzibar.

Alisema Serikali yake inaendelea na sera ya kutoa huduma za afya bure, sera ambayo ilisisiwa na Jemedari wa Mapinduzi matukufu ya Januari 12, 1964, Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume na hadi hivi sasa inaendelezwa.

"Juhudi za makusudi zimekuwa zikichukuliwa katika kuhakikisha sekta ya afya inaimarika ambapo pia, nchi marafiki pamoja na mashirika ya kimataifa yamekuwa yakiendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuhakikikisha sekta ya afya inaimarika na wananchi wanapata huduma za afya," alisema.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland, Eivind Hansen, alisema Hospitali hiyo inajivunia uhusiano na ushirikiano mzuri uliopo kati yake na Hospitali Kuu ya Rufani ya Mnazi Mmoja.

# Ataka maadili kwa wanafunzi wa madrasa

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Mjini, Asha Abdallah Juma, amewataka walimu na wasimamizi wa madrasa zinazofundisha elimu ya dini ya Kiislamu nchini, kusimamia ipasavyo maadili ya wanafunzi wanaosoma katika madrasa hizo.

Aliyasema hayo wakati akikabidhi vifaa mbalimbali vikiwamo mabusati, misahafu na fedha taslimu kwa madrasa ya Ghazal iliyopo Jang'ombe Zanzibar, ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Asha, aliwakumbusha walimu wa madrasa hizo kuhakikisha wanafunzi wanaowafundisha wanakuwa na maadili mema na kuwaepusha kuingia katika matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii ambayo imekuwa ikichangia kuporomoka kwa maadili ya watoto na vijana.

Mbunge huyo alisema maadili ya watoto yanaanzia katika kuandaliwa vizuri katika misingi ya dini, hivyo ni muhimu madrasa nchini zikajitathimini ni kwa kiasi gani zinasimamia maadili ya wanafunzi wao.

"Tunajua changamoto zinazowakabili walimu wa madrasa hasa ukosefu wa kipato kwani wengi wenu mnafanya kazi hizi za kuwalea watoto wetu katika misingi ya kiimani na dini kwa kujitolea bila mishahara wala posho la uhakika, lakini endeleeni nasi tutasaidia kulingana na uwezo wetu.", alisema mbunge huyo.

Akizungumzia vifaa alivyotoa alisema ni mwendelezo wa kutekeleza Ilani ya CCM kwa kuhakikisha makundi mbalimbali yanapata huduma bora za kijamii.

Uongozi wa Madrasa hiyo ulimshukru kwa mchango wake na kuahidi vifaa vilivyotolewa kuvitunza ili viwasaidie wanafunzi wa madrasa hiyo.

# Korti Kuu yabatilisha hukumu ya diwani ACT

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Kigoma, imetengua adhabu ya mwaka mmoja na siku mbili jela iliyokuwa imetolewa na Mahakama ya Wilaya dhidi ya diwani wa Kata ya Mwanga Manispaa ya Kigoma kwa maelezo kuwa adhabu hiyo ilitolewa kimakosa na kubakiza adhabu ya miezi mitano jela iliyokuwa imetolewa na Mahakama ya Mwanzo Mwandiga.

Hukumu ya Mahakama Kuu inafuatia kwenye rufani namba 45/2019 iliyokuwa ikimkabili diwani huyo, Clayton Revocatus maaru 'Baba Revo'.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Jaji wa Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Ilvin Mugeta, baada ya Mahakama ya Wilaya kutoa adhabu kimakosa ya kumfunga mshtakiwa huyo kifungo cha mwaka mmoja na siku mbili jela. Jaji Mugeta alisema adhabu iliyotolewa na Mahakama ya Wilaya ni batili na kusema: "Hivyo ninatengua adhabu hiyo na ninabakiza adhabu ya miezi mitano jela iliyotolewa na mahakama ya Mwanzo Mwandiga, kwa kuwa ilifuata taratibu zote na kanuni za sheria kwa kumtia hatiani mshtakiwa huyo, hata mimi mwenye nimeridhika na adhabu ya mahakama ya mwanzo Mwandiga, hivyo mshtakiwa utatumikia kifungo cha miezi mitano jela iliyotolewa na Mahakama ya Mwanzo Mwandiga."

Alisema katika kesi hiyo Mahakama ya Wilaya ilitakiwa itowe adhabu kwa mshtakiwa ya mwaka mmoja jela kama sheria inavyotaka, badala yake ikatoa adhabu ya mwaka mmoja na siku mbili ambayo ni makosa kisheria.

Upande wa utetezi katika rufani hiyo uliongozwa na mawakili wawili wa kujitegemea, Thomas Msasa na Eliutha Kivyiro, huku upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Robert Magige. Upande wa utetezi ulipeleka sababu sita za rufani kupinga adhabu iliyotolewa na Mahakama ya Wilaya Mkoa wa Kigoma ya kifungo cha mwaka mmoja na siku mbili jela. Sababu ya kwanza ni Mahakama ya Mwanzo Mwandiga ilikosea kisheria na kimatiki kwa kumtia hatiani na kumfunga bila ya kuzingatia maoni ya wazee washauri wa mahakama.

Sababu ya pili ni Mahakama ya Mwanzo Mwandiga ilikosea kisheria na kimatiki kwa kutotilia maanani ushahidi wa mshtakiwa na mashahidi wake. Sababu ya tatu ni Mahakama ya Mwanzo Mwandiga ilikosea kisheria na kimatiki kwa kumtia hatiani bila kesi kuthibitishwa bila kuacha shaka yoyote.

Sababu ya nne Mahakama ya Wilaya ilikosea kimatiki na kisheria kwa kusema kuwa hakuna sheria inayowakataza wazee washauri wa mahakama kuongoza mlalamikaji na mashahidi kutoa ushahidi wao mahakamani, na sababu ya tano Mahakama ya Wilaya ilikosea kisheria na kimatiki kwa kumfunga mleta rufani mwaka mmoja na siku mbili kinyume cha sheria.

Sababu ya sita ni Mahakama ya Mwanzo Mwandiga haikuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri hilo na kuomba mahakama hiyo itengue hukumu ya mahakama hiyo na hukumu ya Mahakama ya Wilaya ili muomba rufani aweze kuachiwa huru.

Awali mshtakiwa huyo anadaiwa kutenda kosa hilo Julai 15 mwaka huu majira ya saa 1 usiku maeneo ya Mwanga kwa Bela katika mataa ya barabara ya Lumumba Manispaa ya Kigoma/Ujiji, mshtakiwa huyo bila halali na kwa makusudi alimshambulia askari polisi mwenye namba F8350 PC Msafiri wa kikosi cha usalama barabarani kwa kumpiga ngumi na makofi sehemu mbalimbali za mwili wake.

Umati mkubwa akiwamo meya wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji, viongozi wa vyama vya siasa na madiwani walifurika Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma kushuhudia hukumu hiyo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Nchini (TIC), Geoffrey Mwambe (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Biashara la Uhalonzi,-Afrika (NABC), Peter Ruiter, wakisaini mkataba wa makubaliano ya kuboresha mifumo ya biashara nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu kuimarika ushirikiano Tanzania, China

**Na Elizabeth Zaya**

TANZANIA imetaja baadhi ya sababu zinazochangia kuendelea kuimarika kwa ushirikiano kati yake na China kuwa ni pamoja na uwapo wa fursa mbalimbali za kiuchumi kati ya pande hizo mbili.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam katika hafla ya kutunuku zawadi kwa wanafunzi Watanzania waliofanya vizuri katika somo la Kichina iliyoandaliwa na Ubalozi wa China nchini.

Alitaja baadhi ya fursa nyingine zinazochangia ushirikiano huo kuwa ni pamoja na fursa za ajira ambazo wananchi wa pande zote wananufaika nazo.

Nyingine alisema ni nafasi ya China katika uchumi wa dunia, fursa za masomo husussani za kubadilishana wanafunzi.

"Hakuna mtu wa kubeza uchumi wa China, ukitaka kufanikiwa hususan kwa nchi zinazoendelea lazima ujifunze kutoka katika nchi hiyo, na ndiyo maana Tanzania tunaendelea kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza huko," alisema na kuongeza:

"Tunafahamu na wao kuna mambo mengi ambayo wananufaika au kujifunza kutoka kwetu, na ndiyo maana wameamua kuanza kujifunza lugha ya Kiswahili na mpaka sasa huko kwao wana vyuo vinne vinavyofundisha lugha yetu."

"Na sisi pia siku hizi kuna masomo ya lugha ya Kichina yanafundishwa ikiwamo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ni lazima tufanye hivyo ili tufaidike na fursa zao mbalimbali, " alisema na kuongeza kuwa zaidi ya wanafunzi 200 kutoka Tanzania wanasoma nchini China kwa msaada wa nchi hiyo.

Balozi wa China nchini, Wang Ke, alisema China itaendelea kuimarisha ushirikiano huo ikiwamo kuongeza nguvu ya kuwasaidia wanafunzi kwenda kusoma nchini humo.

# Benki ya Exim yaingia Ethiopia

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania imezidi kujitanua zaidi nje ya mipaka ya Tanzania kwa kufungua kituo cha huduma za benki hiyo katika jiji la Addis Ababa nchini Ethiopia.

Hatua hiyo ilitangazwa jana na Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Bernard Kibesse, wakati akifungua rasmi tawi jipya la benki ya Exim Tanzania lililopo katika mtaa wa Mkwepu jijini Dar es Salaam, baada ya benki hiyo kukamilisha taratibu za umiliki wa iliyokuwa Benki ya UBL Tanzania.

Katika uzinduzi huo, Dk Kibesse alimuwakilisha Waziri wa Fedha na Mipango, Dk Philip Mpango.

Kufuatia hatua hiyo benki hiyo inakuwa taasisi ya kwanza ya kifedha nchini kuendesha shughuli zake kwenye mtandao wa mataifa matano ikiwamo Ethiopia ambayo inatajwa kuwa ndio nchi ya pili kwa ukubwa wa idadi ya watu barani Afrika. Mataifa mengine ambayo benki hiyo inaendesha huduma zake ni Uganda, Comoros na Djibouti.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na benki hiyo jijini Dar es salaam jana, benki hiyo imepata leseni ya kufungua na kuwa na Ofisi ya mwakilishi wake Ethiopia kupitia tawi lake la Djibouti na imepanga kuanza kazi kutoa huduma zake nchini humo hivi karibuni.

"Tunatarajia kwamba huduma zetu zitaanza kutolewa kikamilifu mapema mwezi Disemba, 2019 kupitia Ofisi ya Mwakilishi wetu kibiashara iliyopo katika Jengo la Zouleka LKG, ghorofa ya 2, Sub City Bole, 2160 / B. Addis Ababa. " alisema Jaffari Matundu, Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo kupitia taarifa hiyo.

"Hii ni hatua muhimu kwa Benki ya Exim ikiwa kama kikundi." alisema Matundu huku akibainisha kuwa ukuaji thabiti wa uchumi nchini Ethiopia ambao umechochewa na uwekezaji mkubwa wa umma na ongezeko la wateja ndio sababu nchi hiyo imekuwa kivutio kwa taasisi za kifedha kuwekeza katika taifa hilo.

HABARI KIMATAIFA

# Uganda yatengeneza simu ya kwanza ya mkononi

**KAMPALA,** Uganda

UGANDA imezindua simu ya mkononi ya kwanza iliyotengenezwa katika taifa hilo pamoja na kuzindua kiwanda kilichoitengeneza.

Kiwanda cha simu nchini Uganda kipo maeneo ya Namanve, mashariki mwa mji mkuu wa Kampala, na kinaendeshwa na kampuni ya China ya ENGO kinachotengeneza simu zinazoitwa SIMI.

**Mwaka jana, Uganda ilipokea simu zenye thamani za bilioni moja kutoka China.**

Simu za kwanza kutengenezwa katika kiwanda cha nchini Uganda, kila siku Uganda itatengeneza simu 2,000 zitakuwa za kawaida, simu 1,500 zitakuwa 'simu za smartphone' na komputa mpakato 800.

'Smartphone' zitauzwa kwa kiasi cha dola 54 na simu ya kawaida ni dola 8. Kuanzishwa kwa kiwanda hicho kumetoa fursa kwa serikali ya Uganda kutoa mwanya wa ajira, huku uwekezaji mkubwa ukiwa unatoka China.

Mwaka jana, Uganda ilipokea simu zenye thamani za bilioni moja kutoka China, huku simu zilizotumwa kwenda China ziligharimu dola milioni 32 kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa.

China inaongoza pia kwa kutoa misaada katika miundombinu ya miradi mikubwa nchini Uganda na mataifa mengine ya Afrika Mashariki. **BBC**



Simu ya mkononi aina ya simi ya kwanza kutengenezwa nchini Uganda. **PICHA: BBC**

## Ndege yaanguka, yaua DRC

**GOMA,** DRC

NDEGE ya abiria iliyokuwa ikiwabeba watu 16 imeanguka katika mji wa

Goma mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kuua watu kadhaa.

Gavana wa Jimbo la Kivu Kaskazini, Nzanzu Kasivita Carly, amesema kwamba watu kadhaa wamefariki dunia, lakini hakutoa idadi kamili .

Ndege hiyo aina ya Doenier 228 ilikuwa ikimilikiwa na kampuni binafsi ya Busy Bee.

Ilitarajiwa kuelekea Beni takribani kilomita 350 kutoka kaskazini mwa Mji wa Goma, na kwamba ilianguka dakika moja baada ya kupaa, kwa mujibu wa chanzo kimoja katika mji wa Goma kilichozungumza na BBC. **BBC**

## Guinea Bissau kuchagua rais

**BISSAU,** Guinea Bissau

RAIA nchini Guinea Bissau wanapiga kura leo kumchagua rais mpya chini ya kiwingu cha hali mbaya ya kisiasa inayotokana na mivutano, maandamano ya vurugu na madai ya jaribio la mapinduzi.

Rais Jose Mario Vaz ambaye utawala wake umeandamwa na bunge lisilofanya kazi, anawania muhula wa pili madarakani pamoja na wagombea wengine 11.

Vaz, anayeongoza chama cha MADEM kisicho na wingi wa viti bungeni, anachuana kwa karibu na Domingos Simoes Pereira, mgombea wa chama cha PAIGC kilichoshinda viti vingi vya bunge wakati wa uchaguzi wa bunge wa Machi. **DW**

## Polisi waua waandamanaji

**BAGHDAD,** Iraq

POLISI na maofisa wa afya nchini Iraq wamesema vikosi vya usalama vimewaua watu watatu baada ya kufyatua risasi dhidi waandamanaji kwenye mji wa kusini wa Nassiriya juzi Jumamosi.

Zaidi ya watu wengine 50 walijeruhiwa kutokana na risasi za moto na mabomu ya kutoa machozi wakati polisi ilipojaribu kuwatawanya waandamanaji waliokusanyika kwenye madaraja matatu muhimu yaliyopo kwenye mji huo.

Karibu watu 330 wameuawa tangu kuanza kwa maandamano ya umma mwezi Oktoba kwenye mji mkuu Baghadad na kusini ya Iraq katika moja ya maandmanao makubwa zaidi tangu kuangushwa kwa utawala wa Saddam Hussein mwaka 2003.

Waandamanaji wanataka kupinduliwa kwa tabaka tawala linalokosolewa kwa rushwa na kuyatumikia mataifa ya kigeni, huku raia wengi nchini humo wakiishi bila kazi, elimu na huduma bora za afya. **DW**

## Hong Kong kupiga kura kuchagua madiwani

**HONG KONG,** China

WAPIGAKURA mjini Hong Kong leo, wanapiga kura kuchagua baraza la madiwani, huku kambi inayopigania demokrasia ikitumaini kuwa uchaguzi huo utatuma ujumbe kwa serikali inayoungwa mkono na China Bara.

Kuelekea uchaguzi wa leo, kisiwa hicho kimekabiliwa na maandamano makubwa na ghasia baina ya polisi na waandamanaji kwa kipindi cha karibu miezi sita sasa.

Jukwaa linaloratibu maandamano limewahimiza raia kupiga kura na kuepusha vitendo vya ghasia, iwapo serikali itaamua kuingilia uchaguzi huo.

Kiasi cha wapigakura milioni 4 wamejiandikisha kushiriki uchaguzi wa leo. Uchaguzi huo unalenga kuwachagua jumla ya madiwani 452 wa Baraza la halmashauri katika wilaya 18, ambalo linatoa uwakilishi wa moja kwa moja. Polisi wamesambazwa katika vituo vya kupigia kura ili kuzuia aina yoyote ya ghasia. **DW**

## Seneti yaidhinisha uchaguzi Bolivia

**PUNILLA,** Bolivia

BARAZA la Seneti nchini Bolivia limeidhinisha kufanyika uchaguzi mwingine wa bunge, huku aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Evo Morales, akipoteza sifa ya kushiriki uchaguzi huo.

Kulingana na tangazo kutoka baraza hilo, wagombea ambao wamekuwa madarakani katika kipindi cha mihula mitatu iliyopita hawatoruhusiwa kuwania tena viti vyao.

Muswada huo wa sheria uliopitishwa kwa kauli moja na baraza la seneti unaelekeza pia wajumbe wapya wa tume ya uchaguzi wapatikane ndani ya kipindi cha siku ishirini.

Rais wa mpito wa Bolivia, Jeanine Anez, amesema atatia saini muswada huo kuwa sheria, lakini amekataa muswada uliopendekezwa na chama cha Morales wa kutoa msamaha kwa rais huyo wa zamani na makamu wake wa Rais, Alvaro Garcia Linera. **DW**

# Shigella kupambana na wenye magari mabovu

**Na Steven William,** MUHEZA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigella ameapa kuwashughulikia wamiliki wa vyombo vya usafiri wa moto mkoani Tanga ambao magari yao yatabainika kuwa mabovu.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wakazi wa mji wa Mkata, wilayani Handeni juzi, akiwaongoza wananchi na viongozi mbalimbali kuaga miili ya madaktari watatu waliofariki dunia katika ajali ya gari, wilayani Handeni.

Madaktari waliofariki katika ajali hiyo ni Razaro Mpiziwa, Lucas Lubacha na Mussa Muro, ambao waliagwa juzi katika Kituo cha Afya cha Mkata, wilayani Handeni kwa ajili ya kusafirishwa.

Shigella alisema kuna matajiri wanaomiliki vyombo vya usafiri mkoani Tanga ambao magari yao yakikamatwa na askari wa usalama barabarani wanapiga simu kwa wakubwa ili yaachiwe.

Aliwaagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe na Kamanda wa Polisi wa Kitengo cha Usalama Barabarani, Solomoni Mwangamilo, watakapopigiwa simu na mkubwa yeyote wakatae kuachia magari mabovu, lengo ni kuzua ajali mkoani hapo. Shigella alisema kupoteza maisha ya madaktari watatu kwa mara moja ni pigo kubwa kwa serikali na Mkoa wa Tanga.

Alimwagiza Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Zena Saidi kupeleka madaktari watatu katika kituo cha Mkata na kituo cha Afya cha mji wa Kabuku ili kuziba nafasi ya marehemu hao.

Vilio na simanzi vilitawala katika mji wa Mkata wilayani Handeni mkoani Tanga wakati wa kuaga miili ya madaktari hao ambao walifariki katika ajali ya lori wakitokea mkoani Kilimanjaro kuelekea katika vituo vyao vya kazi katika mji wa Kabuku na Mkata. Ajali hiyo ilitokea usiku wa kuamkia juzi katika kijiji cha Taula, Kata ya Kwedizinga, wilayani Handeni wakati madaktari hao wakitoka katika Hospitali ya KCMC mkoani Kilimanjaro katika mafunzo ya kutumia vifaa vya kisasa vya kupima magonjwa ya tumbo.

Wakati wa kuaga miili ya madaktari hao, viongozi mbalimbali wa serikali, bunge, walitoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu.



Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi (kushoto), akifanyiwa mahojiano na Mtangazaji wa East Africa Television, Samson Charles, ambapo alieleza jitihada za serikali ya awamu ya tano katika kufikia uchumi wa viwanda na kuipongeza East Africa Radio na East Africa Television kwa kuanzisha kampeni ya kibiashara zaidi ambayo inasaidia kuongeza uelewa wa biashara kwa wananchi. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Kifusi chaua mchimba dhahabu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAYUNGA Bunga (31), Mkazi wa Wilaya ya Itilima mkoani Simiyu, amefariki dunia kutokana na kufukiwa na kifusi kwenye shimo alilokuwa akichimba dhahabu kwenye mgodi mdogo wa Mwakitolyo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya asubuhi, wakati mchimbaji huyo akiwa na wenzake wakichimba dhahabu ambapo yeye alikuwa ameingia shimoni peke yake akichimba, huku wenzake wakipokea mchanga unaodhaniwao kuwa na madini, ndipo alipofukiwa na kufariki.

Mwenyekiti wa wachimbaji wa dhahabu katika mgodi huo, Alphonce Paulo, alisema mara baada ya kijana huyo kufunikwa na kifusi shimoni, wenzake walitoa taarifa ndipo juhudi za uokoaji zikafanyika, lakini walipomtoa walikuta tayari ameshafariki.

"Kijana huyu alikuwa ndani ya shimo ndipo kifusi kikiwa na majabali ya mawe yaka poromoka na kumfukia humo shimoni, tuliitaka kujaribu kuokoa uhai wake, lakini bahati mbaya tulimkuta akiwa ameshafariki," alisema Paulo.

# Mkanganyiko uchaguzi Serikali za mitaa

INATOKA UK.8

kwenda kupiga kura, lakini vituo vimefungwa kwa madai kuwa hawakupata taarifa ya wagombea kupita bila kupingwa.

Katika kata ya Wazo yenye mitaa minane, wagombea wake wamepita bila kupingwa hivyo, hakukuwa na upigaji kura.

Hali kadhalika, Kijitonyama hakukuwa na upigaji kura baada ya wagombea wa CCM kupita bila kupingwa.

Katika kituo cha Kilimahewa juu, Nipashe ilikuta polisi wawili na wananchi watatu waliokuwa wakisubiri kufunguliwa kwa ofisi, huku viongozi waliokuwapo wakiwataka warudi nyumbani kusubiri taarifa kwenye vyombo vya habari.

"Sisi tunatembelea vituo mbalimbali kulinda amani na kuangalia upigaji kura unavyoendelea, hapa ofisi imefungwa na hakuna wa kutoa taarifa kwa wananchi," alisema askari mmoja.

Pia, wananchi waliohojiwa walisema wamefika kupiga kura kwa kuwa walijiandikisha, lakini cha kushangaza wamekuta ofisi zimefungwa bila kuwapo kwa tangazo wala taarifa za kutokuwapo kwa upigaji kura.

Katika mtaa wa Kilimani ambako kuna ofisi ya kata ya Wazo, ofisi ya mtaa ilikuwa imefungwa huku ofisi ya mtendaji wa kata ikiwa wazi na wananchi kwa nyakati tofauti kutaka kupiga kura.

Nipashe ilishuhudia zaidi ya wananchi 20 waliofika na kuondoka kwenye eneo hilo bila kupiga kura majira ya asubuhi.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, walisema hawakupewa taarifa yoyote ya kutokuwapo kwa upigaji kura, hivyo walifika kituoni kutumia haki yao ya kikatiba.

Alisema hakukuwa na taarifa zozote, hivyo walifika kupiga kura na kuambiwa watajulishwa, jambo linalowafanya wajiulize watajulishwa kwa simu au kwa njia gani.

"Tutaambiwaje, tutapigiwa simu, matangazo, tuko gizani, hali hii inakatisha tamaa ndiyo maana tunaona hakuna haja ya kujiandikisha kupiga kura, tunapoteza muda wetu na leo mvua inanyesha ila tumejipanga kuja kupiga kura tunakuta pamefungwa," alilalamika.

Naye, Moses Nyangiriki mkazi wa Mtaa wa Kilimahewa Mbarikiwa, alilalamika kwa kunyimwa haki ya kupiga kura kwa kuwa walijiandikisha kwa lengo hilo.

July Massawe, kwa upande wake alisema baada ya kujiandikisha waliambiwa warudi Novemba 24, kupiga kura, lakini wamekuta ofisi zimefungwa.

"Nimetoka mbali sana, tunapoambiwa kwamba hakuna haja ya kupiga kura kwa sababu vyama vingine vimejiengua, tunashindwa kuelewa, tunajisikia hatujatendewa haki na ni usumbufu sana, na hadi sasa hatujui nani ameshinda ambaye atakuwa kiongozi wetu," alidai.

Mkoani Katavi Mratibu wa uchaguzi wa mkoa huo, alieleza kuwa kulikuwa na vituo 717 kwa ajili ya uchaguzi wa vijiji 172, lakini kote haujafanyika kwa kuwa wagombea wa CCM wamepita bila kupingwa.

Alisema wagombea hao wamepita baada ya vyama vingine kujitoa kwenye mchakato huo na washindi watatangazwa na kuwakabidhi miongozo ya kuanza kazi zao baada ya kuapishwa.

### ACT- Wazalendo

Akiongea na gazeti hili jana kuhusu kuonekana kwa majina ya wagombea wa ACT-Wazalendo katika karatasi za kupigia kura licha ya chama hicho kupiga marufuku nembo za chama hicho pamoja na wagombea wao kuonekana katika karatasi hizo, Katibu Mkuu wa chama hicho, Dorothy Semu, alisema msimamo wao upo palepale na kwamba watachukua hatua baada ya kupata taarifa kamili.

"Kwa sasa ni mapema sana kusema kinachofuata tunaendelea kupokea matukio ya uchaguzi huu tuliojitoa na tathmini ya yote tutatoa uamuzi wa chama kwa matukio kama hayo," alisema Dorothy.

### CUF yanena

Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa CUF, Abdul Kambaya, akizungumzia uchaguzi huo na kutumika kwa nembo za chama hicho licha ya kujitoa katika uchaguzi, alisema chama hicho hakifuatilii chochote kinachoendelea kwenye uchaguzi tangu kilipotangaza kujitoa.

### Jafo apongeza

Uchaguzi katika jiji la Dodoma, ulifanyika katika mitaa miwili ya Chadulu B, Kata ya Makole pamoja na Chihikwi, kata ya Mbalawa kwa CCM) na Chama cha Wakulima (AAFP), kuwa peke vilivyoweka wagombea huku kituo kimoja cha tatu mgombea akijitoa muda mfupi kabla ya uchaguzi.

Akizungumza katika kituo cha kupigia kura cha Chadulu B, Msimazi wa uchaguzi Asha Hemed, alisema kuwa tangu kituo hicho kilipofunguliwa saa mbili asubuhi, idadi ya wananchi waliokuwa wanajitokeza iliongezeka kadiri muda ulivyokuwa ukienda.

Msimamizi wa uchaguzi Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, alisema katika jiji hilo mitaa miwili pekee ndiyo inayofanya uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Katika kituo hichi cha Chadulu B, hadi hivi sasa kuna watu waliokwisha kuja kupigia kura takribani 100, lakini tunatarajia kupata watu kama 500 kwa hali ilivyo hadi hivi sasa idadi hiyo tutaifikia,"alisema Kimaro.

Waziri wa nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa, (Tamisemi), Selemani Jafo, akizungumza na waandishi wa habari wakati akikagua baadhi ya vituo vya kupigia kura, aliwataka wananchi kujitokeza kuchagua viongozi wanaowataka.

Pia, alisema katika vituo alivyotembelea uchaguzi ulifanyika katika mazingira ya haki na amani kwa vyama vyote vilivyogombea katika uchaguzi huo.

Alivipongeza vyama vilivyoweka wagombea katika uchaguzi huo ambao mwaka huu unaongozwa na kanuni za kutosha tofauti na chaguzi zilizopita.

"Watu walizoea ule uchaguzi wa kimazoea lakini awamu hii uchaguzi huu unafanyika kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizowekwa hivyo niwapongeze wote waliopata nafasi ya kushiriki mimi kama msimamzi wa uchaguzi huu ngazi ya taifa nawapongeza sana"alisema Jafo.

Katika hatua nyingine mgombe wa nafasi ya mwenyekiti wa serikali za mitaa wa mtaa wa Njedengwa, kata ya Makulu jijini hapa, Daimu Haji amepita bila kupingwa baada ya mgombea mwenza wa chama cha AAFP, Alex Mahenge, kujitoa dakika za mwisho kabla ya kuanza kwa zoezi la upigaji kura jana asubuhi.

Alipoulizwa sababu ya kujitoa kwake alisema ni kutokana na chama chao kutowasaidia wakati wa kampeni za kugombea nafasi hiyo ya uchaguzi.

***Imeandikwa na Salome Kitomari na Enock Charles (Dar), Marco Maduhu (Shinyanga), Paul Mabeja na Renatha Msungu (Dodoma)***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311


**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*


TWINS AUCTION MART & COURT BROKER
P.O.Box1305 Songea,
Head Office: Nssf Building Room No.12 & 13 Songea,
Branch Office 2nd Floor Mbinga Stand Room No 105 Mbinga,Makambako Near Sabbath Church Mlando Street
.5th Floor,Green Leaf Tower .Lumumba /Mkunguni Street Dar Es Salaam,Capri Point Mwanza Town
Mobile: 0716070298/0754881926/0784718734.Email:Zuberihasani10@Yahoo.Com

TANGAZO HILI LIMETOLEWA LEO 18/11/2019

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

AMPUNI YA TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED & COURT ROKER KWA IDHINI TULIYOPEWA NA MSIMAMIZI WA MIRATHI AREHEMU KALASI HAKIMU ALLY NDUGU AHAMAD SELEMANI SANDA WA MAJENGO MANISPAA YA SONGEA. TUTAUZA KWA NADA WA HADHARA NYUMBA KIWANGA NAMBA 427 KITALU "V" IYOPO MTAA WA MAJENGO QUARTERS. MNADA UTAFANYIKA AREHE 13/12/2019 SIKU YA IJUMAA KUANZIA 4:00 ASUBUHI KATA YA AJENGO MANISPAA YA SONGEA.

ASHARTI YA MNADA:
NUNUZI WA NYUMBA ATAKAE BAHATIKA ATATAKIWA KULIPA 25% A BEI ILIYOFIKIWA PAPO HAPO NA KIASI KILICHOBAKI KILIPWE DANI YA SIKU 14 KINYUME CHA HAPO PESA ILIYOTOLEWA AWALI AITARUDISHWA NA MNADA UTARUDIWA TENA. GHARAMA ZA JBADILISHA HATI MILIKI(TRANSFER OF OWNER SHIP) NA HARAMA NYINGINE HASA USAFIRI NI ZA MTEJA MWENYEWE NA YUMBA ITAANZA KUKAGULIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO ILI

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na:-

MKURUGENZI
TWINS ACTION MART CO.LTD
S.L.P 1305
SONGEA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA**
**AT SAMORA AVENUE**
**CIVIL CASE NO. 82/2018**

**MOHAMED**
**AMOUR..................................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**MASUDI M. KATIMULE.........DEFENDANT**

**O:** MASUDI M. KATIMULE
P.O BOX.........
DSM.

**AKE A NOTICE** that the Plaintiff has instituted a it against you with particulars of claim set out in plaint filed in this court.

ervice of the summons on you has been ordered means of this publication. You are defected to ollect copies of the summons and plaint from the ourt's Registry.

ou here by summoned to appear in this court in erson or by an Advocate or an agentduly thorized on 25-11-2019 at 8:00 a.m. when this iit will be mentioned.

**AKE FURTHER NOTICE** that should you efault to enter appearance in Court on the day ne mention above, the suit will proceed and dgment may given in your absence.

iven under my hand and the seal of this 21 day of ctober 2019.

..............................
RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT ILALA
DAR ES SALAAM


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# LUKAKU: MBINU ZA SOLSKJAER ZIMENIONDOA MAN UNITED

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku amedokeza kwamba kubadilishwa kwa nafasi yake ya uchezaji chini ya kocha Ole Gunnar Solskjaer pale Manchester United alijua kwamba kipindi chake cha uchezaji kimefikia mwisho.

Mshambuliaji huyo wa kati, ambaye alinunuliwa kwa fedha nyingi kutoka kule Everton mwaka 2017, alibadilishwa na kuchezeshwa kama winga kwa miezi yake ya mwisho pale Old Trafford.

Hofu juu ya kiwango chake na ufiti wake kukamfanya Solskjaer kumtumia Marcus Rashford na Anthony Martial katikati, kitu ambacho kilimshawishi Lukaku kuondoka na kwenda Inter Milan Agosti mwaka huu.

"Ilikuwa baada ya mchezo dhidi ya West Ham nyumbani (Aprili 13) - Solskjaer aliamua kunichezesha kama winga wa kulia, kwa upana zaidi," alisema Lukaku akiliambia Gazeti la Corriere dello Sport.

"Uzoefu nilioupata pale Manchester ulinifanya niwe imara zaidi kiakili kwa sababu kila kitu kilikwenda tofauti na nilivyotarajia.

"Sikuweza kushinda kile nilichokuwa nakitumaini, kiwango changu na sikuhisi kwa asilimia 100 kile ambacho nilikitaka. Si kwa kiasi kikubwa kutoka kwenye benchi la ufundi na kutoka kwa wachezaji wenzangu, lakini kutoka kwa watu wanaonizunguka.

"Hivyo, baada ya mchezo dhidi ya Chelsea wa Aprili 28, kocha aliniita kwenye mkutano na nilimwambia nini ninachofikiria au niondoke."

# Mourinho aeleza kwa nini hakumtumia Eriksen

**LONDON,** England

JOSE Mourinho ameelezea uamuzi wake wa kumuacha Christian Eriksen nje ya kikosi chake cha kwanza cha Tottenham akisema kwamba anataka kuelewa nini kilichopo kwenye mawazo ya kiungo huyo.

Eriksen amekuwa akivumishiwa kwamba anataka kuondoka hapo Tottenham baada ya kushindwa kufikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya huku mkataba wake wa sasa ukimalizika Juni 2020.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, Eriksen anapanga kuondoka Januari wakati wa dirisha dogo la usajili na anawaniwa na Manchester United na Mourinho alimuweka nyota huyo wa kimataifa wa Denmark kwenye benchi wakati akiiongoza Spurs kwenye mchezo wake wa kwanza dhidi ya West Ham.

Eriksen hakutumika kwenye mchezo uliopita wa Tottenham uliomalizika kwa sare ya 1-1 dhidi ya Sheffield United, lakini Mourinho aliiambia BT Sport uamuzi ya kumuweka benchi "si endelevu."

"Bilashaka mchezo wa leo (juzi) ulikuwa muhimu, lakini majaliwa yetu ya baadye pia ni muhimu zaidi," alisema Mourinho.

Spurs watacheza na Olympiacos kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Bournemouth nyumbani kwenye michezo yake miwili inayofuata na Mourinho amesema anaangalia namna ya kutafuta njia bora ya kuwa na safu bora ya ushambuliaji.






# *Guardiola ahofia kumkosa Aguero kwa muda mrefu*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anahofu anaweza kuwa bila Sergio Aguero kwa muda mrefu baada ya mshambuliaji huyo kuumia "vibaya" misuli ya nyama za paja wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Chelsea juzi.

Aguero alitolewa nje baada ya dakika 13 na nafasi yake kuchukuliwa na Gabriel Jesus na City wakatoka nyuma kuifunga Chelsea kwenye Uwanja wa Etihad.

City ilirudi mchezoni baada ya kufungwa na N'Golo Kante dakika ya 21 kwa mabao ya Kevin De Bruyne na Riyad Mahrez kuweza kupata pointi zote tatu, lakini sasa analazimika kusubiri kuona kwa namna gani majeraha ya Aguero yatakavyokuwa.

Guardiola aliiambia Sky Sports: "Nafikiri Sergio atakuwa ameumia vibaya.

"Daktari atalazimika kuangalia, alifikiri ilikuwa ni kawaida, lakini inaonekana kaumia zaidi. Lakini tutaangalia kesho (leo).

"Hisia ni kwamba kama misuli yake haitakuwa fiti, tutampoteza katika kipindi kigumu zaidi cha msimu, lakini hivyo ndivyo ilivyo. "Tuna wachezaji vijana na tutawajaribu."

Guardiola pia alibainisha viungo, Rodri na David Silva walionekana wameumia wakati wa ushindi huo dhidi ya kikoci cha Frank Lampard.

Bosi huyo wa City aliongeza: "Kwa Rodri na David Silva, walikuwa na matatizo ya maumivu na walikuwa wamechoka."

## HABARI MICHEZO

# Klopp: Liver imepigana kwa dakika zote 90

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Jurgen Klopp alikuwa na furaha kuona Liverpool ikiibuka na ushindi dhidi ya Crystal Palace baada ya kupigana kwa nguvu na kupata ushindi wa mabao 2-1.

Liverpool walionekana kuzidiwa katika kipindi cha kwanza, na bao walilofungwa na James Tomkins lilikataliwa na VAR.

Lakini Liverpool iliimarika kipindi cha pili baada ya Wilfried Zaha kusawazisha bao la Sadio Mane na wakapata la pili lililofungwa na Roberto Firmino na kuwafanya wapeta ushindi wa 12 kwenye Ligi Kuu katika mechi 13 msimu huu.

Klopp alisema baada ya mchezo huo, kiwango kilichoonyeshwa na timu yake kilimvutia, kwani walipigana kuanzia dakika ya kwanza.

"Changamoto ilikuwa ni kubwa, lakini kila mmoja alicheza kwa nafasi yake na tulipambana kwelikweli," alisema.

"Leo (juzi) sikuwa na tatizo, kwani wachezaji walicheza kwa kujituma na kwa kiwango kinachofurahisha na kwa uhakika kabisa, tulikuwa bora kabisa tangu dakika ya kwanza."





# MAGUIRE AIOMBEA USHINDI SHEFFIELD

**MANCHESTER,** England

HARRY Maguire anafurahishwa kuona klabu yake ya utotoni Sheffield United 'ikipaa' kwenye Ligi Kuu ya England na anawataka kushinda kila mchezo isipokuwa wanapocheza na Manchester United.

Beki huyo wa kati wa England, Maguire aliweka rekodi ya kuwa mlinzi ghali zaidi duniani wakati alipohamia Old Trafford kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 80 akitokea Leicester City kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alikulia kwenye akademi ya klabu hiyo na aliichezea mechi 100 katika ngazi ya timu ya wakubwa kabla ya kuondoka na kujiunga na Hull City mwaka 2014.

"Inamaana kubwa kwangu, klabu ambayo ilinipa nafasi ya kutimiza ndoto yangu na kuwa mchezaji wa kulipwa wa soka," alisema Maguire akiiambia BBC Sport.

"Nawakubali, nitakwenda na kuwapa sapoti yangu kila wanapocheza, lakini si dhidi ya Manchester United.

"Ni klabu iliyonilea na kunifanya kuwa mtu ambaye sasa anaonekana kwenye klabu na uwanjani."



# Kocha Flamengo apagawa ubingwa wa Libertadores

**SAO PAULO,** Brazil

KOCHA wa Flamengo, Jorge Jesus, ameelezea ushindi ilioupata timu yake kwa kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini, Copa Libertadores, kama "muhimu zaidi katika maisha yake ya soka."

Mabao mawili ndani ya dakika tatu kutoka kwa Gabriel 'Gabigol' Barbosa yakawafanya Flamengo kupata ushindi wa 2-1 dhidi ya mabingwa watetezi, River Plate mjini Lima Jumamosi.

Flamengo walikuwa nyuma kwa bao la Rafael Santos Borre la kipindi cha kwanza, hadi Gabriel aliposawazisha dakika ya 89 na kufunga la ushindi dakika tatu baadaye. Mshindi huyo mara tatu wa ligi akiwa na Benfica, huku pia alitwaa taji akiwa na Braga, Sporting CP na Al Hilal, ameelezea mafanikio yake hayo.

"Ni kitu muhimu zaidi katika maisha yangu ya soka," alisema Jesus mara baada ya mchezo huo.

"Ni Copa Libertadores kwa Amerika Kusini na ni Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa Bara la Ulaya.

Timu yoyote katika bara hili inaweza kushinda taji hili. Sasa tutajaribu kushinda taji la Ligi Kuu ya Brazil, maarufu kama Serie A (kama ilivyo kwa Italia), ambalo nalo ni taji muhimu."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG AELEZEA MATATIZO YA ARSENAL

●●● Ni kufuatia sare na Southampton, asema wachezaji wote wanatakiwa kujiuliza kwa nini...

**LONDON,** England

PIERRE-Emerick Aubameyang amesema Arsenal wanatakiwa kujiuliza maswali wao wenyewe baada ya kutoka sare ya kufungana mabao 2-2 na Southampton na kuwaacha bila ushindi kwa mechi tano mfululizo za Ligi Kuu.

**Alexandre Lacazette alifunga mara mbili dhidi ya timu hiyo iliyofungwa mabao 9-0 na Leicester City mwishoni mwa Oktoba, akisawazisha baada ya Danny Ings na James Ward-Prowse kuwaweka mbele wageni hao.**

Bao la pili la Lacazette ambalo ni la nne msimu huu kwenye Ligi Kuu - lilikuja katika dakika za nyongeza na halikushangiliwa sana kwenye Uwanja huo wa Emirates.

Kwa uhakika 'Washika Bunduki' hao waliondoka uwanjani wakizomewa na Aubameyang aliulizwa kama walistahili, na nahodha huyo alijibua: "Sijui.

"Wakati tunapocheza, sisi ndio wa kwanza kukatishwa tamaa wakati mambo yanapokuwa si mazuri. Tutajaribu kupambana. Nafikiri tuna ubora na tunaweza kurudi na kupambana.

"Nafikiri kila mmoja anatakiwa kujiuliza yeye mwenyewe nini anachoweza kubadilisha, nini anachoweza kukifanya zaidi. Kila mmoja anatakiwa kufanya hivyo, mimi kwanza. Nitajaribu kufanyia kazi na kuangalia njia bora za kushinda."

Aubameyang alivaa kitambaa cha unahodha cha Arsenal kwa mara ya kwanza dhidi ya Southampton, lakini kiwango chake kilifunikwa na Lacazette siku ambayo wachezaji wote wa 'washika bunduki' hao walikuwepo.

Huku kikosi hicho cha kocha Unai Emery kikikabiliwa na mchezo unaofuata kwenye Ligi ya Europa dhidi ya Eintracht Frankfurt, Aubameyang ameahidi kikosi chake kuimarika zaidi na kutafuta ushindi wake wa kwanza baada ya mechi saba.

Alipoulizwa nini tatizo kwa Arsenal, Aubameyang alijibu: "Sijui kwa uhakika. Kitu pekee ninachoweza kusema sisi kama timu, wachezaji, tutajaribu kupambana.

"Tunatakiwa kutafuta suluhisho kwa pamoja. Nafikiri tunatakiwa kubakia kuwa imara. Sisi ni wanaume na tunatakiwa kubeba kazi yetu na kuifanya kwa bidii.

"Tuna mchezo Alhamisi na tutaanza kuangalia kutokea mchezo huu ili kubadilisha mambo. Kwa kesi hii, ni rahisi kusema kwa kila mmoja, lakini sisi ni wanaumwe. Sisi ni kundi na tunatakiwa kutafuta suluhisho kwa pamoja. Hicho ndicho tutakachokwenda kukifanya.

"Kila mmoja alikatishwa tamaa leo (juzi), mashabiki na wachezaji. Hatukucheza kwa umakini leo. Si matokeo mazuri kwa upande wetu. Mara zote tukicheza nyumbani tunatakiwa kushinda mechi zetu. Tunatakiwa tuendelee kupambana."

## ZISIKUPITE

### SOLSKJAER KUGEUKIWA MKOPO

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anaamini "pengine hatasajili" mchezaji yeyote kati ya wanaoongoza kwenye orodha ya kusajiliwa na klabu hiyo katika dirisha la Januari na badala yake atageukiwa wa kusajili kwa mkopo. ***(Telegraph)***

### ZANIOLO AWANIWA UTD, PSG

MANCHESTER United na Paris St-Germain wapo tayari kulipa euro milioni 60 kwa kiungo wa Roma na Italia, Nicolo Zaniolo, 20. ***(Il Messaggero - in Italian)***

### KAICHOMOLEA TOTTENHAM

KOCHA wa Ubelgiji, aliyewahi pia kuinoa Everton, Roberto Martinez alitakiwa kwenda kuinoa Tottenham baada ya Mauricio Pochettino kutimuliwa. ***(Daily Star)***

### BAYERN, DORTMUND KWA TROY

BORUSSIA Dortmund inataka kumsajili mshambuliaji wa Tottenham na Jamhuri ya Ireland, Troy Parrott, 17, huku Bayern Munich nayo ikivutiwa na huduma yake. ***(Express)***

### PALACE YAMTAKA BREWSTER

CRYSTAL Palace imewasiliana na Liverpool kuhusu uwezekano wa kumpata kwa mkopo mshambuliaji wa England U-21, Rhian Brewster, 19. ***(Football Insider)***

### IBRA' KUREJESHWA MILAN

AC Milan inataka kumrejesha Zlatan Ibrahimovic, 38, hapo San Siro. Mshambuliaji huyo wa zamani wa Sweden, ambaye hana klabu baada ya kuondoka LA Galaxy, alitwaa ubingwa wa Serie A msimu wa 2010-11 akiwa na klabu hiyo ya Italia. ***(Calciomercato - in Italian)***

### RONALDO DADO AINUFAISHA UTD

MANCHESTER United itapokea pauni 850,000 kutoka Juventus majira ya joto yajayo sehemu ya dili ambapo mshambuliaji wao wa zamani Cristiano Ronaldo, kujiunga na klabu hiyo ya Italia akitokea Real Madrid. ***(The Sun)***

### JESUS AZIVUTIA INTER, ARSENAL

ARSENAL inapambana na Inter Milan kuipata saini ya kiungo mshambuliaji wa Flamengo na Brazil U-17, Reinier Jesus, 17. ***(The Sun)***

### ATAKIWA GALATASARAY

MARIO Balotelli anawindwa na Galatasaray. Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alijiunga na klabu ya mji wa nyumbani kwao, Brescia majira haya ya joto. ***(Calciomercato - in Italian)***

### KUMUUZA SUNG-YUENG

NEWCASTLE itampiga bei kiungo Ki Sung-yueng, 30, katika dirisha la usajili la Januari. ***(Football Insider)***

### BRUCE ATAKA KUMSAJILI BOWEN

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce anataka kumsajili kiungo wa Hull City, Jarrod Bowen, 22, lakini yupo tayari kusubiri hadi mwishoni mwa msimu. ***(Daily Star)***

### ASTON VILLA KWA BENRAHMA

ASTON Villa bado inavutiwa kumsajili winga wa Brentford na Algeria, Said Benrahma, 24, katika dirisha la Januari. ***(Sky Sports)***

## HABARI MICHEZO

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 10 | 8 | 1 | 1 | 19 | 3 | 25 |
| 2. Kagera Sugar | 11 | 7 | 2 | 2 | 16 | 9 | 23 |
| 3.TZ Prisons | 12 | 4 | 8 | 0 | 14 | 9 | 20 |
| 4. Lipuli | 11 | 5 | 3 | 3 | 19 | 12 | 18 |
| 5. Alliance | 11 | 4 | 5 | 2 | 10 | 8 | 17 |
| 6. Azam | 8 | 5 | 1 | 2 | 8 | 4 | 16 |
| 7. Polisi Tanzania | 10 | 5 | 1 | 4 | 11 | 10 | 16 |
| 8. Mtibwa Sugar | 12 | 4 | 4 | 4 | 10 | 11 | 16 |
| 9. Namungo | 11 | 5 | 1 | 5 | 10 | 11 | 16 |
| 10. Ruvu Shooting | 12 | 4 | 3 | 5 | 9 | 13 | 15 |
| 11. Coastal Union | 11 | 4 | 2 | 5 | 11 | 10 | 14 |
| 12. Mbao | 12 | 3 | 5 | 4 | 9 | 10 | 14 |
| 13. Yanga | 6 | 4 | 1 | 1 | 9 | 6 | 13 |
| 14. JKT Tanzania | 10 | 3 | 3 | 4 | 8 | 10 | 12 |
| 15. Mwadui | 12 | 2 | 6 | 4 | 8 | 11 | 12 |
| 16. Biashara Utd | 11 | 2 | 3 | 6 | 6 | 11 | 9 |
| 17. KMC | 9 | 2 | 2 | 5 | 6 | 10 | 8 |
| 18. Mbeya City | 11 | 1 | 5 | 5 | 7 | 17 | 8 |
| 19. Ndanda | 10 | 1 | 4 | 5 | 6 | 11 | 7 |
| 20. Singida Utd | 12 | 1 | 4 | 7 | 5 | 15 | 7 |

# KILI QUEENS IKIIVA KENYA, MKWASA AIWAZIA AFCON

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA kocha Mkuu wa Timu ya soka ya Taifa ya Tanzania ya Wanawake (Twiga Stars) na Kilimanjaro Queens ya Bara, Boniface Mkwasa, amekitaka kikosi hicho kujipanga na kufikiria kusaka tiketi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Mataifa Afrika (AWC).

**Mkwasa aliwahi kukiongoza kikosi hicho na mwaka 2010 alifanikiwa kukipeleka katika fainali za Kombe la Mataifa Afrika zilizofanyika jijini Johannesburg nchini Afrika Kusini.**

Tangu mwaka huo, Tanzania haijapata tiketi ya kushiriki fainali hizo, lakini timu yake ya Kilimanjaro Queens ikiwa ni bingwa mara mbili mfululizo wa mashindano ya Kombe la Chalenji ambapo leo itashuka tena dimbani kucheza fainali ya tatu kwa kuvaana na Kenya.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkwasa, alisema kuwa timu hiyo ni ya muda mrefu na yenye wachezaji wazoefu, hivyo kwa sasa inatakiwa kupambana na nchi za Afrika Magharibi na si Afrika Mashariki peke yake.

"Nawapongeza kwa kufika tena hatua ya fainali, lakini kwangu ninaamini sasa hivi wajipange kucheza tena michuano ya Afrika, wanastahili kuwa huko, hadhi yao si ya kuishia hapa Afrika Mashariki, huku wameshaonyesha wanaweza, wasonge mbele," alisema Mkwasa.

Aliwataka wachezaji kuongeza bidii katika ligi ili kumpa kocha wao kazi nyepesi ya kuwandaa inapokaribia mashindano mbalimbali.

"Sasa kuna ligi, huko nyuma hatukuwa na ligi na tulicheza Afcon ya Wanawake na Olimpiki, natamani na nitafurahi kuona wakicheza tena mashindano hayo, wanaweza na wasikate tamaa, huwa ninazungumza nao nikipata nafasi kwa lengo la kuwajenga," Mkwasa alisema.

Kilimanjaro Queens iliyoko chini ya Bakari Shime 'Mchawi Mweusi' inatarajia kuwakaribisha wenzao wa Kenya katika mchezo wa fainali utakaochezwa kuanzia saa 10:00 jioni, wakati Burundi itawakabili Uganda kwenye mechi nyingine ya mapema ya kusaka mshindi wa tatu majira ya saa 7:30 mchana.



Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta, akimlalamikia mwamuzi wakati timu yake ya KRC Genk ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Royal Excel Mouscron kwenye mechi ya Ligi Daraja la Kwanza A Ubelgiji, iliyopigwa Uwanja wa Le Canonnier mjini Mouscron juzi. Samatta alifanyiwa mabadiliko 'sab' katika dakika ya 72. **PICHA: MTANDAO**

# *Biashara United yataka tatu za Lipuli*

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu yake kupata sare ya bila kufungana na Mtibwa Sugar, Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, amefurahia matokeo hayo lakini akiahidi kuondoka na pointi tatu katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaofuata dhidi ya Lipuli.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema tangu alipotua katika klabu hiyo, amekinoa kikosi chake kwa siku tano tu, lakini ameanza kuona mabadiliko kwa wachezaji wake.

Baraza alisema anaamini atapata matokeo mazuri katika mchezo dhidi ya Lipuli FC, kwa sababu tayari nyota wake wanaelewa kile wanachotakiwa kukifanya.

"Nimeanza na sare, si mbaya, ilikuwa mechi ngumu lakini wachezaji wangu wamepambana, tulitengeneza nafasi nyingi kipindi cha kwanza, hatukuzitumia, ilikuwa tumalize mechi kipindi hicho, lakini tunatarajia kupata ushindi katika mechi ijayo, nimekuwa nao kwa siku tano, wamenionyesha kuimarika, ni jambo jema na ishara nzuri ya huko tunakoelekea," Baraza alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, aliliambia gazeti hili kuwa mchezo huo ulikuwa na ushindani na mara nyingi Biashara United wamekuwa bora zaidi wanapokuwa nyumbani kwao.

"Ugenini kupata pointi moja ni jambo la kushukuru, haikuwa mechi rahisi, wachezaji wote wamepambana lakini mwisho wa siku hatukuweza kupata mabao, ni sehemu ya mchezo," alisema Katwila.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Simba yenye pointi 25 na imeshuka dimbani mara 10 imeendelea kuongoza wakati Singida United waliocheza michezo 12 na wana pointi saba wanaburuza mkia.

# Walima miwa vitani Kaitaba

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA wa timu ya Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila ameahidi kuendeleza kichapo katika mchezo wao dhidi ya wakulima wenzao wa miwa, Kagera Sugar, watakaocheza leo katika Uwanja wa Kaitaba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema wataingia kwa tahadhari kubwa katika mchezo huo ambao utakuwa mgumu na wenye ushindani.

"Tunaendelea kujifua kwa ajili ya mchezo wetu wa kesho, lengo ni kutoka na pointi tatu,"alisema Katwila.

Hata hivyo, kocha huyo alisema katika mchezo uliopita dhidi ya Biashara United, kuna makosa machache ya kiufundi aloyabaini na kuahidi kutojirudia katika mchezo wa kesho.

"Kuna makosa madogo madogo ambayo nimeyabaini katika mchezo uliopita ninaendelea kuyafanyia kazi ili yasijitokeze katika mchezo wetu ujao,"alisema.

Aliahidi kupambana kwa kila hali ilimradi timu yake isishushuke daraja miongoni mwa timu nne zitakazoshushwa msimu huu.

# Michezo

Jumatatu Novemba 25, 2019

Nipashe




Aubameyang aelezea matatizo ya Arsenal UKURASA 30

MSULI...




Beki wa kulia wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold (kulia) akihaha kumkaba winga wa Crystal Palace kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Selhurst Park juzi. Liver ilishinda 2-1. **HABARI UK. 28**

# Kagere amvaa Okwi, Samatta vs Salah Caf

## Ni katika kinyang'anyiro cha tuzo ya Mchezaji Bora Afrika 2019, pia yumo Mane, Mahrez...

**CAIRO,** MISRI

SHIRIKISHO la Soka Afrika (Caf), limetangaza orodha ya wachezaji wa awali waloingia katika kinyang'anyiro cha kuwania tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka 2019 pamoja na ile ya wachezaji wanaocheza klabu za ndani barani Afrika.

**Mshambuliaji wa kimataifa wa Rwanda na Klabu ya Simba, Meddie Kagere, amechaguliwa katika orodha ya wanasoka wanaowania tuzo ya mchezaji bora wa Afrika mwaka 2019 kwa klabu za ndani.**

Katika kinyang'anyiro hicho, mbali na wachezaji wengine Kagere, atachuana na mshambuliaji wa zamani wa Simba, Mganda Emmanuel Okwi ambaye kwa sasa anaichezea Ittihad Alexandria ya Misri.

Wachezaji wengine watakaochuana na Kagere na Okwi ambaye ameorodheshwa kama mchezaji wa Simba kutokana na mafanikio aliyoyapata msimu uliopita akiwa na Wekundu wa Msimbazi hao, nchi wanazotoka na klabu wanazozichezea zikiwa katika mabano ni Ali Maaloul (Tunisia na Al Ahly), Anice Badri (Tunisia na Esperance), Emmanuel Okwi (Uganda na Simba), Denis Onyango (Uganda na Mamelodi Sundowns), Meddie Kagere (Rwanda na Simba), Ferjani Sassi (Tunisia na Zamalek), Fousseny Coulibaly (Ivory Coast na Esperance), Franck Kom (Cameroon na Esperance) na Herenilson (Angola na Petro de Luanda).

Wengine ni Ismail El Haddad (Morocco na Wydad Casablanca), Jean Marc Makusu (DR Congo na AS VITA), Kodjo Fo Doh Laba (Togo na RS Berkane / Al Ain), Mahmoud Alaa (Misri na Zamalek), Meschack Elia (DR Congo na TP Mazembe), Taha Yassine Khenissi (Tunisia na Esperance), Tarek Hamed (Misri na Zamalek), Themba Zwane (Afrika Kusini na Mamelodi Sundowns), Tresor Mputu (DR Congo na TP Mazembe), Walid El Karti (Morocco na Wydad Casablanca), Youcef Belaili (Algeria na Esperance / Ahli Jeddah).

Aidha, katika kinyang'anyiro cha Mchezaji Bora wa Afrika 2029, majina 30 pia yametangazwa ambapo katika orodha hiyo wachezaji 10 kati ya hao wanacheza soka Ligi Kuu England akiwamo mshindi wa tuzo hiyo misimu miwili iliyopita, Salah.

Kadhalika, wamo wachezaji wenza wa Salah katika kikosi cha Liverpool, Sadio Mane kutoka Senegal na Naby Keita wa Guinea, kuwamo kwao kulitokana na mafanikio waliyoyapata kwa kutwaa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Manchester City, Riyad Mahrez, ambaye aliisaidia Algeria kutwaa Kombe la Mataifa ya Afrika 2019 nchini Misri, ni miongoni mwa wachezaji wa Algeria waliotajwa katika oodha hiyo.

Kipa wa Uganda na Mamelodi, Denis Onyango yumo pande zote, ile ya wanaowania Mchezaji Bora wa Klabu za ndani Afrika na hii ya Mchezaji Bora wa Afrika.

Wachezaji wengine katika kinyang'anyiro hicho watakaochuana na Samatta na Salah nchi na klabu wanazotoka katika mabano ni Achraf Hakimi (Morocco na Borussia Dortmund), Andre Onana (Cameroon na Ajax), Baghdad Bounedjah (Algeria na Al-Sadd), Carolus Andriamatsinoro (Madagascar na Al Adalah), Denis Onyango (Uganda na Mamelodi Sundowns), Eric Maxim Choupo-Moting (Cameroon na Paris Saint-Germain), Ferjani Sassi(Tunisia na Zamalek), Hakim Ziyech (Morocco na Ajax).

Wengine ni Idrissa Gueye (Senegal na Paris Saint-Germain), Ismail Bennacer (Algeria na AC Milan), Jordan Ayew (Ghana na Crystal Palace), Kalidou Koulibaly (Senegal na Napoli), Kodjo Fo Doh Laba (Togo na Al Ain), Mahmoud Hassan "Trezeguet" (Misri na Aston Villa), Mbwana Samatta (Tanzania na Genk), Mohamed Salah (Misri na Liverpool), Moussa Marega (Mali na Porto), Naby Keita (Guinea na Liverpool), Nicolas Pepe (Ivory Coast na Arsenal), Odion Ighalo (Nigeria na Shanghai Shenhua), Percy Tau (South Africa na Club Brugge) pamoja na Pierre-Emerick Aubameyang (Gabon na Arsenal).

Pia wamo Riyad Mahrez (Algeria na Manchester City), Sadio Mane (Senegal na Liverpool), Taha Yassine Khenissi (Tunisia na Esperance), Thomas Partey (Ghana na Atletico Madrid), Victor Osimhen (Nigeria na Lille), Wilfred Ndidi (Nigeria na Leicester City), Wilfried Zaha (Ivory Coast na Crystal Palace) pamoja na Youcef Belaili (Algeria na Ahli Jeddah).

# Kili Stars kundi la kifo Cecafa

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya soka ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), imepangwa katika kundi gumu kwenye mashindano ya kuwania Kombe la Chalenji yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Desemba 7 hadi 19, mwaka huu jijini Kampala nchini Uganda.

Katika droo iliyochezeshwa jana jijini Dar es Salaam na viongozi wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), inaonyesha kuwa Tanzania Bara imepangwa katika Kundi C pamoja na Kenya, Djibouti na ndugu zao Zanzibar maarufu Zanzibar Heroes.

Akitangaza ratiba hiyo, Katibu Mkuu wa Cecafa, Nicholas Musonye, alisema Kundi A litaongozwa na wenyeji Uganda, Burundi, Ethiopia na Eritrea wakati Kundi B linaundwa na wageni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Sudan, Sudan Kusini na Somalia.

Musonye alisema kuwa timu mbili zitakazofanya vizuri katika kila kundi na nyingine mbili bora kutoka kundi lolote, zitatinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ambayo bingwa mtetezi ni Kenya maarufu Harambee Stars ambao walishinda kombe hilo mwaka juzi wakiwa wenyeji wa michuano hiyo.

"Libya waliomba, nchi nyingine pia ziliomba, lakini tukaona mwaka huu tuwaalike DRC (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo), hawa ni majirani zetu," alisema Musonye.

Katika droo nyingine iliyochezeshwa jana ya michuano ya Kombe la Chalenji kwa vijana ya wasichana wa umri chini ya miaka 17, Uganda imepangwa na Ethiopia, Eritrea na Sudani Kusini wakati Kundi B litakuwa na Tanzania Bara, Burundi na Djibouti.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002